ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.

19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi la Fuoni.	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake

41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tano - Tarehe 22 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika: (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam 87

Kupima Virusi vya Ukimwi kwa Shuruti

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza**:-**

Kwa kuwa kupima virusi vya ukumwi VVU ni suala la hiari, na kwa kuwa ugonjwa huo hatari umezidi kuambukizwa na kuua wananchii wengi nchini.

(a) Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kushurutisha watu kupima kwa lazima kwa kuanzia na viongozi wa kisiasa, Serikali na wafanyakazi.

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa kupima VVU kuwe ni moja ya sifa na masharti ya kuomba ajira na kugombea nafasi za kisiasa hapa nchini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 87 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, napenda niungane na maelezo ya Mhe. Mjumbe wa Baraza lako tukufu kwamba UKIMWI bado ni tishio katika nchi zilizo Kusini mwa jangwa la Sahara ikiwemo Zanzibar na bado tunaendelea kupoteza watu wetu kutokana na maradhi haya.

Hata hivyo, pamoja na kutambua ukweli huo, Serikali haijaona haja ya kutoa maamuzi ya kulazimisha watu kupima au kuweka sharti katika kuomba ajira au kugombea nafasi za Uongozi wa kisiasa au Serikalini kutokana na sababu nitakazozieleza katika majibu ya (b).

(b) Mhe. Spika, napenda kulikumbusha Baraza lako tukufu kuwa mnamo mwezi wa Disemba mwaka 2013 Baraza lako tukufu lilipitisha Mswada wa Sheria ya kuweka masharti ya kukinga na kusimamia masuala ya UKIMWI Zanzibar, kulinda na kuendeleza haki za watu wanaoishi au walioathirika na virusi vya UKIMWI na mambo mengine yanayohusiana nayo. Kwa mujibu wa Sheria hiyo Ibara ya 21 kifungu 1, 2, 3 vimeweka zuio la kulazimisha upimaji. Kifungu cha 3 kinaweka msisitizo kwamba hakuna mtu atakayelazimishwa kupima VVU kama sharti la kupata ajira, kuoa au kuolewa, kupata udakhili wa chuo, kuingia au kutoka Zanzibar au kupata huduma mbali mbali. Kwa mantiki hiyo, kupima virusi vya UKIMWI kunabaki kuwa ni suala la hiari kwa muhusika au linakuwa si la hiari pale tu Daktari au Mahakama wanapoamua vyenginevyo kwa mujibu wa (vifungu vya 21 (4) na 22(4) .

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kuwajulisha Wajumbe kuwa kushurutisha upimaji wa VVU kunaendana na hatua za kuwanyanyapaa na kuwabagua watu wanaoishi na VVU na hilo ni kinyume na Sheria na sera za nchi yetu na hata mikataba ya kimataifa ambayo kwa pamoja inamlinda mtu dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote ile.

Sera ya Taifa ya UKIMWI (2006) imeweka miongozo tosha juu ya upimaji wa VVU katika sura ya tatu na inaweka muongozo wa upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa lazima utafanyika pale haki za kibinaadamu na kisheria zitapotokea kuvunjwa. Mazingira yatayolazimisha hatua hii kuchukuliwa ni pamoja na udhalilishaji wa kijinsia na

ubakaji. Mhe. Spika, naomba nisisitize kwamba suala la ajira na kuomba nafasi za kisiasa au uongozi katika Serikali halikuwekewa sharti hilo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia, upimaji wa VVU ni njia mojawapo inayosaidia kupunguza maambukizi ya UKIMWI endapo utakuwa wa hiari. Kushurutisha kupima kutapelekea watu wanaoishi na VVU kujificha na pia kutapelekea ubaguzi wa watu wanaoishi na VVU ambao ni kinyume na Sheria na sera za nchi na Mikataba ya Kimataifa. Hivyo, endapo tuna dhamira ya kweli ya kupunguza maambukizi, basi kila mmoja wetu achukue tahadhari na kuachana na tabia za hatari zinazopelekea maambukizi ya VVU. Serikali kwa upande wake itahakikisha kwamba huduma zote muhimu zinazohusiana na UKIMWI zinapatikana katika hali ya ubora, kwa urahisi na wepesi kwa kila anayehitajia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii tena kumshukuru Mhe. Waziri kwa umakini wake na ni mfano wa Mawaziri katika Baraza hili kwa kujibu maswali ya msingi na miongoni mwa askari wachache wa mwamvuli ambao wanaoweza kumsaidia Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein.

(1) Mhe. Spika, kwa kuwa nchi nyingi zimeamua kuingiza tatizo la UKIMWI katika mitaala ya Elimu, lini wanafunzi wa Skuli zetu za msingi na Madrasa wataanza kuelimishwa wakati gonjwa hilo si la siri?

(2) Mhe. Spika, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha katika Bajeti ya mwaka jana iliyomalizika kuwasaidia watu walioathirika katika maradhi ya UKIMWI hasa ukizingatia dawa wanazotumia za kupunguza makali, kula yao inatakiwa iwe kubwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna umuhimu mkubwa wa masuala ya UKIMWI kuingizwa katika Mitaala yetu ya masomo na naamini katika Mitaala yetu ya Maskuli tayari masomo haya yameingizwa na yanafundishwa, na kwa kweli katika baadhi ya Skuli Binafsi tumegundua hata katika ngazi ya chini kabisa ya Chekechekea basi wanapewa *A, B, C* ya jinsi ya kujikinga na maradhi ya UKIMWI na kuhusu suala lenyewe la maradhi ya UKIMWI.

Kuhusu suala la kuingiza Mitaala hii katika Madrasa ni jambo ambalo linazungumzika vile vile, na kwa sababu Tume ya UKIMWI inafanya kazi karibu na Taasisi zetu za kidini basi tutaona ni jinsi gani linaweza kuingizwa nalo ili litusaidie kwa sababu na huko nako kuna jamii kubwa ya watoto wetu ambao wanapata elimu hiyo.

(2) Mhe. Spika, suala hili ni suala ambalo linataka kujua kiasi gani serikali imewasaidia waathirika wa gonjwa la UKIMWI katika kupata matibabu dawa za kurefusha maisha. Lakini pia kuwasaidia katika suala la lishe na mambo mengine.

Mhe. Spika, kidogo Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba suala la gonjwa la UKIMWI ni suala Mtambuka. Wizara ya Afya inashughulikia katika suala zima la kuwapatia dawa hizi za kurefusha maisha na mambo mengine vile vile yanayohusiana na lishe, na baadhi ya NGO's na Ofisi yetu ina shughuli nzima ya kuratibu masuala haya, na kwa sababu suala hili linahitaji *data* kwa leo hii itakuwa vigumu kumpa jibu hapa, lakini namuahidi kwamba yale yanayohusiana na Ofisi yangu basi tutamletea jibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Nam. 45

Kutorushwa Hewani Hotuba ya Mzee Karume

Mhe. Saleh Nassor Juma– Aliuliza**:**

Kwa kuwa Tanzania tumo katika mchakato wa Katiba, vyombo vingi vya habari vinavyomilikiwa na Serikali, vikiwemo *ZBC* na *TBC1* vimekuwa vikitoa mara kwa mara hotuba ya muanzilishi wa Muungano huo kwa upande mmoja; kwa maana ya Mwalimu Julius K. Nyerere huku vikitupilia mbali hotuba ya Muasisi wa upande wa pili wa Muungano Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, hata zile hotuba zake muhimu za mwisho wa maisha yake.

Je, hiyo ni dharau ya makusudi au ukosefu wa umakini wa vitengo vya kumbukumbu (*Archives)* katika vyombo hivi vya *ZBC* na *TBC1*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) limekuwa mstari wa mbele kutoa habari na matukio mbali mbali yanayohusu Taifa letu yakiwemo ya hotuba za Viongozi, Waasisi wa Muungano na aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji (*ZBC*), limekuwa likitoa hotuba za Marehemu Abeid Amani Karume, kila mara pale panapokuwa na jambo muhimu la Kitaifa kama Sherehe za Mapinduzi, Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kama vile "Kupendana" tarehe 01-5/04/2014 na "Vijana na Siasa" tarehe 26-29/03/2014.

Mhe. Spika, hivyo, siyo sahihi kwamba Shirika la Utangazaji linafanya dharau ya makusudi au ukosefu wa umakini wa vitengo vya kumbukumbu katika vyombo vya *ZBC*.

Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji Zanzibar *ZBC* halina utaratibu wala utamaduni wa kutupilia mbali hotuba za Waasisi wa upande wa pili wa Muungano, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume hata zile hotuba za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mhe. Spika, tunapenda kukuhakikishia kwamba *ZBC* iko makini kwa usimamizi wa kumbukumbu zote zinazohusu matukio muhimu hasa hotuba za viongozi.

Aidha, *ZBC* itaendelea kuzitumia hotuba za Marehemu Abeid Karume na Mwalimu Julius Nyerere kutoa ujumbe wa kuelimisha wananchi wa Zanzibar na Tanganyika kwa jumla kwa manufaa na maslahi ya watu wa Taifa hili la Tanzania.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika...

Mhe. Spika: Samahani kidogo hii kubadilisha makaazi nayo ina tatizo, ukitizama kule kumbe siye. Sasa Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikuombe radhi kwa kubadilisha makaazi.

Mhe. Spika, kwa kuwa mara nyingi mtu hutakiwa apate chakula pale anapokuwa na njaa na kupata maji pale anapokuwa na kiu. Kwa kuwa swali langu la msingi niliulizia suala zima la Hotuba za Muasisi wetu Mzee Abeid Aman Karume zilikosekana sana na kuzipata za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tu katika kipindi chote kile cha Bunge la Katiba.

Kwa kuwa Wajumbe wa Bunge la Katiba wengi waliomo humu wamezaliwa baada ya Mzee Abeid Aman Karume kufariki kwa vile hawakupata hasa ile nia ya Mzee Abeid Aman Karume katika kuidhibiti Zanzibar na kuitetea. Sasa hotuba zake zingekuwepo zingeweza kuwasaidia Waheshimiwa Wajumbe ambao wengi kipindi kile walikuwa wadogo kuweza kujenga misimamo ya kuitetea Zanzibar katika Bunge lile.

Je, kuendelea kusikiliza hotuba za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa upande mmoja peke yake na kuziacha za Mzee Abeid Aman Karume huku zikiwa hazipatikani sana huko si kuwanyima taarifa hawa Waheshimiwa kina Mhe. Jaku Hashim Ayoub walizaliwa karibuni hawa kukosa hoja za kuitetea Zanzibar kule?

Je, kwa kufanya hivyo unakubaliana na mimi kwamba serikali ilifanya makosa na kama ilifanya makosa serikali je, iko tayari kujirekebisha itakapofika Agosti Bunge hili litakaporudi?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, *ZBC* iko makini sana katika suala la kuhakikisha kwamba Hotuba za Muasisi wa Mapinduzi Mzee wetu Abeid Aman Karume wananchi wa Zanzibar wanazisifia na wanazihusudu sana. Kwa hiyo, naomba nimwambie kwamba utaratibu wetu ni kwamba huwa mara

nyingi tunazitoa asubuhi kuanzia saa 12:15 kupitia *ZBC Radio*. Kwa hiyo, katika kipindi kile tumejitahidi sana kuhakikisha kwamba Hotuba za Mzee wetu zinasikika.

Kwa hivyo, ninachomuomba Mhe. Mwakilishi na pia Wawakilishi na pia wananchi wawe na utaratibu wa kuamka mapema baada ya kuswali msilale msikilize redio, watasikia namna ambavyo Mzee wetu alikuwa anatupa mawaidha mbali mbali ambayo kwa kweli hadi leo ni *living instrument* kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa majibu yako ya kusema kwamba *ZBC* iko makini. Lakini nataka kuithibitishia hapa mbele ya Baraza lako hili pamoja na wananchi nje wanaotusikiliza kwamba haiko makini, kwa mfano hai hii leo nafikiri kipindi cha Magazeti hakikutoka.

Je, na kama kinatoka wakati mwengine bila ya wakati baada ya saa 1:30 kinafika mpaka 1:45 ni sababu gani anaweza kutwambia Mhe. Waziri kuwa *ZBC* iko makini?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, suala la kutoka au kutotoka vipindi mara nyengine ni suala la mawasiliano na masuala ya utaratibu mwengine. Bahati mbaya kipindi cha Magazeti tunakiendesha kutoka Studio iliyoko Dar-es Salaam hatukitoi kutoka Studio zilizopo hapa Zanzibar kwa sababu ya wepesi wa upatikanaji wa magazeti pale Dar-es Salaam ukizingatia hapa Zanzibar, na sisi tumeamua kipindi kile kiwe kinapatikana asubuhi mapema.

Sasa mara nyengine hutokea matatizo madogo madogo ya kiufundi ambayo yanasababisha kipindi kile kisipatikane. Lakini katika mageuzi makubwa ya kuweka Studio mpya katika maeneo yetu Pemba na Unguja, pia tumo katika utaratibu wa kuhakikisha kwamba na pale Dar es Salaam tunaweka pia studio mpya ya kisasa ambayo itaweza sasa kutuletea vipindi hivi bila ya matatizo yoyote.

Kwa hiyo tuna mageuzi makubwa *(big reform)* ya kulifanyia Shirika la *ZBC;* na moja ni kujenga studio mpya za kisasa. Tumeanza na Pemba ipo katika hatua ya mwisho, hivi sasa tumeanza pale *Karume House*, lakini baadae tukimaliza hapo tutakwenda pale Dar es Salaam kuhakikisha kwamba maeneo hayo matatu yote ya matangazo kunakuwa na studio za kisasa ambazo zitaweza kutuletea matangazo bila matatizo.

Kwa hiyo huo ndio umakini wetu kwamba pamoja na uzoefu tulionao lakini tumo katika matayarisho ya kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri. Kwa hiyo wananchi waendelee kutuvumilia kidogo baada ya muda mfupi hali yetu itakuwa imetengenea vizuri.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri ametwambia *ZBC* ipo makini, na vile vile katwambia kama magazeti yanatoka Dar es Salaam ndio maana ikawa wakati mwengine yanakatika katika. Lakini hivi karibuni *ZBC* matangazo yake huwa yanakatika. Je, hizo hotuba zitafahamika kweli.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko karibu wiki kwamba *ZBC Television* vipindi vyake vinakatika katika kuanzia siku ya Bajeti ya Serikali. Sasa uchunguzi niliofanya mwenyewe ni kwamba tatizo halipo *ZBC, ZBC* mitambo yake tunayotumia sasa hivi kurushia vipindi ipo vizuri kiufundi. Nilidhani kwamba labda tatizo ni mitambo yetu ya kuunganishia maudhui pale Rahaleo, uchunguzi niliofanya ipo makini. Tatizo liliopo ni kwamba kuna baadhi ya wananchi wanaipata *ZBC* kutoka katika ving'amuzi vyengine.

Sasa wanaotumia ving'amuzi vyengine *link* baina ya ving'amuzi hivyo na *ZBC* ndio vyenye matatizo. Kwa hiyo *ZBC* hatuna matatizo, *Z-MUX* hatuna matatizo. Kwa hiyo nawaomba wananchi watafute ving'amuzi ambavyo ni vizuri vya kuangalia. Wakitafuta ving'amuzi vyengine ambavyo vina matatizo watailaumu *ZBC* kama inakatikakatika kumbe ni ving'amuzi ambavyo bei zao ni dhaifu. Kwa hiyo sisi *ZBC* na *Z-MUX* hatuna matatizo, nawaomba wananchi watafute ving'amuzi ambavyo ni vizuri vitakavyowapatia matangazo yao vizuri.

Nam. 65

Usumbufu wa Kupatikana Vyeti vya Kuzaliwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa katika dunia hii ya sasa sote tunafahamu manufaa na faida ya kuwa na cheti cha kuzaliwa, na hali inayoonesha kwamba wananchi wanapokwenda kuchukua vyeti vya watoto vinakotolewa huwa kuna usumbufu mkubwa.

(a) Je, wananchi hawana haki ya kupatiwa vyeti hivyo.

(b) Wizara itachukua hatua gani hivi sasa kupunguza msongamano wanaoupata wananchi wakati wa kuchukua vyeti vyao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny. Waziri wa Katiba na Sheria) – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Kimataifa pamoja na Sheria zetu za hapa Zanzibar, kila mtoto ana haki ya kusajiliwa. Hivyo mtu yeyote anaweza kupatiwa cheti cha kuzaliwa baada ya kukidhi na kutimiza matakwa ya Kisheria.

Nakubaliana kwamba katika utoaji wa huduma hii, wafanyakazi wetu wanaweza kukosea au kuleta matatizo madogo madogo hapa na pale. Matatizo haya tumeyaona na tumejitahidi kuyarekebisha. Bado tunawaomba wananchi wanapopata matatizo haya basi watuarifu haraka haraka ili tuweze kuyarekebisha.

Mhe. Spika, mtu anaweza kupatiwa cheti cha kuzaliwa baada ya kukamilisha mambo yafuatayo:-

(a) (i) Kuwasilishwa kipande chake (B1) mara tu baada ya kupokea kutoka hospitali au kwa Sheha wake.

(ii) Kujaza fomu ya usajili wa nje ya wakati *(Late Registration)* na kumaliza taratibu zote za kisheria zilizowekwa.

(b) Ni kweli kuna ufinyu wa nafasi ya kutolea huduma katika Afisi zetu za Vizazi na Vifo, hasa tukizingatia kwamba jengo linalotumika hivi sasa halipo katika mfumo wa utoaji huduma kwa watu wengi kwa wakati mmoja. Hata hivyo, ili tuondokane na tatizo hilo Wizara ipo katika hatua za ukamilishaji wa jengo la Wizara ambapo mara baada ya kukamilika kwake, Idara ya Vizazi na Vifo wataweza kupatiwa nafasi ya kutosha na kufanikisha kutoa huduma kwa wananchi bila ya kuwepo msongamano na usumbufu mwengine wowote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri ya kusikitisha naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, inasikitisha sana, ni lini Zanzibar itaingia katika utaratibu wa kutoa huduma za mipango badala ya kubahatisha. Kwani mtu anapofuata cheti karibu wiki mbili nenda rudi, nenda rudi, wakati taratibu zote zimekamilika.

La pili, kama kuna jengo, jengo ni finyu. Kwa nini tusiweke mabenchi au magogo ya minazi pale badala ya watu kuwa wanasukumana katika *corridor* zile.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny. Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Spika, mimi nimejibu kwamba tatizo ni ofisi. Lile eneo ambalo tulikuwa pale Mambo Msiige tumewekwa kule ambako pana benki ya zamani kwa kweli hali pale mazingira si mazuri. Tukubaliane kwamba Serikali imeliona hilo na ndio maana tukatoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa jengo kubwa la kisasa. Nadhani kama Mhe. Mwakilishi halijui

basi pale Polisi Mazizini upande wa pili huku kuna jengo moja kubwa, lile ndio jengo ambalo litakuwa la Wizara ya Katiba na Sheria na litakuwa na nafasi pana kwa ajili ya shughuli hizi.

Kwa hiyo hatutaweka magogo ya mnazi wala mabenchi, tutakuwa na maeneo mazuri kwa wananchi wetu kupata huduma na tutahakikisha kwamba sasa tunaondokana na utaratibu ule wa zamani, tunakwenda kwa utaratibu wa kileo wa kutumia kompyuta na mtandao katika kuhakikisha suala hili linakwenda vizuri, kwa haraka na kwa uhakika.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza kwamba Serikali imepanga utaratibu mzuri wa kuimarisha Ofisi za Usajili wa Vizazi na Vifo katika mawilaya ili kuona kwamba msongamano unapungua katika ofisi kuu pale ya kupokea vyeti Mambo Msiige. Ni lini Serikali itamalizia wilaya nyengine ambazo hazina ofisi hizi, ofisi hazijaimarishwa kwa kupokea vyeti hivi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny. Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Spika, kwanza Wizara inapokea pongezi zake za namna ambavyo tulivyojiandaa kuhakikisha kwamba tunakamilisha au tunajitayarisha katika kujenga ofisi za kisasa za vizazi na vifo katika wilaya zetu.

Mhe. Spika, naomba kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba Wizara inaweka mipango mizuri zaidi ya kuona kwamba kwanza baada ya kukamilisha jengo letu hapa kutakuwa na kitengo maalum cha mtandao ambao utaziunganisha Ofisi za Wilaya na ofisi yetu iliyopo hapa Mazizini kuona kwamba shughuli hizi zinafanyika kwa wakati mmoja ili kuokoa muda na wakati. Sasa ni kweli kuna baadhi ya wilaya hazijakamilisha, mfano Wilaya ya Wete na wilaya nyengine. Wilaya ya Wete tuna tatizo hatujapata nafasi na tukipata nafasi tutakamilisha, na wilaya nyengine ambazo zimebakia kukamilisha basi katika mwaka huu wa fedha tutahakikisha kwamba tumetenga fedha maalum kuhakikisha kwamba ujenzi huu unakamilika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu cheti cha kuzaliwa ni haki ya kila mtu. Na kutokana na bahati mbaya kuwa katika nchi hii hivi sasa tunao wananchi wengi mpaka wazee, kwa sababu ya wazee wao kutowakatia vyeti vya kuzaliwa hapo mwanzo hawana vyeti vya kuzaliwa na wanahangaika kutafuta vyeti vya kuzaliwa. Wanajaza fomu na baada ya kujaza fomu na kukamilisha kila kitu hutakiwa kulipa shilingi 32,000 ambazo hawazidiriki. Hivyo kwa umuhimu wa vyeti hivi na hasa kuwapa wananchi haki ya kutumia demokrasia yao hata katika uchaguzi. Haoni kuwa Mhe. Waziri wakati umefika wa kuwa wazee kama hawa ama kuondolewa kabisa malipo haya au kupunguziwa kwa kiasi ambacho watu wataweza kulipa ili na wao wapate vyeti vyao na kutumia demokrasia yao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny. Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna baadhi ya watu wengi ambao wapo nchini mwetu lakini wazazi wao hawakuwahi kuwakatia vyeti vya kuzaliwa. Hili tumeliona na ndio maana Serikali ikaweka utaratibu wa kuwasajili wale ambao hawakuwahi kukatiwa katika ule utaratibu wa *Late Registration*. Hili linafanyika makusudi katika kuwapa haki wale ambao hawakupatiwa nafasi huko nyuma.

Mhe. Spika, pia naomba nikubaliane naye kwamba yapo malalamiko ya wananchi kuwa shilingi 32,000 zilizowekwa ni nyingi. Malalamiko hayo ni ya kweli Wizara imeyapokea. Kwa hiyo ninachomuomba Mhe. Mwakilishi ni kwamba rai yake tumeipokea na tunaifanyia kazi na hatua yoyote ambayo itafanyiwa kazi basi Baraza lako tukufu Mhe. Spika, tutaweza kulijulisha.

Nam. 35.
Baadhi ya Maeneo ya Muyuni Kukosa Huduma ya Umeme

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Jimbo la Muyuni) – Aliuliza**:-**

Huduma ya umeme imekuwa muhimu katika maisha ya wananchi kwa vile sasa huduma hiyo imekuwa kichocheo cha maendeleo ya wananchi kwa shughuli mbali mbali za kujiingizia kipato. Licha ya ukweli huo, bado kuna maeneo ya Jimbo la Muyuni ambayo huduma hiyo haijasambaa vya kutosha.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kusambaza huduma hiyo katika maeneo ya Jimbo la Muyuni ili kutoa fursa kwa wananchi kupata maendeleo ya haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, azma ya Serikali ya Mapinduzi ni kupeleka umeme katika vijiji vyote viliopo Zanzibar yaani Unguja na Pemba. Hivyo, tunamuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane ili kuvitambua vijiji vyake vilivyomo katika jimbo ambavyo havijapata huduma hiyo na tuweze kuviingiza katika Bajeti zijazo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kusikitisha naomba nitoe masikitiko yangu kwako Mhe. Spika pamoja na Mhe. Naibu Waziri. Suala la msingi halifahamiki kuimarisha huduma, naona huduma hazipo. Mimi nimesharipoti mimi mwenyewe binafsi kama Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kwa Mkurugenzi, kuna nguzo zimeanguka Pete zinahatarisha maisha mbali ya wananchi wenyewe na hakuna hatua waliyochukua. Je, Mhe. Naibu Waziri unatoa kauli gani kuhusiana na suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme lengo na madhumuni makuu ni kuimarisha huduma hii. Kwa hiyo kama kuna tatizo katika kijiji kimoja ndani ya jimbo lake aidha la kuanguka nguzo za umeme au kuwa na nguzo mbovu, basi tutajitahidi kulishughulikia tatizo hilo na namhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba suala hilo tutalisimamia na tutaliweka sawa si muda mrefu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, umeme ni chachu ya maendeleo katika vijiji na tunashukuru vijiji vingi sasa hivi vimepata kutiliwa umeme huo, lakini wananchi wengi wa vijijini uwezo wao ni mdogo. Je, Shirika linaweza likawakopesha wananchi kutiliwa umeme na halafu wakalipa kidogo kidogo ili lengo la Serikali likaweza kutumika sawa sawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuhakikisha kwamba wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba wanapata mafanikio makubwa na kuitumia huduma hii ya umeme. Kwa hiyo Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme inao utaratibu wa kuwakopesha wananchi huduma hiyo kwa kuwaunganishia ndani ya nyumba zao na kulipia nusu ya gharama ya huduma hiyo. Kwa hiyo namuomba Mwakilishi kama wapo wananchi wake ambao wanahitaji huduma hiyo basi sisi tupo tayari kuwasaidia katika njia hiyo ya mkopo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwaondoshea wananchi tatizo la maji safi, umeme pamoja na mambo mengine. Serikali ya Awamu ya Sita ilijitahidi sana kuueneza umeme katika vijiji vyetu vya Unguja na Pemba. Na nia ya Serikali ni kumaliza tatizo hilo la umeme kwa vijiji vyote. Sasa je, Mhe. Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya vijiji Serikali bado ile azma yake haijakamilisha ya kuwapelekea umeme. Na kwa kuwa wananchi wa vijiji vyetu ni maskini. Ni lini Serikali ya Awamu ya Saba itaendeleza pale ilipoacha Serikali ya Awamu ya Sita kuwamalizia vijiji vile ambavyo wananchi hawajapata umeme ili na wao wafaidi matunda yao ya Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Na je, kama Serikali haitafanya hivyo ikawa mpaka wananchi wachange pesa ndio wawapitishie vijijini. Haioni kama baadhi ya vijiji ambavyo havijapata umeme haiwatendei haki.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa vizuri katika suala zima la kusambaza huduma hii ya umeme. Lakini vile vile Serikali ya Awamu ya Saba imefanikiwa kwa kiwango kikubwa na bado inaendelea kusambaza huduma hiyo ya umeme katika vijiji kama nilivyoeleza hapo awali. Kwa hiyo namhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba bado lengo la Serikali ni kuhakikisha vijiji vyote vya Zanzibar kuvipelekea huduma hiyo. Kwa hiyo tumejipanga vizuri na tunaomba Mhe. Mwakilishi avute subra. Kwa vile vijiji ambavyo bado havijapata huduma hiyo basi tutahakikisha huduma hiyo itapatikana kadri ya vile hali ya uwezo itakavyotuwezesha.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.Pia nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Seif Ali Iddi kwa kutuletea hotuba hii ya makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2014/2015. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nikupongeze na wewe kwa umahiri wako katika kuliendesha Baraza lako hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, jana wakati tunaendelea na kikao chetu hapa, ulitupa nasaha na maelekezo, na wewe mwenyewe ukasema kwamba ni muumini wa umoja na mshikamano. Kwa kweli tukupongeze sana, kwa sababu uliyoyasema ni ya kweli, ni muumini wa umoja katika nchi yetu na mshikamano wa Tanzania wote. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba mimi pia ni muumini wa umoja, upendo na mshikamano wa Wazanzibari wote na Watanzania wote kwa ujumla, lakini nichukue fursa hii kuwaomba viongozi wenzangu, Waheshimiwa wenzangu tuungane na wewe na Rais wetu katika kujenga umoja na mshikamano, kwa sababu sote ndio vioo vya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Mhe. Spika, bila ya sisi viongozi wetu kuwa mfano kwa wananchi ambao ndio waliotuchagua, ndio hali ya mtafaruku inatokezea katika nchi yetu. Mhe. Spika, bila ya kuwa na amani na utulivu katika nchi yetu, bila ya kuwa na umoja na mshikamano, maendeleo ambayo viongozi wetu wanajipiga kifua katika kuwaletea Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla hayatopatikana.

Ni wajibu wetu sote tushikamane, tusibaguane, tuwe kitu kimoja. Wazanzibari wa Unguja na Pemba na kwa Watanzania kwa ujumla. Kwa sababu tutapoleta mgawanyiko kwa Wapemba na Waunguja, itakuja kwa Wazanzibari na Watanzania Bara, haileti picha nzuri kuona kwamba sisi viongozi tunaanza kuwabagua wananchi.

Mhe. Spika, ninayasema haya kwa sababu kwa matokeo ambayo yanatokea huko nje, kumekuwa na kubaguana, matusi, kuzomewa kwa baadhi ya viongozi wetu waliomo humu ndani hususan katika matokeo ambayo yaliyopita hivi punde kupitia mchakato mzima wa Katiba. Sitaki nizungumzie suala la Katiba lakini ninasema kwamba si jambo jema kwa viongozi kusimama ndani ya viriri, kuwaongoza au kuwashajihisha wananchi kuwatukana, kuwakebehi, kuwazomea viongozi ambao wamechaguliwa na wananchi.

Mhe. Spika, juzi nikiwa katika maeneo ya Kwahajitumbo pale Msikiti wa Biziredi, nilipita lakini kauli ambazo zilizotoka pale kwa wananchi ambao hawapendi amani na utulivu tulionao, umoja na udugu tulionao. Kwa sababu Mhe. Spika, sote ni Wazanzibari wa kuzaliwa, wa wazee wetu na mababu zetu. Sote ni wazalendo kindakindaki, ni Watanzania; tuna haki, kila mmoja ana haki yake, kila mmoja ana maamuzi yake mbali ya kufuata maamuzi au maelekezo ya chama chake.

Mhe. Spika, nimeyasema haya kwa hali halisi inavyoendelea huko nje, hali sio nzuri, tunaanza kubaguana. Hii italeta ishara mbaya huko mbele tunakokwenda. Niwaombe sana viongozi wetu, niwaombe sana viongozi wenzangu tuepukane na jazba za kisiasa, tuepukane na jazba za kubaguana, tuwe wamoja, tushikamane tujenge nchi yetu, tuimarishe uchumi wa nchi yetu. Tuendeleze umoja ambao tupo nao, kwa sababu bila ya amani, upendo na udugu hatutofika kule tunakotarajia. (*Makofi*).

Mhe. Spika, yalisemwa mengi wakati nilipozungumza Watanzania na Wazanzibari tuache kubaguana kabila zetu, udini wetu, unasaba wetu; kwa sababu sote ni wamoja wa damu moja. Hata ukiangalia ndani ya Baraza lako hili tukufu, basi utakubaliana na mimi kwamba sote ni ndugu wa damu moja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, inapotokea hali ya mtafaruku huko mitaani, mwisho wa uvumilivu utafikia kikomo. Kwa sababu mimi nimechaguliwa na wananchi wanaonipenda, wanaoniamini, wanaonithamini. Hawatojisikia vizuri mimi au mwenzangu yeyote mwengine kuanza kubaguliwa, kuanza kutukanwa, kuanza kuzomewa. Hii ni ishara mbaya kwa sisi wenyewe Wazanzibari kuanza kutukanana na kuanza kubaguana. Kwa hivyo ninasema chonde chonde, tuanze kujenga umoja na mshikamano wetu sisi humu viongozi, tuwaelekeze wananchi wetu, wapiga kura wetu ili tujenge mustakabali wa nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo nije katika suala zima la mchakato mzima aliozungumza kaka yangu Mhe. Mohammedraza Hassanali kuhusiana na fedha milioni 71 za *Mapinduzi Cup*. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Mohammedraza Hassanali kwa uzalendo wake, kwa kuipenda nchi yake katika kutoa fedha zile ili kuendesha mashindano yale.

Mhe. Spika, aliyoyasema ni ya kweli kwamba fedha zile ambazo zilikopwa, sisi wengine kwa kweli tulikuwa hatujui, mimi nilikuwa sijui, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Ndugu Mirza alikuwa hajui, na Mjumbe mwenzetu Bwana Farouk Karim alikuwa hajui suala hili. Mimi kweli nilikutana na Mhe. Mohammedraza Hassanali *airport* na nikamwambia Mheshimiwa mbona mara hii unatutupa mkono au kwa vile kumetokea kutokuelewana ndio hutaki kutuunga mkono. Akasema mbona nimeshatoa milioni 10 na tayari jana nimetoa milioni 71 nimempa Mwenyekiti wenu. Yaani Kaimu Mwenyekiti Bi. Sherry.

Nikamwambia mimi sina habari lakini ninakwenda Dar es Salaam nikirudi nitalifuatilia suala hili. Kweli nililifuatilia Mhe. Spika, na nikahoji katika kikao kwa nini sisi Wajumbe wengine mumekwenda kukopa pesa nyingi kama hizo bila ya sisi kupewa taarifa. Sasa matumizi ya fedha zile zilivyotumika na maombi ya fedha zile zilivyoombwa, kweli ilikuwa ni tofauti, kwamba wamekwenda kulipa madeni mengine kuliko vile zilivyoombwa.

Mhe. Spika, lakini nimshukuru sana na nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye aliyekuwa mlezi wa kamati ile na ndiye aliyechukua dhamana ya fedha zile. Kitendo ambacho alichokuwa anafanyiwa Mhe. Mohammedraza Hassanali au maneno aliyokuwa anaambiwa yamefika aliyoyasema. Waswahili wanasema, "*baniani mbaya kiatu chake dawa*". (*Makofi*).

Sasa laiti kama wenzangu wangekubaliana na ushauri wangu ambao niliokuwa ninawapa yasingefika haya. Mhe. Mohammedraza Hassanali ni haki yake fedha zile. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye analifahamu vizuri suala hili Mhe. Mohammedraza Hassanali apewe fedha zake tuondokane na maneno ya kashfa.

Mhe. Spika, sasa kulikuwa na fungu ambalo la milioni 150 ambazo fedha zile zilikuwa zisaidie katika kuendeleza michezo kwenye sherehe za Mapinduzi. Lakini la kushangaza au la kusikitisha, fedha zile hazikupatikana, zilizopatikana ni chache sana takriban hata milioni 30 hazifiki. Laiti kama fedha zile zingepatikana hii aibu ya Mhe. Mohammedraza Hassanali isingefika ndani ya Baraza lako Mhe. Spika.

Sasa sielewi ni tatizo gani kwamba fedha hazikupatikana, kwa sababu Mhe. Spika, katika michezo ambayo yote iliyofanywa wakati wa sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi, mchezo ambao ulikuwa unaingiza *income*, yaani unaingiza fedha ni mchezo mmoja tu wa mpira wa miguu. Michezo mengine yote ilikuwa inatumia tu haiingizi. Kwa hivyo ndio tatizo lililoleta kwamba matumizi yalikuwa ni makubwa, fedha ni kidogo, ndio ikafikia hatua hii ya Mwenyekiti wetu na wenzake kwenda kwa Makamu wa Pili wa Rais kumuomba Mhe. Mohammedraza Hassanali aazimwe pesa zile ili kwa kutegemea zile fedha milioni 150 zitakapopatikana kuja kulipwa Mhe. Mohammedraza Hassanali.

Mhe. Spika, kwa hivyo niombe sana na nimuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha kwamba lile fungu ambalo limetengwa, fedha zile zipatikane ili Mhe. Mohammedraza Hassanali alipwe pesa zake. Tunamtegemea na yeye mwenyewe jana kasema kwamba yupo tayari wakati wowote kusaidia nchi yake kwa jambo lolote ikiwa la michezo ikiwa la maendeleo.

Mhe. Spika, kuja jambo ambalo nilisema nilizungumze leo hapa. Mhe. Spika, kumetokea ugonjwa wa dharura au ugonjwa wa ghafla, unaitwa ugonjwa wa dengue. Sasa ugonjwa huu umeanzia kwa wenzetu Tanzania Bara pale Dar es Salaam na ni ungojwa ambao unahatarisha maisha ya binadamu. Sasa wenzetu wameanza na mikakati ya kuupiga

vita ugonjwa kwa kuanza kupulizia madawa kwenye magari yanayokwenda mikoani na maeneo ambayo ni nyeti ambayo yanasababisha kwa kuzalishwa kwa mbu yule ambaye anasababisha ugonjwa ule.

Sasa kwa vile Zanzibar tunatumia vyombo vya baharini ikiwemo boti, ndege, majahazi. Sasa ni vyema kwamba serikali kwa sababu nimelizungumzwa hapa kwenye hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuweza kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusaidia kupiga dawa katika vyombo ambavyo vinakuja Zanzibar.
Taarifa ambazo zimeshatolewa na Wizara ya Afya kwamba ugonjwa huu kwa kweli umeshaingia Zanzibar na watu wawili watatu wameshapatikana na ugonjwa huu. Ili kuweza kupunguza kuenea kwa ungojwa huu ndani ya nchi yetu hii kwa visiwa vyetu hivi viwili vya Unguja na Pemba, ni vyema kwamba serikali ikahakikisha kwamba vyombo vile ambavyo vya baharini, boti, meli ambazo zinasafirisha wananchi wetu pamoja na ndege, kuhakikisha kwamba vinapigwa dawa ili kuepukana na janga hili ambalo limetokea.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Maafa. Niipongeze sana Idara ya Maafa kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya...

Mhe. Spika: Unazo dakika 5 kumalizia hotuba yako.

Mhe Nassor Salim Ali: Kazi ambapo hutokea maafa mbali mbali katika nchi yetu hii.

Mhe. Spika, lakini nitoe malalamiko yangu kwa wananchi wangu ambao wamepatikana na maafa kipindi cha mvua kubwa hapa Zanzibar. Wakati tukiwa Dodoma wananchi wangu wa Jimbo la Rahaleo Shehia ya Makadara walipatwa na maafa kwenye nyumba zao. Ninawashukuru Idara ya Maafa walikwenda kuwaona lakini mpaka leo hakuna chochote kile walichosaidiwa.

Mimi nikiwa kama Mwakilishi wao, nimeonana nao, nimeweza kuwachangia kile ambacho nilichokuwa nacho, niliwachangia takriban shilingi 1,500,000 lakini hichi hakitoshi. Niiombe Idara ya Maafa yanapotokea maafa waende kuangalia na kuwasaidia wananchi, sio Jimbo la Rahaleo au Makadara tu na sehemu nyengine popote panapotokea maafa. Kwa sababu wananchi wetu hali zao ni duni, maskini, hawana uwezo, inapotokea mambo kama haya ya kimaafa ambayo yanaletwa na Mwenyezi Mungu, sisi binadamu tusaidiane, serikali iwasaidie wananchi wetu. Isiende tu kuwaangalia kuwapiga porojo na kuondoka, hapana, tuwasaidie kwa hali na mali. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa vile muda wangu umekwisha niunge mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Niendelee kusema kwamba ubaguzi, utengano, ushawishi wa kutukanana, kuzomeana ukome kwa nchi yetu hii. Tuwe wamoja tusibaguane, sote ni wamoja, sote ni Watanzania, isiwe huyu ni Mnyamwezi, huyu Mmakonde, huyu Mpemba; sote ni wamoja tuwe kitu kimoja, tujenge nchi yetu, tujenge Tanzania yetu na niendelee kuunga mkono serikali mbili. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana. Ni zamu yake sasa Mhe. Kazija Khamis Kona na baadae Mhe. Omar Ali Shehe wakati Mhe. Ali Salum Haji anajitayarisha.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwa kuanza mchango wangu naanzia na migogoro ya ardhi. Mhe. Spika, kitabu cha Mhe. Waziri katika ukurasa wa 19 kinaeleza serikali bado inaendelea kufuatilia ufumbuzi wa kudumu. Kuhusu suala la migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa hali hii inatokana na tabia ya wananchi na baadhi ya viongozi kuuza au kukodisha ardhi bila ya kufuata sheria za nchi.

Sasa Mhe. Spika, mimi niiombe serikali, nadhani inawajua baadhi ya viongozi ambao wanasababisha migogoro hii ya ardhi pamoja na wananchi wake. Sasa mimi naiuliza hii serikali inashindwa na nini kuwachukulia hawa watu hatua ili waondokane na tatizo hili la migogoro ya ardhi. Kama haichukuliwi hatua Mhe. Spika, migogoro hii itaendelea na kuendelea tu!

Mhe. Spika, nikiendelea hapo hapo katika migogoro ya ardhi, katika kitabu chake kinasema, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari amelitolea tamko, amelitolea maagizo mara kadhaa suala hili kwa kuwataka viongozi na wananchi kutojihusisha na mambo yoyote yanayopelekea kuwa na migogoro ya ardhi.

Sasa Mhe. Spika, suala lolote ukilisema kwa maneno bila ya vitendo, halifiki muafaka. Sasa hapa ili tuondokane na migogoro ya ardhi, serikali ichukue juhudi kubwa ili kuhakikisha wale wote ambao wanasababisha hii migogoro ya ardhi wanachukuliwa hatua za kisheria, ili migogoro ya ardhi iondoke au ipungue katika nchi yetu.

Mhe. Spika, bajeti ya mwaka jana 2012/2013 kama sijasahau Mhe. Waziri kitabu chake kilieleza ya kwamba migogoro ya ardhi, baadhi ya migogoro imetatuliwa. Sasa mimi nataka kujua kwa mwaka huu wa 2013/2014 ni migogoro mingapi iliyotatuliwa, ili na sisi tujue na ni maeneo gani na maeneo gani ya migogoro hiyo iliyotatuliwa.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika kitabu cha Mhe. Waziri kinasema kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, katika ukurasa wa 14. Mhe. Spika, kama kweli serikali iko tayari kisawa sawa kuwawezesha wananchi wake kiuchumi basi iwe tayari. Kwa sababu Mhe. Spika, tunawawezesha wananchi, lakini hatuwajengei mazingira mazuri.

Kwa mfano, wananchi labda tunawapa mifugo ya vifaranga, lakini tukiwaangalia wale wananchi hata yale maeneo ya kuwekea ile mifugo yao hayaridhishi. Sasa hapa tunamuwezesha mwananchi au tunamkomoa mwananchi wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, niiombe serikali inapowawezesha wananchi hasa kwa kuwapatia mifugo, basi wawaangalie wananchi je, tayari wameshajiwezesha sehemu ya kuweka mifugo yao, ndipo tuwawezeshe wananchi kuwapa vifaranga au mifugo ya kuku.

Mhe. Spika, nchi yetu inategemea utalii sana kwa kukuza uchumi wetu, lakini Mhe. Spika, bado serikali haijajipanga kwa hili. Kwa sababu gani nikasema hivyo Mhe. Spika. Kwa sababu nchi yetu huwa kunatokea mambo mbali mbali ambayo yanatahadharisha ndani ya nchi yetu. Hutokea wahalifu mbali mbali katika sehemu za mahoteli. Sasa nataka niiulize serikali imejipanga vipi na hili ili kuhakikisha uchumi wetu unakuwa katika sekta ya utalii.

Mhe. Spika, pia naomba nipewe ufafanuzi kuhusu huu utalii kwa wote; kwa sababu Mhe. Spika, utalii kwa wote ninavyotafsiri mimi ni yale mahitaji yanayohitajika katika mahoteli, wananchi wetu ndio wapate kupeleka mfano bidhaa zao, kama kilimo, biashara na mambo mengine. Lakini serikali bado iko nyuma haijawawezesha wakulima wetu kulima kilimo kilicho bora, ili bidhaa zao zikawa zina kiwango zikaweza kupelekwa katika mahoteli yetu. Je, serikali hapa itawaambia vipi wananchi wetu ili na wao wafaidike na huu utalii kwa wote.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu miundombinu. Hapa imezungumzwa miundombinu ya barabara, sekta ya huduma za kiuchumi nayo nadhani huwa inachangia zikiwa barabara zetu nzuri. Lakini Mhe. Spika, barabara ya kutokea Malindi hadi Mkokotoni ukifika sehemu za pale Kitope na kuendelea kuna madaraja ambayo huweza kusababisha hatari kubwa, na sisi tunajivunia nchi yetu kiuchumi kupitia utalii. Sasa mtalii unampitisha maeneo yale, anaona hali halisi ya madaraja yale yalivyo. Hii Mhe. Waziri si aibu hii, hebu tutengenezeni haya madaraja ili yasije kutuletea athari ya baadaye. Mhe. Spika, madaraja yako hali mbaya na huenda yakatuletea athari kubwa, Mwenyezi Mungu tumuombe asitujaalie yakafikia hayo.

Mhe. Spika, pia barabara yetu ya Kijini Mhe. Waziri naona kila siku barabara ile tunapigwa kalenda tu. Sasa niiombe serikali pamoja na kwamba imetusaidia kututilia fusi, lakini fusi lile sasa hivi limeshachimbika chimbika, niiombe serikali nayo iione barabara ile ili wananchi wetu wafaidike na matunda ya serikali yao. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru na naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Kazija Khamis Kona. Nimkaribishe basi Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Ali Salum Haji ajitayarishe na baadaye Mhe. Asha Bakari Makame.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili angalau na mimi niweze kuzungumza machache kuhusiana na bajeti hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, nakushukuru na pia nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uwasilishaji mwanana kabisa wa hotuba yake hii, naamini alijipanga katika kuiwasilisha hotuba yake.

Mhe. Spika, Makamu wa Pili wa Rais, wizara hii tunayoijadilia msimamizi wake mkubwa ni Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, jukumu lake kubwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwanza ni usimamizi wa wizara hii. Lakini pili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa mujibu wa Katiba yetu ndiye mshauri wa Mhe. Rais pamoja na Makamu wa Kwanza. Vile vile Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye ni Msimamizi Mkuu wa shughuli za serikali katika Baraza letu la Wawakilishi.

Kwa msingi wa majukumu ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tutabaini kuwa ni muhimili katika uendeshaji wa serikali hii yeye ni muhimili mkubwa. Utendaji, uwajibikaji pamoja na utekelezaji wa majukumu ya serikali yanategemeana sana na umakini wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, naomba nianze na Baraza la Wawakilishi. Chombo hiki Mhe. Spika, ni kama alivyosema Mhe. Aboud Jumbe, muasisi wa chombo hiki kwamba ndio ngome ya wananchi. Wananchi wa Zanzibar ngome yao ndio hii Baraza letu la Wawakilishi, lakini uwepo vile vile wa chombo hiki ni kielelezo cha utekelezaji wa dhana ya Utawala Bora katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha miaka minne kwa kweli mimi bado nasikitika kwamba kumekuwa na kusuasua sana katika utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na chombo hiki kwa serikali, ama wakati mwengine kumekuwa hakuna kabisa utekelezaji wa majukumu. Serikali imekuwa kwa mara nyingi na kwa makusudi kabisa ikipuuza sana utekelezaji wa maagizo ya chombo hiki. Kwa kufanya hivyo Mhe. Spika, tunabaini kuwa ni udhalilishaji na wakati mwengine ni uvunjifu wa Katiba yetu, kwa sababu serikali kwa mujibu wa katiba yetu inawajibika katika chombo hiki.

Kwa hivyo, moja katika kosa ambalo tunalo na hili nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama yeye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za serikali katika Baraza hili, ajitahidi na awe makini sana ili kuona kwamba yale maagizo yote yanayotolewa na chombo hiki yanatekelezwa. Kwa kufanya hivyo itaonekana kwamba tuko katika Utawala Bora na tunaendelea na demokrasia.

Mhe. Spika, tulishuhudia katika kamati nyingi, Kamati Teule pamoja na maamuzi mengine, hadi leo maamuzi yale hayajatekelezwa. Ripoti nyingi za Kamati Teule hadi sasa hazijatekelezwa na bahati mbaya zaidi serikali haina ule utamaduni wa kurudi katika chombo hiki na kutoa maelezo juu ya utekelezaji.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakapokuja kufanya majumuisho, atuelezee yale mambo yote ambayo hadi sasa yametekelezwa na yale yote ambayo hayajatekelezwa kwa nini hayajatekelezwa, na atupe sababu ya kwamba kwa nini maagizo yale ya chombo hiki kwa kweli hayajatekelezwa.

Mhe. Spika, chombo hiki pia kama tunavyofahamu kwamba katika nchi yetu tuna chombo cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mdhibiti kazi yake kubwa ni kuandika ripoti, lakini mwisho wa siku ripoti zile huletwa Barazani kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Baraza nalo hukabidhi Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuzifanyia kazi. Tutaona kwamba kamati zetu za Baraza ikiwemo Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali, tuna jukumu na tuna umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kwamba kazi zetu zinakwenda kwa mujibu wa tulivyopangiwa. Katika nukta hiyo, naomba nirudie tena kusisitiza umuhimu wa kuongeza bajeti katika Baraza la Wawakilishi pamoja na kamati, kwa sababu kamati ndio zenye kazi na jukumu maalum la kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali kwa mujibu wa matakwa ya Katiba yetu.

Mhe. Spika, naomba na nirudie tena kwa mara nyengine kwamba kuna kila haja na katika nukta hii naomba nikushukuru Mhe. Spika, ofisi yako pamoja na ofisi ya Katibu wa Baraza, kwa namna mnavyoipa muda wa kutosha sasa Kamati yetu ya *PAC*. Naomba nisisitize na nirudie kwamba kuna umuhimu, kwa sababu Mdhibiti sasa ukaguzi wa mahesabu unaingia katika hatua nyengine. Kwa hivyo, ikiwa Mdhibiti ataingia katika hatua nyengine, ndivyo Kamati ya *PAC* nayo inatakiwa ijihakikishe kuwa inaelekea katika hatua hizo, hasa za kiutaalamu.

Mhe. Spika, kulikuwa na maombi ya muda mrefu kwa Kamati ya *PAC* kupatiwa mafunzo na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alilichukua jukumu hili, lakini hadi sasa kwa kweli tunaona ni kimya hakuna majibu yoyote, na kwa kufanya hivyo Mhe. Spika, kamati haiendani na kasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Tunaposisitiza mafunzo katika kamati zetu na hasa Kamati ya Kuchunguza Mahesabu ya Serikali ni kitu cha lazima na ni jambo ambalo lina umuhimu mkubwa sana.

Mhe. Spika, naomba sasa niende kwenye Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi ni chombo kilichopo kwa mujibu wa Katiba yetu na kimepewa jukumu la kuratibu na kusimamia chaguzi, kuanzia uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, uchaguzi wa Wawakilishi, pamoja na Waheshimiwa Madiwani. Mwakani tukijaaliwa tutakuwa na uchaguzi mkuu mwengine. Chombo hiki kwa umuhimu wake, kinatakiwa kiwe ni chombo ambacho kimejaa watendaji waadilifu pamoja na Tume yake.

Vile vile ni chombo ambacho kinatakiwa watendaji wake pamoja na Tume yenyewe iwe na umakini mkubwa. Chombo hiki kikiwa na watu waadilifu na walio makini basi kitapelekea nchi yetu kuwemo katika hali ya usalama; na tukisema amani na usalama maana yake ni kusema kwamba maendeleo yako karibu. Lakini chombo hiki kikiwa na watendaji wababaishaji na waliokuwa sio waadilifu Mhe. Spika, ni kusema kuwa nchi hii na nchi nyingi duniani huingia katika machafuko makubwa.

Mhe. Spika, ladha ya chaguzi zozote zile ni kile kitendo cha kuona kuwa *turnout* ya wapiga kura, idadi ya wapiga kura inakuwa ni kubwa katika kila chaguzi; na hii maana yake ni kutokana na zoezi la uandikishaji wa wapiga kura katikati baina ya uchaguzi mmoja na uchaguzi mwengine. Bahati mbaya sana kwamba chaguzi zetu kuu mbali mbali hufanyika huku tukiwaacha nyuma wananchi wengi waliokuwa wana haki pasi na kupiga kura.

Mhe. Spika, kitendo hicho kwa kweli hakikubaliki, kwani ni kitendo kinachokwenda nje ya utaratibu na utamaduni wa kukuza demokrasia katika nchi zetu. Chaguzi hufannyika; mfano hivi sasa kuna Wazanzibari wengi ambao ni Wazanzibari wa kuzaliwa kwa baba na mama na babu, lakini bahati mbaya sana kila chaguzi huwa hawashiriki na hawashiriki kwa sababu moja tu, kuna sheria ambazo ni za kibaguzi. Mpaka sasa hivi Zanzibar tuna sheria ambazo ni za kibaguzi. Kwa sababu leo ikiwa ni Mzanzibari baba na mama na babu dahari kwa dahari, lakini kwa sababu tu kuna sheria ya kukuzuia wewe na tayari miaka 18 umeshafika na kukawa na sheria kama hiyo inayokubagua wewe Mhe. Spika, tunasema hiyo ni sheria ya ubaguzi. Nchi zote zinazoamini katika demokrasia hupigania sana katika kuhakikisha kwamba haimbakishi mtu isimshirikishe katika suala zima la kuchagua na kuchaguliwa.

Sasa leo Mhe. Spika, tunaingia katika uchaguzi. Nafikiri utakuwa ni uchaguzi wa tano huu tangu tuanzishe mfumo wa vyama vingi. Chaguzi zetu zinafanyika huku nyuma zikiwaacha maelfu kwa maelfu ya watu ambao ni wananchi wazaliwa wa nchi hii, wamefika miaka 18 na hawana fursa hiyo Mhe. Spika, chaguzi zetu huwa zinaingia doa hapo. Hilo linatokezea kwa sababu kuna sheria, kama hiyo sheria ya vitambulisho na nyengine kuwanyima watu fursa ili wasitekeleze haki yao ya kidemokrasia na ya msingi.

Mhe. Spika, chombo hiki kipo kwa sababu ya kutunga sheria na kubadilisha sheria. Kama hivyo ndivyo, kwa nini sheria hizi hazibadilishwi au kuna maslahi gani ambayo yanafanya kwamba kuwepo kwa sheria hizi na kuwanyima wananchi wengine wasitekeleze haki yao ya kidemokrasia.

Mhe. Spika, kuna kipindi kimoja mimi na Mhe. Mohamed Aboud; Waziri katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais, tulialikwa katika suala zima lile la vitambulisho vya Taifa. Nikalalamika kwamba Mhe. Mohamed Aboud kuna sheria hii na bahati nzuri tuna habari kwamba keshokutwa italetwa sheria, naomba sana serikali ilete Barazani sheria hii ili tuibadilishe, kama kuna vizuizi tuviondoshe. Mhe. Mohamed Aboud akaniahidi kwamba hiyo sheria italetwa na kweli sheria ililetwa, lakini kile ambacho tulizungumza na kukubaliana kwa kweli hakikuletwa. Kwa sababu niliwaambia kama ikiwa tatizo ni kupatikana kwa vyeti vya kuzaliwa basi sheria ifanyiwe marekebisho ili angalau hayo mambo ambayo yanaonekana kuwa ni vikwazo vikubwa viondoshwe.

Hata wenzetu Bara huko wanavyofanya sasa hivi, kwamba mtu kitu chochote kile kinachoweza kumu-*identify* na ku-*identify* uzaliwa wake, ku-*identify* pengine na umri wake, leseni za biashara sijui nini. Ni vitu vyote vya halali ambavyo vinapokelewa. Kwa nini leo iwe sisi ni lazima uwe na kitambulisho cha *ZAN ID*. Bahati mbaya zaidi vurugu ukienda kuitafuta hiyo *ZAN ID* Mhe. Spika, ni tatizo. Sasa mimi bado nina nasihi. Maana yake mimi nikisema ninataka amani, nasema nataka amani katika utako wa moyo wangu, sisemi kwamba nataka amani kwenye mdomo tu.

Leo kuna watu humu ni wahubiri wakubwa Mhe. Spika, wa amani lakini amani ile huihubiri kwenye ncha ya mdomo tu, ndani ya nafsi zao wana chuki zilizowajenga Mhe. Spika, hatuwezi kuvumilia jambo kama hili; mimi binafsi nikimuona mtu yeyote hata kama ni baba yangu mzazi ni mchochezi wa kuwachochea na kuwagombanisha Wazanzibari huyo siko radhi nae na tutafarikiana maisha. Wazanzibar wote ni kitu kimoja; Zanzibar ni moja na

itaendelea kuwa moja daima. Leo kama kuna mtu yeye ni muhubiri wa kutaka Waunguja na Wapemba wafarikiane huyo Mwenyezi Mungu ana pahala pake kamuwekea! Haiwezekani Mhe. Spika, tuhuhubiri amani katika nafsi zetu tusihubiri kwenye ncha za midomo tu!

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa sababu mimi ni muumini kabisa kabisa wa Zanzibar, ni muumini wa amani ya kweli, ni muumini wa utulivu wa kweli Mhe. Spika, nainasihi sana Serikali yangu tufike pahala hili tatizo tuliondoshe ili wananchi katika nchi yao wapate haki zao, maana yake sasa hivi tunaona zaidi ni mambo ya kupiga kura, sasa hivi Mheshimiwa Spika, ukienda popote kama huna *ZAN ID* hupati, popote lazima uwe na kitambulisho cha *ZAN ID*. Sasa Mhe. Spika, nanasihi na naishauri tena Serikali ifikirie utaratibu wa kuleta sheria hapa na kuibadili sheria ili kuwawezesha wananchi wetu wengi waliotimia miaka 18 wawe na uwezo wa kupiga kura na kuwachagua viongozi wao.

Mhe. Spika, katika hili nataka nihoji suala la uwezo wa Tume ya Uchaguzi. Sasa karibuni kulikuwa na usajili wa wapiga kura na tukapata taarifa kwamba kuna majimbo matano kumbukumbu zake zimepotea, sasa Mhe. Spika, hili ni tatizo kwa sababu Tume ya Uchaguzi ikifika pahala ikipoteza kumbukumbu sijui tutakuwa na usahihi gani wakati wa kura, hilo daftari la kura tunalolitegemea ambalo litakuwa halipo na litakuwa lipo sahihi, hii nahoji kwamba Tume ya Uchaguzi itakuwa imejipanga vipi katika suala zima la umakini na kiteknolojia katika kuhakikisha Serikali inaiwezesha ili matatizo kama haya yasijitokeze; kwa sababu hili ni tatizo, leo ikiwa kumbukumbu za majimbo matano zimepotea tutakuwa tuna uhakika gani kwamba daftari zima baadae halitokuja kupotea katika Uchaguzi wa mwaka 2015. Naiomba Serikali ijitahidi sana kuiwezesha Tume ya Uchaguzi kivifaa na kiutaalamu pamoja na watendaji wake katika kuona kwamba tatizo kama hili kwa sababu litakuja kuwa ni janga la taifa Tume ya Uchaguzi kupoteza takwimu.

Mhe. Spika, katika hilo kwa sababu tumepata taarifa kwamba tukijaaliwa mwakani kabla ya uchaguzi kutakuwa na uandikishaji wa lala salama, naiomba Serikali iiwezeshe tena Tume ya Uchaguzi kuona kwamba zoezi hili la uandikishaji wa wapiga kura wapya kwa awamu ya mwisho linakwenda bila ya matatizo yoyote, kwa sababu tunaamini kwamba zoezi hilo likipita basi kwa kweli tutakuwa tumefunga mlango sasa na tutakuwa tupo tayari kwa ajili ya kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 Mwenyezi Mungu aujaalie uje ufanyike salama na umalizike salama.

Lakini katika hotuba hii ya Makamu wa Pili, pia ameelezea kwamba kuna mpango wa Tume ya uchaguzi Mhe. Spika…

Mhe. Spika: Unazo dakika tano Mheshimiwa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Tume ya Uchaguzi katika kukata majimbo. Mhe. Spika, mimi katika hili naomba nilitolee tahadhari kwa sababu tulishuhudia kwamba majimbo katika awamu iliyopita majimbo yalipunguzwa kutoka Pemba, sasa hii ni tahadhari na kuna maneno yamezungumzwa hasa kwamba Pemba yatapunguzwa tena majimbo mengine Mhe. Spika, naomba hilo lisije likatokea na tunaitahadharisha sana Serikali kupitia Tume ya Uchaguzi wasije wakafanya hivyo, kwa sababu vigezo vya kukata majimbo tukichukua Sensa ya mwaka 2012 Mhe. Spika, Mikoa minne tuliyokuwa nayo Zanzibar wastani wa wapiga kura inalingana na Kusini Pemba, Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba takriban wastani wa wapiga kura inalingana ni *around* 23,000 ni wastani huo.

Kwa hivyo kutakuja kuwa hakuna sababu yoyote kusema kwamba tunapunguza jimbo, mimi nadhani sasa hivi suala la kupunguza majimbo kwa mujibu wa Sensa kama ikiwa kigezo ni sensa hakuna, kwa sababu mikoa yote minne ukiacha mbali Mkoa wa Mjini Magharibi ambao tunajua ni mjini takriban ndio dasturi yake na ndio sifa yake kwamba watu wawe ni wengi. Kwa hivyo natahadharisha hilo wasije wakatumia kigezo hicho katika kuona kwamba wanakata majimbo.

Mhe. Spika, kuna hoja iliyozungumzwa hapa kwamba kuna kaya masikini na tunaiona Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kulipa kaya masikini, hivi naomba nimuulize Mheshimiwa Makamu wa Pili ni kigezo gani mnachokitumia katika kupimia kaya masikini? Naomba utakapokuja unambie kigezo hichi ndio tunachotumia kuona kama hii ndio kaya masikini. Kwa sababu napata wasi wasi kwamba ikiwa kigezo hicho jimbo langu la Chake Chake katika Shehia zilizomo katika Jimbo la Chake Chake hakuna kaya masikini, mimi najua Chake Chake zimo kaya masikini, lakini mbona katika kitabu chako hicho hakuna hata kaya masikini moja, hakuna hata shehia moja zilizomo ndani ya jimbo la Chake Chake au mimi sina masikini kule? Mimi napata wasi wasi, napata wasi wasi

kwanza Mhe. Waziri utakapokuja naomba ukiri kwamba Chake Chake hakuna masikini na kwa nini pesa hizo usipeleke, na wasi wasi naujenga hapa Mhe. Spika, mimi nadhani hizi ni pesa za wakubwa hupiga kuni tu, na kwa msingi huo mimi naomba nimshauri au nimuombe Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, nina wasi wasi mkubwa sana azikague fedha hizo. Kwa sababu hata katika ripoti tunayomalizia hii kuna hoja kuhusiana na fedha zile wanazolipa pensheni imeonekana kwamba kuna tatizo fedha zile za wazee wale pesa za ruzuku kwa wazee wasiojiweza.

Kwa hivyo na hili namuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu afanye kazi ya kuelekea huko sasa akaziangalie hizi fedha wanazosema kwamba zinalipwa masikini, mimi nina wasi wasi mkubwa hakuna watu masikini, ni wale wale matajiri huchukua fedha zao wakatia mifukoni tu.

Mhe. Spika, mwisho naulizia mfuko wa *CDF*. Tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali *CDF*; na hili umuhimu wake ni kwamba Mhe. Spika, ni ukweli kwamba fedha hizi huenda kwa wananchi moja kwa moja, naiomba Serikali sana sana ifikirie kwa sababu hizi ni fedha ambazo zina faida kubwa, tunaomba serikali iongeze fungu hili, kwa sababu wakiongeza fungu hili *impact* yake inaonekana wazi wazi kuwasaidia moja kwa moja wananchi. Lakini vile vile nitoe tahadhari kwa Waheshimiwa, inaonekana kwamba mpaka leo kuna Waheshimiwa fedha za mwaka jana hawajazitumia na wengine waliotumia hawajatoa marejesho na hili ndilo linalotumika sasa kuwa ni kigezo kwamba Serikali ijaribu kuzuiazuia fedha zisitolewe. Mimi nasema kwa yeyote aliyekuwa hajawa tayari kutumia fedha hizi sisi tuliokuwa tayari tumeshatumia na tumeshapeleka marejesho fedha zitolewe sisi tuna haja nazo, sisi ambao tayari tumeshatumia na tumesharejesha mpaka Wakuu wa Wilaya na Mikoa tushawapelekea sisi tupewe, kwa sababu tuna haja nazo waliokuwa hawana haja basi achana nao!

Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais. Kwanza nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa namna anavyojitahidi kutenda haki katika majukumu yake ya kazi, na namna alivyo muadilifu katika suala zima la matumizi ya fedha katika ofisi yake, na nina sababu za msingi za kusema hivyo Mhe. Spika, kupitia kitabu chake hiki katika maelezo ya kurasa mbali mbali na nitawatolea mfano baadae pindi nitakapokuwa nachangia katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, kwanza niishukuru ofisi yake kwa namna ilivyoweza kutatua changamoto za kero za Muungano na karibuni changamoto nyingi zimeshaanza kupatiwa ufumbuzi, ikiwemo suala zima la utekelezaji wa haki za binaadamu, uwezo wa Zanzibar kujiunga na mashirika ya kimataifa; la usafiri baharini, suala la misamaha ya mikopo ya fedha kutoka *IMF*, uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi, Mfuko wa maendeleo wa jimbo wa SMT, kodi ya maendeleo kutokana na *PAYE.* Shukurani za dhati kwa jitihada zake katika kuyapatia ufumbuzi hayo na namuomba asichoke, na kwa yale ambayo tayari yameshapata ufumbuzi basi kuna haja ya kuweza kuyasimamia ili haki itendeke kwa wananchi wa pande zote za Muungano.

Mhe. Spika, baada ya hilo nilikuwa nataka nizungumzie ukurasa wa 37 Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, hapa limezungumziwa suala la migogoro ya ardhi namna Afisi hii ilivyojitahidi kuyapatia ufumbuzi masuala haya, lakini bado kuna matatizo mawili matatu ambayo yamebakia. Nimuombe basi Mheshimiwa Makamu kupitia kwenye Afisi yake kuharakisha kwa yale yaliyobakia ili waweze kupata ufumbuzi wa haraka kwani kutopatiwa ufumbuzi ni kuleta matatizo kwa wananchi walio masikini wa nchi hii ambao ardhi zao zina migogoro ya hapa na pale.

Mhe. Spika, katika ukurasa huo huo wa 37 kirumi nne suala la utekelezaji wa ahadi za viongozi wakuu wa Serikali. Hapa kidogo mimi nataka nizungumzie jambo moja dogo tu na ninavyotaka kuzungumza ni namna ya kumuomba Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kitengo hichi kijitahidi kufuatilia zile ahadi, kwa sababu kuna ahadi tokea Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais haijapewa jina hilo tangu ipo Ofisi ya Waziri Kiongozi; na jambo hili nilikuwa nalipigia kelele siku nyingi kwenye kamati mpaka kwenye maeneo mbali mbali; kwamba wakati ule ofisi ile ilipokuwa Ofisi ya Waziri Kiongozi kuna ahadi ya Skuli ya Kisiwandui namna ya kutengeneza uwanja wao wa ndani, na wakati nipo kwenye Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika ziara zetu tulipata malalamiko makubwa Skuli ya Kisiwandui, kwamba Skuli ya Kisiwandui ina wanafunzi wa elimu mjumuisho wengine hawaoni ule uwanja ukiingia maji inakuwa wale vijana wanashindwa kutafuta njia zao ambazo

wamejiwekea kimazoea kupita kutokana na kadhia ya maji, unajua mlemavu anakuwa na njia zake maalumu ambazo ameshaziweka.

Sasa inapotokezea kujaa maji ile njia yake inabidi abadilishe njia sasa kutafuta njia ya haraka kwa siku moja inakuwa ni tatizo, sasa niombe kwamba ahadi ile ya Makamu wa Pili hebu tuifuatilie tuone tatizo lake liko wapi na kuweza kuipatia ufumbuzi, kwa sababu imekuwa ni ahadi ya muda mrefu na malalamiko yamekuwa mengi. Kamati iliyopita imeshapewa malalamiko hayo na sisi tumeshawahi kuzungumzia maeneo mbali mbali.

Jengine Mhe. Spika, nataka nizungumzie Ofisi yetu ya Baraza la Wawakilishi jana Mheshimiwa Mwenyekiti alipokuwa akisoma hutuba yake hapa alizungumzia jengo la banda la gari na hakuridhishwa na ujenzi ule, na sisi ndio kioo; mazuri yanatakiwa yaanze hapa taasisi zinazobakia ndio zifuate mfano wetu sisi na mara nyingi nimekuwa nikipiga kelele Mhe. Spika, hata juzi wakati ninachangia bajeti ya Wizara ya Fedha nilisema kwamba kuna njia nyingi za kuzuia mianya ya upotevu wa fedha si lazima tupambane na watu hata kujenga majengo yasiyokuwa na viwango pia ni upotevu wa fedha.

Mhe. Spika, tokea asubuhi nilikuwa natafuta namna ya kuweza kunisaidia, jengo lile naamini unanisikia na wewe ndio msimamizi mkuu utalifanyia kazi haraka lakini kama fedha huna basi yale maturubali yakaondoshwe kwa sababu yanaondosha taswira nzuri ya jengo lako la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya kutoka kwenye taasisi yangu mwenyewe ya Baraza la Wawakilishi nataka nizungumzie Tume ya Uchaguzi. Kitengo hiki ni kikubwa na kila mtu anayesimama hapa anakizungumzia kwa sababu bila ya wao hata sisi ndani ya Baraza hatuwezi kuingia, kwa sababu wao ndio wanaotusimamia, wao ndio wanaosimamia chaguzi zetu hatimae wao ndio wanaotufanya sisi tuweze kuringa na kuingia katika chombo chako hichi cha kutunga sheria. Kwa sababu pasipo na uchaguzi hatuwezi kupata Wawakilishi wa wananchi.

Mimi naanza kukizungumzia chombo hichi kwa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa namna wanavyojitahidi kufanya kazi zao na namna wanavyofanya kazi zao kwa uadilifu mkubwa sana, na ushahidi wa yote haya ni namna tulivyomaliza uchaguzi wetu uliopita uchaguzi mdogo wa Kiembesamaki hakukuwa na migogoro wala malalamiko yoyote, hii ilitokana na utendaji bora wa Tume yetu ya uchaguzi, lakini hawa ni binaadamu na binaadamu wana mapungufu na Mwenyezi Mungu anasema *(khalakal-insaana dhaifa)* kwamba kila binaadamu ana mapungufu yake wanaweza kuwa na dhamira nzuri, sasa basi pale ambapo panatokezea kwa bahati mbaya kuteleza tusiwe tunawasakama, kwa sababu hata na sisi tunateleza Mhe. Spika.

Jana nilikusikia sana ulipokuwa ukikanya kwa Wajumbe wako wa Baraza namna ya kuwa na *tune* ya kuzungumza; amani ya bara yote ni mapungufu, sasa isiwe mapungufu kwetu sisi lakini pande nyengine ya taasisi ikiwa na mapungufu tuanze kuwasakama kwamba hawafanyi kazi vizuri hatuwatendei haki Mhe. Spika, kwa Afisi ya Makamu wa Pili kusaidia taasisi hii kuipa nyenzo za kisasa ili waweze kufanya kazi zao kwa wepesi.

Lakini la pili ninalomuomba Makamu wa Pili wa Rais wawasaidie taasisi hii kuwawezesha katika kupata mafao yaliyokuwa mazuri. Hii taasisi ina ushawishi kama mafao hayakuwa mazuri tunaleta wepesi kwa wafanyakakazi baadhi tu kuweza kuhadaika na kutoweza kufanya kazi zao zilizokuwa nzuri, sasa Mheshimiwa Makamu wawezeshe Tume ya Uchaguzi katika kupata vifaa vya kisasa, lakini wawezeshe katika kupata fedha za kutosha katika masuala yao ya utendaji wa kazi ili kuondokana na mambo madogo madogo ya kuweza kushawishiwa ili wasitende kazi zao vizuri, lakini mpaka sasa hivi Tume ya Uchaguzi inafanya kazi vizuri na tunajiridhisha sote kama wananchi wa Zanzibar.

Lakini Mhe. Spika, niwaombe Tume ya Uchaguzi kaka yangu hapa aliyemaliza Mheshimiwa Omar Ali Shehe alisema Pemba kusiguswe katika kuyapunguza majimbo, mimi sizungumzii Pemba; Tume ya Uchaguzi wenyewe wanajua wanafanya kazi zao kwa mujibu wa utaratibu wanaangalia sensa namna ilivyofanya kazi na mipaka jinsi ilivyo, lakini kama wao Pemba hawataki kupunguziwa majimbo sisi Zanzibar sio kama tunataka Mheshimiwa kwa mujibu wa utaratibu wa sheria za nchi hii, kwa mujibu wa kazi zao ndugu zetu wa Tume ya Uchaguzi wayaangalie zaidi Mhe. Spika, Majimbo ya ukanda wa Magharibi pamoja na Wilaya ya Kati na Kusini, kama kule hakuhitajiki kupunguzwa Unguja kunahitajika majimbo yaongezwe, *population* imekuwa kubwa, majimbo yana *geography* ngumu tofauti na maeneo mengine.

Mhe. Spika, hata sensa inasema katika jimbo la Fuoni wana wapiga kura karibuni 70,000 mwenzangu ana 24,000, 24,000 ukigawa kwa 70,000 unapata majimbo matatu kwa 72,000. Kwa hivyo nafikiri jimbo la fuoni linahitaji kukatwa kuwa majimbo matatu badala ya kuwa jimbo moja lililopo sasa hivi Mhe. Spika.

Na si hilo tu kuna jimbo la Koani ukiangalia *geography* yake jimbo la Koani limeanzia Koani yenyewe, Machui, unatoka Machui unakwenda Ubago, unatoka Ubago - Jumbi, unakwenda Bungi, Unakwenda Unguja Ukuu, unakwenda Uzi Mheshimiwa kaka yangu Mussa Ali Hassan namuonea huruma sana, majimbo manne kwa jimbo moja la Pemba majimbo ya Unguja yaangaliwe katika azma ya kuweza kuyasaidia ili kuwe na usawa katika utendaji wa haki kwa Wawakilishi wako nafikiri wenzangu wa Tume ya Uchaguzi wamesikia na watalifanyia kazi.

Mhe. Spika, nimezungumza suala la kutenda haki kwa wananchi waliokuwa na haki ya kuweza kujiandikisha kuweza kupiga kura kila mtu anazungumzia kwa mantiki yake, mara nyingi tunakuwa tunapenda kuitupia lawama Serikali na vyombo vyetu hivi vya sheria lakini tunatizama sehemu moja sehemu ya pili tunashindwa kuitizama.

Mhe. Spika, sio kama Tume ya Uchaguzi ina matatizo, baadhi ya matatizo tunayo sisi wenyewe wananchi, kwa nini niseme hivyo Mhe. Spika, sasa hivi kumetokezea utamaduni wa miaka mitatu minne hii kwamba ndugu zetu kutoka Pemba huwa wanakataa kujiandikisha katika makaazi yao wanakuja kutaka kujiandikisha katika makaazi ya Unguja na hususan Magogoni na Kwerekwe, sasa unapomwambia mtu afuate sheria ili uandikishwe uwe mpiga kura sheria inazungumza utimize miaka 3, sasa mtu anakuwa na mwezi mmoja, mwezi wa pili analazimisha aa mimi niandikishwe, lakini ukiangalia stakbadhi zake zinaonekana yeye ni mkaazi wa Mkoani anakwambia nimehamia muda mrefu, ukiangalia *document* za masheha muda aliohamia hauna urefu wowote.

Sasa mimi nafikiri katika kutenda haki lazima tuangalie pande zote mbili; hasa na sisi wananchi basi tunapaswa kuangalia wapi unastahiki kuandikishwa kuwa mpiga kura. Tatizo sio kuwa kama unakataliwa usiwe mpiga kura, tatizo linajitokeza kwamba unapotaka kuandikishwa kuwa mpiga kura hapastahiki kisheria. Sasa ninafikiri na hili sisi kupitia wananchi nalo pia basi waliangalie kwamba tuache kuvitupia lawama vyombo vya sheria tukataka kujiongezea sisi haki zilizokuwa hazina msingi wa sheria.

Mhe. Spika, nataka pia nizungumzie suala la madawa ya kulevya. Mheshimiwa hili janga bado zito sana na kelele zimekuwa nyingi. Mhe. Hamza hapa hayupo lakini wakati Mhe. Hamza alipokuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Kiongozi, aliandaa mikakati ya namna ya kupambana na janga hili. Mimi sitaki kulizungumza sana lakini ninafikiri kuna haja ya Ofisi ya Makamu wa Pili kujaribu kukaa na Mhe. Hamza kumuuliza mikakati aliyoipanga wakati alipokuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Kiongozi ambayo ilisaidia kupunguza kwa kasi kubwa sana masuala ya uingizaji na utumiaji wa madawa Zanzibar. Mimi nataka kuzungumzia hapo wenzangu watazungumzia zaidi kwa sababu nina mengi Mhe. Spika, nataka niendelee kuzungumza.

Nataka nizungumzie Mhe. Spika, katika suala la Idara Maafa, niipongeze Serikali kwa kuanzisha kitengo hiki…

Mhe. Spika: Kwa muda wa dakika tano.

Mhe. Ali Salum Haji: Ninakushukuru nitajitahidi kutumia ili nimalize kwa muda. Kitengo ni kizuri mambo waliyoyapanga ni mazuri lakini Mhe. Spika, pamoja na mazuri haya panapo zuri basi na mabaya pia yanakuwa yanajitokeza. Niwaombe Ofisi kutafuta namna basi ya kuwa na kitengo kitakachokuwa na mfuko utakaowawezesha wale ambao wanaathirika na majanga ya maafa.

Mhe. Nassor Salim hapa alizungumzia maeneo yake ya Rahaleo. Mhe. Spika, upepo wa Rahaleo pia uliikumba kadhia hiyo Jimbo la Kwahani. Sasa nataka nitoe indhari moja tu kwa Ofisi. Mhe. Spika, katika janga lile la upepo ambalo limetokezea miezi sita, saba nyuma, katika Jimbo langu la Kwahani palifanyika ziara ya kuwapa pole watu wale iliyofanywa na Mkuu wa Wilaya. Na Mkuu wa Wilaya alitoa agizo kwa masheha kuorodhesha wale watu ambao wamepata matatizo makubwa. Matumaini ya wananchi anapokuwa nyumba imeharibika paa lote limeezuka, Sheha anapokwenda kwa kauli ya kiongozi wake wa juu Mkuu wa Wilaya kwamba aorodheshe na ataje tathmini ya majanga yaliyompata, mwananchi yule anategemea kwamba serikali yake itamsaidia.

Lakini pasipo na kusaidiwa tunawapa kazi ngumu masheha, leo sheha akija kupata suala jengine kutaka kwenda kwa mwananchi, kama mwananchi yule alishindwa kusaidiwa alipopata tatizo, atashindwa kutoa ushirikiano kwa sheha katika jambo jengine lolote linalojitokeza. Sasa niombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kutafuta namna ya

kupata mfuko ili maagizo ya viongozi wengine wa serikali wanapokwenda kutoa agizo la kazi kwa masheha katika kufanyiwa tathmini ya majanga yaliyowapata basi wananchi wale wapate kufarijika na kuondosha kadhia ile. Na nina imani kwamba lile suala bado liko kwa Mkuu wa Wilaya, sijui kama kwako limefika, kama halijafika Mheshimiwa waonee huruma wananchi wa Jimbo la Kwahani waliopata kadhia ya upepo uliojitokeza katika siku za karibuni ili angalau wapate chochote cha kwenda kuwasaidia.

Mhe. Spika, nataka nimalizie mambo mawili madogo sana; moja la kaya maskini. Mhe. Spika, na mimi nimuombe Mhe. Makamu wa Pili nataka vigezo kwa sababu hata Kwahani pia sijawaona watu wa Kaya maskini. Na natumai kwamba mimi kama Mwakilishi wao, ninazijua kaya nyingi ambazo zinaishi katika mazingira ya umaskini tena uliokuwa umebobea, sasa nataka kujua vigezo na sababu, na kama bado labda hawajafikia katika Jimbo la Kwahani, basi watakapoanza safari hii waanzie na Jimbo la Kwahani waendelee na majimbo mengine.

Na la kumalizia kabisa Mhe. Spika, ninataka kuzungumzia ukurasa wa 25 muelekeo wa vipaumbele. Mhe. Spika, nimeanza mwanzo kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais namna anavyofanya kazi kwa uadilifu kabisa. Hapa katika vipaumbele pana suala la kuimarisha huduma za usafiri na makaazi ya Makamu wa Pili. Mheshimiwa sababu ya kumsifu Mhe. Makamu wa Pili kwa kutenda haki, namna alivyokubali kufanyiwa ukarabati wa jengo lake na kukataa kwenda kukodi nyumba za watu binafsi kwa gharama kubwa na kuitia hasara serikali zisizo na msingi kwa baadhi ya viongozi wakuu wa kitaifa.

Mhe. Spika, ninakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuwa katika jengo hili la Baraza lako tukufu kwa hali ya afya njema. Lakini pia Mhe. Spika, mwanzo kabisa nichukue nafasi hii kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete pia na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutimiza miaka 50 ya Muungano wetu wa Tanzania. Pia niutakie kila la kheri Muungano huu ili uweze kuendelea dumu daima.

Lakini pia nichukue nafasi hii Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Waziri wake pia na watendaji wake wote wakuu ambao wamemsaidia kwa namna moja au nyengine kutuletea hotuba hii mwanana; ambayo kwa kweli imesomwa kwa aina yake, ni mara ya kwanza hotuba iliyosomwa kwa aina yake. Nichukue pongezi za dhati kabisa nikupongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwanza nizungumze baadhi ya mambo ambayo sitotaja ukurasa kwa ukurasa kwa sababu ni mambo mengine ambayo jengine limetokea huku lakini na jengine limeoana huku. Mimi nimefurahi sana katika hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais kuna mambo ambayo yamesisitizwa kutumia matumizi mabaya ya fedha kiholela holela. Sasa naomba serikali kwa jumla kwa sababu yeye ndio Msimamizi Mkuu wa Watendaji wote pamoja na Mawaziri wote wa Wizara zote za Zanzibar. Ningeomba sana tutumie utaratibu ambao tulikuwa nao nyuma Mhe. Spika.

La kwanza kumbi za mikutano tutumie kumbi zetu ambazo ziko katika mawizara yetu mbali mbali, lakini pia nitoe wito hata Baraza la Wawakilishi zina kumbi, pia nao semina na mikutano tujaribu kutumia kumbi zetu ili kutotumia fedha pasipo na lazima. Hilo moja.

Lakini jengine imetajwa humu kununua thamani na vifaa vya ofisi. Mhe. Spika, huko nyuma na mpaka leo tuna Mafunzo wanatengeneza, tuna watu wa Chuo ambacho kinatengeneza sanaa, nimekusudia mapambo mbali mbali ya ofisi kama sofa seti, meza na baadhi ya vifaa. Ningeliiomba sana serikali tukarudia ule mfumo wa nyuma ili kuhakikisha tunatengeneza vitu madhubuti kuliko kutengeneza nyumba za panya. Maana kuna masofa mengine ni nyumba za panya Mhe. Spika, tutengeneze *sofa set wood* ambazo sisi kiasilia ndio mambo yetu ya sanaa.

Katika mambo mawili hayo nayaomba sana na ninamuomba sana Makamu wa Pili wa Rais kwa kweli katika Wizara zetu zihakikishe zinatumia vile vifaa ambavyo vimo katika aila yetu. Tuna Chuo cha Ufundi, tuna wenzetu hawa Mafunzo, kama tunavyotumia majenzi yetu kuwapa vikosi vyetu basi na mambo haya mengine tuyatumie hivyo hivyo katika Wizara zetu mbali mbali Mheshimiwa. Saa nyengine tunanunua vifaa siku mbili ya tatu unaona mkono ukinyanyuka unanyanyuka nao, wakati tuna mafundi wazuri wenye kutengeneza vitu vizuri ambavyo vinapigiwa mfano, na wenzetu wengine wanatoka huko wanakuja kuagizishia vitu ambavyo kwa kweli ni vizuri. Hilo la pili.

Lakini jengine Mheshimiwa niseme tu mimi kila nikisimama kwenye vikao vyetu mbali mbali vya Baraza na hata katika vikao vyetu kama hivi vya Baraza la Wawakilishi nasema jamani hawa wanawake wamekosa nini? Akinamama wamekosa nini kwamba na wao hawapatiwi huu mfuko, sisi si lazima Mhe. Spika, tupatiwe kama wanavyopatiwa wenzetu wa jimbo. Lakini sisi tunafanya kazi za mikoa hatufanyi kazi za jimbo Mhe. Spika. Kama sheria ningeliomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hii sheria basi ibadilishwe angalau na akinamama na wao wapate chochote.

Mhe. Spika, ukingalia wanawake wanatumia fedha nyingi zaidi kuliko wanaume katika majimbo. Kama mfano wangu mimi, mimi ni wa kitaifa si wa jimbo, si wa mkoa mimi ni wa kitaifa, tena taifa lenyewe ni Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa hivyo naomba Mheshimiwa haya mambo na ukiangalia akinamama ndio wazalishaji wakuu wa shughuli zote katika nchi. Hebu chonde Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ninajua sheria ipo kama kuna mabadiliko tuombeeni na sisi huko mlikowaombea hawa wenzetu ili na sisi tuweze kutumia hii haki ya kusaidia akinamama wenzetu. Lakini si akinamama tu hata wananchi wetu katika sehemu mbali mbali za taifa letu hili la Zanzibar. Ninakuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Na nakuomba hii ni changamoto ukiianzisha hapa na Tanzania Bara na wao itakubalika, hebu tuizungumze hii kwa Tanzania na sisi ili tuweze kupatiwa mchakato huu wa fedha. Sisi hata ukitugaia milioni kumi si lazima ishirini. Ninakuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Sasa nije katika wale wanaopewa fedha hizi katika majimbo. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais watanisamehe Wawakilishi wa majimbo, maana kila mtu hulia mama yangu halii mama yetu, hulia mama yangu. Sasa mimi ninalizungumzia hili, naomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais maana nilisikia tetesi na nimesikia kwenye Bunge, sasa naomba Ofisi yako uje utufafanulie hizi fedha ambazo umeambiwa umezila. Hizi pesa *CDF* umezila, sasa naomba hapa Waziri husika uje utufafanulie ilikuwaje.

Maana yake mimi ninavyokumbuka kwamba hizi fedha ziliingizwa tarehe 7/05/2014, zilitoka kule nyinyi mkazipata tarehe 8, maana yake mimi nilikuja nikamuuliza Waziri makusudi nilitoka hapa asubuhi nikaenda nikamuuliza pale. Hivi nilivyopata taarifa mimi ni kweli au vipi, sasa tusizungumze maneno kuwasingizia viongozi, kwa kweli si jambo la maana na wala si jambo la busara. Mtu anavyozungumza kitu awe na uhakika nacho, sasa nitakuomba Mhe. Waziri uje unihakikishie fedha hizi ilikuwa kuwaje? Utueleze tuelewe tusizungumze tu maneno ambayo kwa kweli hayana muelekeo mzuri kumzulia kiongozi. Hilo moja.

Lakini jengine fedha hizi hizi za majimbo kipindi kilichopita kuna watu wamepata hizi fedha za majimbo. Mimi ninaiomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, aliyekuwa harejeshi hizi fedha asipewe, aliyekuwa harejeshi matumizi. Kwa sababu fedha hizi makusudio makubwa Mhe. Spika ni kupelekwa kwenye jimbo kutafuta miradi ya wananchi. Lakini kuna wengine mpaka leo sijui washazipiga kuni au sijui vipi? Maana yake nitasema washazipiga kuni, yule aliyekuwa hajarejesha. Wewe fedha zinaingizwa moja kwa moja, sasa tafuta mradi wako ambao wa kuhakikisha pamoja na ile timu yako unayofanyia kazi urejeshe marejesho. Na ndio maana nikasema na sisi wanawake hizi fedha tupewe wasipewe wanaume tu peke yao ili kuwe na mashindano maalum hapa Mhe. Spika.

Lakini jengine Mhe. Spika, mimi niseme kijana wangu hapa Mhe. Omar Ali Shehe alizungumza sana kuhusu habari ya amani kwamba tunasema hapa tu. Mimi nasema hatusemi hapa, kama kweli tuna nia Mhe. Spika, na nia tulikuwa nayo na tumekwenda nayo vizuri tu, tukiacha mambo yetu ya siasa kila mtu na chama chake, lakini hapa katikati tulivurugana tukubaliane, sijui kulikuwa na kitu gani kimefanya kwa sababu mimi kawaida huwa ninasema ukweli.

Sasa tujiulize sisi wenyewe viongozi kulikoni, tujiulize sisi viongozi sote tuliomo humu kwenye Baraza la Wawakilishi, kumepita nini? Kama kweli tunataka umoja na kweli tunasema katika udhati, katika mtu ambaye sipendi ubaguzi basi na mimi mmojawapo. Kwa sababu ubaguzi ukianza kubagua ujue hata wanao uliowazaa utawabagua, wale wanao uliowazaa ndani ya nyumba utawabagua!

Kwa hivyo mimi ninasema kwamba kwa kweli tukae tujiulize ni kitu gani kilichotufanya sisi tukaanza sasa hivi, au kwa sababu keshokutwa 2015 kuna uchaguzi ndio tunaanza visa sasa hivi. Kwa sababu tunaelekea kwenye uchaguzi, maana sisi tutaelewana vizuri lakini ikifika karibu ya uchaguzi basi tunaanza kupurukushana. Kwa nini tujiulize, amesema kijana wangu Mhe. Omar Ali Shehe, kwamba sisi ni baba mmoja mama mmoja. Mtumbatu kamuoa Mpemba, Mpemba kamuoa Mmakunduchi, sasa unabagua nini wakati mmeshakula pamoja. Unaweza ukamtukana Mtumbatu, ukimtukana Mtumbatu unajitukana wewe mwenyewe. Ukimtukana Mmakunduchi unajitukana wewe mwenyewe Mpemba.

Mimi ninauliza kwa nini? Kulikoni? Hebu tuwe wakweli, tusiwe wa kusema hapa na miongoni mwetu ni kweli katika mtu Mhe. Spika, niliyekuwa sipendi ubaguzi ni mimi. Na katika mtu ambaye mimi nikeshakusema neno langu kama hivi, yamekwisha lakini safari hii hayaishi. Maana yake mimi nikishakusema hapa *ahlan wasahlan* lakini safari hii hayaishi, tumefanyiana vitendo vibaya sana sisi wana CCM pamoja na CUF, kulikoni, kuna nini hebu tuwe wakweli. Mimi huwa sitaki kusema haya lakini mtu akianza na mimi namaliza, mimi nilikuwa sitaki kusema kabisa haya kwa sababu ni mmojawapo ambaye nimewekewa mabango utafikiri nimeua. Lakini najua kwamba mimi ni mtu muhimu katika nchi hii, kwa sababu unapotangazwa kwa ubaya, unapofanya kila kitu unajulikana kwamba wewe ni muhimu. Mimi nasema tuwe wakweli tuache malumbano yaliyokuwa hayana maana.

Naomba sana, tena naomba sana, kama kweli tunataka umoja na amani katika nchi hii basi tuanze tena upya, si hivyo tusiwabague wananchi wetu wala tusiwachochee. Kwa sababu mimi napita humo nazomewa, lakini mimi ndiye yule yule Asha Bakari sibadiliki, sio kama mtu akinizomea ndio nitatoka mashavu, ndiye yule yule. Kwa hivyo, mimi nasema tuwe wakweli tusidanganyane Mhe. Spika.

Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami asubuhi hii kupata nafasi ya kutoa yangu machache niliyonayo juu ya hoja iliyoko mbele yetu. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi hii kusimama hapa kwani wako wengine wengi wenye umri wangu sasa hivi wanafukiwa, wengine kama ni Waislamu wanasomewa na kadhalika. Kwa hivyo, mimi nishukuru kuwa mpaka dakika hii niko hai na bado pumzi zangu zinakwenda, na nataka kuzungumza machache kwenye chombo hiki cha kutunga sheria cha Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nianze kwenye Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Mwaka uliomalizika wa fedha ofisi hii iliombewa karibu shilingi 780 milioni na ushei, kati ya hizo shilingi 521 milioni na ushei ilikuwa ni kazi za kawaida na shilingi 258 na kidogo mishahara, maposho na michango mengine mbali mbali.

Mwaka huu ofisi hii imeombewa shilingi 483 milioni ambapo takriban ni karibu ya nusu ya maombi ya mwaka jana, lakini kwa mishahara imeombewa shilingi 330 milioni na kidogo na matumizi mengineyo shilingi 152 milioni.

Mhe. Spika, kidogo niulize, mwaka jana maombi yalikuwa makubwa mara hii karibu ni nusu ya mwaka jana. Je, kuna kazi ambazo mwaka jana zilikamilika hadi kufikia mara hii maombi yawe madogo kiasi hiki? Lakini pia niulize kuwa mwaka jana maombi ya mshahara hayakuwa makubwa kuliko mara hii, mara hii ni makubwa sana. Najua kama kuna nyongeza za mishahara na kadhalika, lakini kuna tofauti karibu ya shilingi 71 milioni baina ya mwaka jana na mwaka huu. Je, kama kuna nyongeza za mishahara na mengineyo, nyongeza hii imefika kima chote hicho kwa tofauti hii iliyopo hapa?

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo machache nije kwenye ukurasa wa 8 ibara ya 15, nizungumzie padogo tu panapozungumzia dhana ya Mapinduzi ilikuwa ni kuleta maisha bora kwa kila Mzanzibari na kuondoa ubaguzi wa aina zote. Hiyo ni moja, lakini pia Mapinduzi kulingana na Chama cha Afro Shirazi kabla ya Mapinduzi kilileta Mapinduzi kwa sababu mbali mbali, haikuwa kwa sababu hii tu, pengine Afro Shirazi ilihisi kuwa watu katika nchi yao hawakuwa na uhuru wa kujitawala, wafanyakazi ilikuwa wanalipwa maposho madogo kuliko kazi wanayoifanya na ilikuwa hawana haki ya kumiliki ardhi katika nchi yao.

Tutazame wafanyakazi wa leo je, mishahara wanayolipwa inakidhi haja? Wakati ule ilikuwa haikidhi je, leo inakidhi? Kama haikidhi haja kwa nini na lengo moja likawafanya wafanyakazi wetu wakati mishahara ambayo itakidhi haja ya maisha yao.

Mhe. Spika, kwa mtizamo wangu mimi mishahara ya watu wa chini haikidhi haja yao. Kwa hivyo, kwa hili bado hatujapiga hatua kutoka pale tulipokuwa nyuma. Kwa hili hatujapiga hatua sana, kwa sababu mpaka leo mishahara bado haijakidhi haja.

Mhe. Spika, mfanyakazi anavyotakiwa kazi anayofanya imuendeshe kwa mambo yote, imlishe, imvishe, imuuguze, impatie makaazi na kila kitu na pia isomeshe watoto wao, kama hatujafika hatua hiyo basi mpaka leo mishahara ya wafanyakazi haijakidhi haja, na tuna hatua kubwa kufikia mishahara yetu ikidhi haja, tuko mbali sana kufikia hapo.

Nije kwa hili lililozungumzwa la kuondoa ubaguzi wa aina zote. Kiukweli Mhe. Spika, ilikuwa hili ndio lengo, baada ya Mapinduzi ikatokea hii *inter marriage* huyu kamuoa huyu, huyu kamuoa yule, lengo ni kuondoa hizo tofauti. Lakini je, sisi viongozi wa leo tunaendeleza dhana hiyo iliyokusudiwa wakati huo? Kama hatuiendelezi kwa nini? Mimi nahisi dhana hii ya kuondoa ubaguzi wa aina zote pole pole inatoweka ambapo ni jambo baya na la hatari.

Mhe. Spika, sitaki nirudie uliyoyakataza lakini wewe mwenyewe unayasikia, umeyashuhudia, umoja, utulivu na amani iliyopo kaagizwa mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi humu kuwa apeleke hoja, lile lilikuwa sio ombi, kaagizwa peleka hoja ya kuwauliza Wazanzibari kama wanataka Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa au laa. Hii ni dhana ambayo inaashiria kuondoa huo umoja.

Kuna mchangiaji kasema ofisini ukienda ni mtu wa mjini na Mpemba, kwanza hii si kweli. Miongoni mwa watu wachache katika ofisi zetu ni Wapemba. Kwa hivyo, dhana ile ilikuwa si ya kweli lakini tuliivumilia hatukuikemea, kusema kwamba Wapemba ni wengi kuliko wengine inaashiria nini?

Mhe. Spika, mtu kusimama akajikaza kuwa hii sio serikali ya vikaratasi na vinafanyiwa uchaguzi ni uchaguzi wa nini, watu wa aina hii wanaashiria nini. Tuasane mimi na wenzangu wote tuwe wakweli, tusitende hapa kumbe tuko vyengine.

Mhe. Spika, wako watu wanaoaswa kuwa mbali kidogo na wengine ndani ya Baraza hili; watu wa Baraza moja, tunafanya kazi moja, lakini utapoonekana kuwa unaambatana sana na Mhe. Mohamed Haji Khalid na watu wa aina yake unaambiwa aa, *why*? Kwa hivyo, hii dhana ya kutobaguana ni nzuri na itatuletea tija, lakini kwa ndani ya moyo wangu naona tunapotea.

Mhe. Spika, mambo haya madogo madogo yanayotokea katika wakati huu ndio yanayosababisha kama wenzetu duniani wakapigana kutokana na chokochoko ndogo ndogo za aina hii.

Mhe. Spika, nije kwenye masuala ya Muungano. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais miongoni mwa mafanikio aliyoyasifu na ni kweli ni amani na utulivu, hivi amevipa kipaumbele sana na ni sawasawa alipe kipaumbele. Kwa sababu bila ya amani na utulivu hakuna kitakachoendelea.

Lakini Muungano huu pamoja na kwamba kuna amani na utulivu mkubwa, changamoto ziliopo ni nyingi na zimeshindwa kupata ufumbuzi kwa muda mrefu. Na zile ambazo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kaziona kuwa ziko katika hatua nzuri bado ni changamoto na zitaendelea kuwepo. Kwa mfano, Zanzibar kukosa mgao wa mapato yatokanayo na faida ya Benki Kuu ni changamoto, vyovyote ilivyo itaendelea kuwepo. Kwa sababu hawa waliotuzuilia hiyo faida bado wapo na bado wanaona kama Zanzibar *is their colony.* Kwa hiyo, mtu koloni lake analipa vile anavyotaka yeye. Kwa hiyo, hii ni changamoto ipo na itaendelea kuwepo.

Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi. Hii imeonekana kuwa iko katika hatua nzuri lakini suala hili kabla mimi kuwepo hapa lilikuwepo na likatolewa katika Muungano. Sisi tumekuja tumeambiwa mazungumzo yanaendelea tusiwe na haraka, tusiwe na hivi, keshokutwa tunamaliza liko hivyo hivyo na tutaendelea kuwa hivyo hivyo. Kwa hivyo, hii ni changamoto na itaendelea kuwa changamoto wala mimi siamini kuwa liko katika hatua nzuri kama ilivyoelezwa.

Mhe. Spika, Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje. Hii Zanzibar nafasi hiyo haina kulingana na Muungano huu ulivyo, hawana haki ya kujiunga na nafasi yoyote. Mfano mzuri wa Dr. Salmin Amour Juma alifanya hivyo na sitaki nitumie neno baya, lakini alizuiwa kuwa asifanye hivyo, itafanya Tanzania na haikufanya wala haifanyi.

Mhe. Spika, kuhusu ajira kwa Wazanzibari katika Taasisi za Muungano, ukiacha Jeshi la Polisi na Uhamiaji na sehemu nyengine ndogo ndogo. Katika ofisi nyengine za nchi za nje Wazanzibari hatuna nafasi wala hatutegemei kuwa tutapatiwa nafasi hiyo katika taasisi hizo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa unazo dakika tano.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Hee, ninazo kidogo sana. Tume ya Pamoja ya Fedha ndio hivyo hivyo ni changamoto na changamoto hizi zimekuja kwa nini, pale changamoto kubwa kuliko zote ni Zanzibar kukosa

mamlaka yake. Suala la Muungano Zanzibar baada ya kupoteza kiti chake cha Umoja wa Mataifa, Zanzibar ilikuwa *khalas;* haipo, kwa sababu haina uamuzi wowote. Hii ndio changamoto kubwa kuliko zote, hizi nyengine ni vidokezo tu, lakini kwa kuwa imekosa maamuzi ya kinchi hii ni changamoto kubwa na imekuja kwa ajili ya Muungano huu, bila ya kutokea marekebisho katika Muungano huu Wazanzibari tutaendelea kuwapigia mabwana magoti, watakayo ndiyo watayotupa, wasiyotaka watatwambia hili haliwahusu.

Mhe. Spika, Zanzibar kuwa haina mamlaka ya kujiamulia mambo yake hii ndio changamoto, kama ni changamoto, kama ni tatizo, kama ni kikwazo, hiki ndio kikubwa kuliko vyote. Mchawi wetu ni Zanzibar kuwa haina mamlaka yake, tufanye Muungano ambao Zanzibar ita-*retain* ili iweze kujiamulia mambo yake wala isiamuliwe pahala pengine.

Mhe. Spika, hizo dakika tano sitaki nizimalize, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika naomba nikushukuru kunipa nafasi hii. Wakati Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anatoa hotuba yake jana, lakini leo muda huu Televisheni yetu ya Taifa haifanyi kazi kwa sababu ya uwezo mdogo, au vifaa vyake na mambo mengi; *sofa set wood, sofa set wood, sofa set wood.* Sasa ndio nasema kwamba nianzie hapo kuwa televisheni ilitegemewa itoe matangazo haya moja kwa moja kwa ajili ya kuwasaidia elimu na taarifa wananchi wetu, lakini hivi nazungumza pamoja na wenzangu basi televisheni zetu hazifanyi kazi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Salmin Awadh Salmin, na naomba nitofautiane kidogo na wenzangu pale alipotangaza nia yake ya kuleta hoja binafsi Barazani. Nampongeza kwa sababu Mhe. Salmin Awadh ni Mwakilishi na Wawakilishi kuna sheria kamili ya Kinga, Haki na Fursa za Wawakilishi ikiwa ni pamoja na kuleta hoja binafsi Barazani. Nadhani kama atafanya hivi ni haki yake na lazima kama ni Mwakilishi nimpongeze.

Nampongeza kwa sababu mimi niliwahi kutangaza nia yangu kule Dodoma kwamba nitakaporudi hapa binafsi kama Hija Hassan nitaandaa hoja binafsi ya kuwataka Wazanzibari waulizwe na waridhie iwapo Muungano wanautaka au hawautaki. Sasa nilipoona mwenzangu ametangulia kuleta hoja yake ni imani yangu kwamba Ofisi ya Baraza la Wawakilishi itatusaidia kitaalamu ili tuweke hoja mbili sambamba kwenye Baraza hili, hoja ya kuulizwa uhai wa *GNU* miaka minne na hoja ya kuulizwa Muungano wa miaka 50 ili twende sambamba wananchi waamue mustakabali wao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo, si sahihi Wajumbe kumlaumu Mhe. Salmin Awadhi Salmin wakati anatumia fursa yake na haki yake ya kinga kwa mujibu wa Kanuni.

Mhe. Spika, pongezi za pili nikupongeze wewe binafsi kama mtu ambaye anaenzi na kulinda amani ndani ya chombo hiki ni Mhe. Pandu Ameir Kificho na wengine wote wanadanganya tu kwa sababu ya kuficha ukweli. Wewe umekuwa ukisema na kuchukuwa hatua kwa yale mambo ambayo umekuwa unahisi yanaelekea kubaya, mfano wa karibu ambao taarifa tunazo sio rasmi. Kuna Wawakilishi humu ndani walipendekeza kwamba huu muundo wa Wawakilishi wa kukaa kitako CCM, CUF, CCM, CUF, Spika upangue na CCM wakae kwao na CUF wakae kwao. Ni wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho kwa taarifa zetu ndio uliosema hili haliwezekani, huu si utaratibu.

Mhe. Spika, kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani, tunakupongeza sana, wewe ni mstari wa mbele wa kulinda amani na umoja wa Wazanzibari na niseme kwamba watu wasijidanganye amani haizungumzwi mdomoni, amani iko ndani ya moyo wa kila mtu. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe kama kuna mtu tunamshukuru sana kwa Baraza hili Mhe. Pandu Ameir Kificho ametuashiria hilo zamani. Hili tumeliona kule Dodoma yeye alikuwa mstari wa mbele katika kutusaidia kutuweka pamoja.

Mhe. Spika, ndani ya ujana wangu mimi sikuwahi kuvuta bangi au sigara,lakini nasikia wale waliopitia mchezo ule pale unapomaliza kuvuta, basi watu wote unawaona wadogo na wewe ndie mkubwa. Kwa hivyo, tusilewe na madaraka tukawaona watu wote wadogo, sisi ndio wakubwa, watu wote wanahaki sawa kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa.

Mhe. Spika, nadhani tulinde amani kwa vitendo na sio kusema mdomoni.

Mhe. Spika, niende kwenye Tume ya Uchaguzi ambayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amezungumza kwamba kuna mpango wa kuangalia upya mipaka ya majimbo.

Mhe. Spika, jambo hili hufanyika duniani kote, lakini kwa viashiria vikubwa viwili. Kwanza kwa idadi ya watu, lakini pili kwa jiographia ya majimbo husika. Sasa mimi nimetumia sensa ya mwaka 2012 ambayo ninayo. Wazanzibari kwa mujibu wa sensa hii ni milioni 1.3. Mkoa wa Mjini Magharibi una watu laki tano tisini na tatu nukta sita saba ambayo ni sawa sawa na majimbo 19, ukigawa kwa majimbo kumi na tisa ni wastani wa jimbo la Mjini Magharibi ni watu thalathini na moja elfu mia mbili na arubaini na sita. Mkoa wa Kaskazini Pemba una watu laki mbili kumi na moja elfu mia saba thalathini na mbili, majimbo tisa kwa wastani wa watu elfu ishirini na tatu mia tano ishirini na tano kwa kila jimbo.

Mhe. Spika, Mkoa wa Kusini Pemba una watu laki moja sitini na tano elfu mia moja kumi na sita. Majimbo tisa wastani wake ni watu ishirini na mbili elfu. Mkoa wa Kaskazini Unguja una watu laki moja thamanini na saba mia nne hamsini na tano, Majimbo manane wastani wake una watu elfu ishirini tatu mia nne na thalathini na moja na Mkoa wa Kusuni Unguja una watu laki moja kumi na tano elfu mia tano thamanini na tano, wastani wa watu ishirini na tatu elfu kwa majimbo matano.

Mhe. Spika, kwa hivyo, Mikao yote minne ya mashamba ina wastani ya wapiga kura sawa sawa na kijigoraphia Mikoa yote minne ya mashamba inafanana. Mkoa ambao una watu wengi ni Mjini Magharibi ambao una watu laki tano na tisini na tatu kwa majimbo kumi na tisa wastani wa thalathini na moja elfu mia mbili na arubaini na sita.

Mhe. Spika, kama hiyo ndiyo hoja, Mkoa wa Mjini Magharibi baina ya Jimbo la Mji Mkongwe na Jimbo la Rahaleo hapana barabara hata moja inayofika kilomita nne, kwamba jimbo na jimbo kilimita nne hakuna barabara, ni tafauti na majimbo ya shamba ambako Chwaka na makunduchi ni kilomita nyingi. Kwa hiyo, vile vile, kijiographia hakuna hoja na kama idadi ya watu, ndio kigezo, naomba niwaambie Tume na Serikali Mkoa wa Dar-es Salam kwa mujibu wa sensa una watu milioni nne, lakini tatu sitini na nne elfu kwa majimbo manane sawa sawa na wastani wa watu laki tano na arubaini na tano elfu mia tano kwa kila Jimbo.

Mhe. Spika, lakini Mkoa wa Lindi kwa mujibu wa sensa una watu laki nane sitini na nne kwa majimbo sita, ni sawa sawa na wastani wa jimbo moja watu laki moja na arubaini na nne. Kama kigezo ni watu wengi maana yake Mkoa wa Dar-es Salaam kungekuwa na majimbo thalathini ikiwa Lindi na Majimbo sita maana yake Dar-es Salaam imezidi Lindi mara tano.

Mhe. Spika, kwa hiyo, sio hoja idadi ya watu, mimi nimepiga kura kuanzia 1990, ni mwaka mmoja tu wa 2010 chini ya Mhe. Aman Karume ndio ambapo Wazanzibari hawajauwana, hawajapigana,miaka mingine yote Wazanzibari wamegombana, wameuana na wamehasiana na ukichunguza kitaalamu ni sababu ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, naungana sana na Mhe. Omar Ali Shehe kunasihi sana serikali msitupeleke huko tena, kwa sababu za kitaalamu za ugawaji majimbo hazipo, labda kuwe na lengo la kusababisha watu waendelee kugombana na kupigana, msitupeleke huko tena. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nasema haya ili iwe kumbukumbu yakitokezea watu waseme Hija Hassan Hija alisema msitupeleke huko tena,ikiwa sababu za takwimu ndio hizo za kitaalamu, ikiwa sababu za kijiographia ndio hizi hamna sababu ya msingi labda iwe mna sababu ya kutaka watu warejee kule walikotoka.

Mhe. Spika, naomba sana chonde chonde Wazanzibari msitupeleke huko tena kwa kweli hatutaki hilo.

Mhe. Spika, hoja ya pili, ni uandikishaji wa wapiga kura, Mkoa wa Mjini Magharibi umeandikisha vyeti ya kuzaliwa kwa mujibu wa sensa hii asilimia 81.9. Mkoa wa Kusini Unguja umeandikisha vyeti vya kuzaliwa asilimia 71.7. Mkoa wa Kaskani Unguja asilimia 67.3, lakini Pemba Kaskazini ni asilimia 59.3 na Kusini Pemba yangu mimi asilimia 54.3, ni dhahiri kwamba Mikoa yote miwili ya Pemba kasi ya vyeti vya kuzaliwa ni ndogo na sababu ni moja tu watu wanadhaniwa kuwa hawa wapinzani watapiga kura.

Mhe. Spika, kwa hiyo, takwimu hizi zinaonesha wazi kwamba kwa namna yoyote ile wananchi wa Pemba wamekuwa wakibaguliwa kitaalamu. Wakifuatiwa na wananchi wa Kaskazini Unguja wanabaguliwa kitaalamu. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakuomba sana Mzee wangu usitupeleke huko, wananchi wanabaguliwa kwa

uandikishaji kwa sababu ukiandikisha cheti cha kuzaliwa, maana yake unapata haki za kupiga kura. Kwa hiyo, mnanyimwa kitaalamu ili wasipate haki yao, bado mnasema nchi ina amani.

Mhe. Spika, amani si kupigana tu, unapomnyima mtu haki yake ya msingi, hiyo sio amani, msidhani kwamba amani ni kupigana tu. Amani ni manunguniko ambayo yamo ndani ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, niende Baraza la Wawakishi, naomba sana Wawakilishi wenzangu wanivumilie na huu ni mchango wangu na ni maoni yangu. Mimi siungi mkono na natanganza kabisa kabisa natoa pesa zote ambazo zilitengwa kwa Kamati Teule nafuta, pesa zote zilizotengwa kwa safari za nje za Wawakilishi nafuta na pesa zote za nyongeza ya *PAC* zipunguzwe. Kwa nini nafuta pesa za Kamati Teule? Kamati Teule hizi zimekuwa zikifanya kazi kubwa ...

Mhe. Spika: Mheshimiwa unazo dakika tano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naheshimu sana, lakini naona saa inakwenda *Speed* sana kwa dakika tano, lakini nashukuru.

Mhe. Spika, Ripoti za Kamati Teule zimekuwa zikitumia pesa nyingi, lakini hakuna matunda. Kwa hiyo, naomba Wawakilishi wenzangu bajeti hii 2014/15 Fedha ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ifute, fedha za safari za nje zifutwe na fedha ya *PAC* zipunguzwe ziwe sawa sawa na za Kamati nyengine.

Mhe. Spika, jambo jengine ni matumizi ya serikali, Wizara ya Fedha imekiri kwamba matumizi ya serikali ni makubwa na naomba nihoji matumizi haya hasa safari za nje, hivi leo kuna watu wanaitana wafanyakazi wa ndege, leo Emirates, kesho Qatar, kesho kutwa Dokha, keshokutwa *Ethiopian Air line,* watu wanabadilisha ndege juu yaa anga na ndio maana zipo taarifa kwamba safari moja tu ya ziara ya Makamu wa Pili wa Rais kwenda Marekani, serikali ilitumiwa Dola laki tatu hamsini elfu, naomba tusahihishwe kama hilo ni kweli.

Mhe. Spika, mimi najiuliza kuna haja gani safari kama hiyo kwenda watu 30 kwa *trip* moja. Jana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati safari hii anaisifia kwamba serikali imeingia *Computers* 250 kwa matumizi ya dola laki tatu hamsini karibu milioni mia tano na kidogo. Jambo ambalo angepelekwa Waziri mmoja angepata *Computers* 250, *Computers* 700 mpaka *Computers* 1000.

Mhe. Spika, matumizi haya si halali kabisa, watu lazima wazingatie uhalisia, uchumi wetu na mapato ya nchi na wananchi wake.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa na kulingana na muda ni suala zima la uwezeshaji wananchi. Mwisho kule kuna suala zima la wananchi waliosaidiwa, kuna kiambatanisho kule, kuna Shehia moja ya Shamiani Mwambe ambayo imo katika Jimbo langu, kuna kata zimesaidia fedha. Fedha iliyotengwa na kutolewa ipo, lakini kwa wananchi waliopewa ile fedha kuna vichoro huku kwa manaa na *dash*. Naomba Ofisi ya Makamu ya Pili wa Rais wanieleze ni kwa nini fedha ilitolewa, lakini wananchi wangu hawakupata fedha ile.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusisitiza kwamba Tume ya Uchaguzi iwe makini isiwarejeshe watu walikotoka, Wazanzibari wamechoka na matatizo na kila mtu akiudhiwa anaweza akakasirika, usitupeleke huko na kwamba Wawakilishi mkubali kwamba fedha za *PAC*, fedha za Kamati Teule, fedha za safari za nje za Wawakilishi zifutwe hazina tija kwa manufaa ya Wazanzibari wote. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii kusema machache katika kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuingia katika mchango, naomba niwakumbushie Wajumbe wenzangu kwamba tunapochangia hapa tutilie maanani ile Kanuni ya 59 (3) inayosema kwamba Mjumbe yoyote anapokuwa akisema barazani, atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu.

Mhe. Spika, Mjumbe aliekaa kabla ya kuzungumza Mhe. Hija Hassan Hija alisema kwamba Mhe. Salmin Awadh, Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi amepewa agizo alete mswada wa kufuta Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, nashukuru Mhe. Hija Hassan Hija alipokuja amelieleza vizuri kwamba Mhe. Salmin awadh ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na ana haki ya kuhoji na kuleta mswada wowote anaojisikia kuleta kama ni Mjumbe anaewakilisha wananchi wa Jimbo la Magomeni.

Mhe. Spika, kwa hiyo, nimeona tu niwakumbushie Wajumbe wenzangu Kanuni ya 53, ili wakati wakichangia wawe wana uhakika na wanayoyasema.

Mhe. Spika, kwa kuanzia kwanza nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Waziri pamoja na watendaji wote kwa kuleta hotuba hii, Lakini pia, kwa uwasilishaji mzuri ambao umewasilishwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, nataka nianzie na hali ya siasa, naunga mkono hotuba ya Makamu sambamba na Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba hali ya siasa sasa ni ya utulivu na amani na hii imetokana na uwelewa mkubwa wa wananchi kutambua kwamba amani na utulivu ni muhimu katika kuendeleza Taifa letu.

Mhe. Spika, lakini pia, naomba niwakumbushe baadhi ya Wajumbe hapa kwamba amani hii na utulivu ambayo imedumu kwa miaka 50, sasa imetokana na mfumo mzima wa Muungano wetu ambao ni wa serikali. Kwa hiyo, niwaombe wananchi kwa namna yoyote ile wasikubali kuvunja amani hii kwa kutaka kuleta mambo yasiyofahamika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, waswahili wanasema "Mchuma janga hula na nduguze" kuna baadhi ya watu huja Zanzibar huku na kuleta chokochoko za siasa kwa makusudi ya kutafarakanisha Taifa letu,lakini watu hawa hawa hawakai hapa wanakuja wanatia chokochoko, halafu wanaondoka, likitukuta ndio lile janga ambalo tutakuwa tumelichuma na ndugu zetu wao hawapo wengine wapo Singida, wengine wako Tabora, wengine wako Kilimanjaro hawapo kabisa.

Mhe. Spika, baada ya kumaliza hilo, naomba niongelee suala la Muungano. Kuna baadhi ya Wajumbe wamesema hapa kwamba pamoja na kwamba wamepongeza jitihada za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi nzuri ambayo wanaifahanya ili kuhakikisha kwamba kero za Muungano zinaondoka.

Mhe. Spika, lakini pia, wako waliobeza jitihada hizi, lakini mimi nilikuwa nataka kusema tu mabadiliko ni *Process*, yaani huwezi ukalala zaidi ya masaa manane, halafu ukakuta siku ya pili ukiamka kila kitu kiko sawa. Mabadiliko ni *Process* kama kuna kero ambazo zimeshughulikiwa, ndio zimeshashughulikiwa, lakini kuna kero ambazo tumeambia ziko katika *Pipe line* zinaendelea kushughulikiwa na hivyo tuamini kwamba kama zipo zilizoshughulikiwa na zikamalizika, tuamini pia kwamba zipo hizi ambazo zilioko kwenye *Pipe line* zitashughulikiwa na zitamalizika.

Mhe. Spika, hata hivyo kero haziishi, unamaliza leo kesho zinakuja nyengine, ndio maana nikasema kwamba mabadiliko ni *Process* mna-*solve* hili na jengine linatokea.

Mhe. Spika, baada ya hapo, naomba niingie kwenye Ofisi ya Faragha. Ofisi ya Faragha katika majukumu ambayo imejipangia, naomba nipe muda kidogo natafuta hiyo sehemu ambayo Ofisi ya Faragha ipo.

Mhe. Spika, katika majukumu ambayo imejipangia moja tumeona kwamba imejaribu kufatilia ahadi za Viongozi wakuu, nimeshaiona ukurasa wa 28, moja kati ya kazi ambazo imeshughulikia ni Ofisi, imeratibu na kufatilia ahadi 11 zilizotolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kati ya hizo ahadi 7 zimetekelezwa.

Mhe. Spika, tunavyofahamu kwamba tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu 2015. Hizi ahadi za Viongozi Wakuu ni moja kati ya kero ambazo zinawakera wananchi wanapoahidiwa mambo, halafu yasifikiwe kama yalivyoahidiwa. Sasa naomba nilikuwa naangalia malengo ambayo wamejipangia Ofisi hii kwa mwaka 2014/15 sijaona kwamba zile ahadi 4 zilizobakia kwamba zitakwenda kushughulikiwa katika kipindi cha 2014/15. Zipo 7 ambazo zimeshughulikiwa, lakini 11 - 7 kuna 4 ambazo hazijashughulikiwa.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba kwamba ahadi hizi zishughulikiwe kabla hatujafika 2015 ili kuona kwamba zile ahadi ambazo viongozi wetu wameziahidi kwa wananchi zinapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, naomba niingie katika Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali. Hapa nina maswali machache tu kuhusu mradi wa *TASAF* ambao katika maelezo yao wamesema kwamba idara imesimamia utekelezaji wa mradi wa *TASAF* awamu ya tatu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

Mhe. Spika, kwanza Mhe. Waziri akija nilikuwa naomba anieleze kwamba ni vigezo gani vinatumika kutambua hizi kaya maskini, lakini la pili ni kiasi gani cha fedha ambazo kila kaya inalipwa inapogundulika pale kwamba hii kaya inastahiki kulipwa na ulipaji huo nilikuwa nataka kujua kwamba kuna *rate* maalum, yaani kuna *flat rate* wanalipwa kwa wote au inategemea na ule umaskini wa mtu, maana kuna umaskini na ufukara kila siku Mhe. Suleiman Hemed Khamis anasema. Sasa nilikuwa nataka kujua kwamba wanalipwa kiwango kimoja au inategemea na ule umaskini wa kaya.

Mhe. Spika, lakini jengine katika kiambatanisho 3A cha huu mradi wa *TASAF* nilikuwa naangalia idadi ya kaya zilizoorodheshwa pamoja na idadi ya kaya zilizopokea malipo, lakini pia, kuna kaya zisizopokea malipo. Nilikuwa nataka kujua ni kwa nini kaya zinaorodheshwa, lakini zipo ambazo zinalipwa na nyengine hazipokei malipo.

Mhe. Spika, nilitaka kujua sababu kwa nini hizi kaya zinaorodheshwa, lakini kuna baadhi zinapokea malipo na baadhi zisizopokea malipo na kama kuna sababu zozote zinazosababisha hivi, ni kwa nini waziorodheshe zile kaya zote? Kwa nini wasiorodheshe zile ambazo zinastahiki kulipwa tu na zile nyengine wakaziacha? Nilikuwa naomba maelezo kwa sababu hii haileti ufahamu mzuri na mmeshasikia watu wengine wameanza kusema kwamba wanadhani huu mradi ni pesa tu ambazo wakubwa wanataka kuzipiga kuni? Lakini mimi siamini hivyo, isipokuwa nilikuwa nataka tuelezwe tu ule utaratibu mzuri ambao unatumika katika kugawa haya malipo kwa kaya za maskini.
Mhe. Spika, nikimaliza hapa nataka niingie katika Idara ya Upigaji Chapa. Nilikuwa naangalia Idara ya Upigaji Chapa, mapato yameshuka kwa kiasi kikubwa sana na yameshuka kwa sababu wameelezea kwamba kulikuwa kuna zoezi la uhamishaji wa mashine kutoka pale zilipokuwa kwenda sehemu mpya ambayo wamehamia, lakini nilikuwa nataka kujua kwamba wao walijua kuwa watahama na kwa nini walijiwekea malengo makubwa sana, nafikiri ya milioni 500 kama sikosei.

Mhe. Spika, unajua hii haileti picha nzuri, kama mmeshajua kwamba nyinyi mna mpango wa kuhama. Kwa hiyo, kiwanda hakitofanya kazi, kwa nini walijiwekea kiwango kile kikubwa cha fedha, halafu badala yake kukawa kuna kiwango cha chini cha makusanyo ya mapato? Lakini pamoja na hayo, nilikuwa natoa wito tu kwa idara hii kwamba mwaka huu ichape kazi ipasavyo ili kuona kwamba ile *difference* iliyopotea katika mwaka ule kwa sababu ile ya kuhama ione kwamba *at least* inakuwa *covered* katika mwaka huu wa 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nilikuwa naangalia ukusanyaji wa mapato wa Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Kuna mapato yanayopatikana kutokana na utafiti unaofanywa na watafiti wetu katika Idara ya Nyaraka. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na kila siku tunapokwenda katika Idara ya Nyaraka tunasikitishwa sana na ile hali ambayo tunaikuta ya Idara ile. Sasa tulikuwa tunawaambia kwa nini hii ada ambayo inakusanywa hapa isitumike angalau kwa kuweka mandhari mazuri ya lile jengo na mambo mengine ambayo yanayohitajika pale? Tukaambiwa kwamba pale watafiti wanakwenda wanafanya tu utafiti wao, wanapokea kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini sasa nilikuwa nataka kujua ni mapato ya kiasi gani ambayo yanapatikana kutokana na tafiti ambazo zinakuja kufanywa katika Idara ile?

Mhe. Spika, lakini nimeangalia sehemu ya mapato hapa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais sioni mapato hayo. Kwa hiyo, inaonekana kama mapato hayo hapa hakuna, lakini pia, kule katika Idara ya Nyaraka pia hayapo. Nilikuwa nataka kujua kwamba haya mapato yanaingia wapi? Mhe. Waziri, akija hapa aelezee.

Mhe. Spika, kwa hayo, machache nakushukuru na naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Assaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa dhati kabisa kwa neema yake aliyotujaalia ya uhai na uzima tukapata nafasi ya kuendelea na shughuli tuliyokabidhiwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, nimshukuru sana na kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ofisi yake na watendaji ambao ndio sifa anazozipata kazi nzuri wanayoifanya watendaji hao. Naamini timu iliyopo huko ina uwezo mkubwa, sasa ni juu ya serikali kuwawezesha ili wakafikia malengo yaliyowekwa.

Mhe. Spika, Wawakilishi wa Baraza lako tukufu wameshasema mengi mazuri na serikali inasikia na serikali hii ni serikali sikivu, basi ayasikie ili watakaojaaliwa *Inshaallah* mwaka kesho yasiwepo tena ama yabakie machache sana.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze hapa kwenye Ukimwi, Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya na Mazingira. Kwa sababu kitabu kimejaa mazuri mengi na muhimu nitajitahidi kugusagusa.

Mhe. Spika, bado tuna hatari kubwa ya janga la ukimwi, maisha ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla wake nguvu kazi vijana na bahati mbaya si vijana peke yao na wazee pia.

Mhe. Spika, suala la ukimwi na dawa za kulevya lina kasi kubwa wanayoita michepuko na michepuko hasa kwa vijana inawakumba kutokana na ukosefu wa ajira. Sasa juhudi hizi zinazoendelea za serikali na hata wenzetu wanaosaidia kutoka nje, zinaweza zikafika mahali zikagonga kufuatana na kasi kubwa ya ongezeko linavyokwenda.
Mhe. Spika, kwa wenzetu wanaotumia madawa sasa ya gonjwa hili, afya zao hunawirika na bahati mbaya inaweza kuwa ni kivutio, lakini hapo hapo kumbe ndio janga lenyewe kwa yule ambaye bado hajakuwa nalo.

Mhe. Spika, nadhani bado serikali hili hebu ilitizame tena kwa kina kirefu, lakini kichocheo kikubwa nacho ni dawa za kulevya. Suala la madawa mimi napata tabu sana hadi sasa kuamini kwamba limeshindikana kiasi hichi.

Mhe. Spika, napata tabu, natizama wakati ule wa msimu wa uvunaji wa karafuu, serikali inavyochukua hatua vikosi vyote vya ndani hivi vya SMZ na vile vya Muungano kwa pamoja vinashirikishwa kuhakikisha kwamba konde moja ya karafuu haitoki ndani ya visiwa hivi, lakini nashindwa kuelewa kwa nini makontena ya madawa za kulevya yaingie? Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali, jamani tusaidianeni, hebu tunaangamia kwa kasi kubwa, wanaoangamia ni watoto wetu, sisi na Taifa.

Mhe. Spika, mazingira visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kijiografia maumbile ndio hayo, sisi wenyewe tunaongezeka siku hadi siku tena kwa kasi ya labda asilimia 2 nukta ngapi. Tusipokuwa makini na jana nilikwambia Mhe. Spika, miongoni mwa wanaotajwa na wewe umo, umo kwa maana dhima ya nchi hii, wewe ni kiongozi mkubwa.

Mhe. Spika, ushauri huu mnapokaa mshauriane, Wazanzibari wanaongezeka, lakini visiwa vinamong'onyoka siku hadi siku, lakini kuna mambo ni uzembe na dharau tu basi, hakuna hatua zinazochukuliwa, watu wanatizamwa nyusoni ni bwana gani, ni mtoto wa kina nani, basi kwake kuvunja sheria ni halali yake. Haya ni maradhi na dawa yake sijui nini, lakini yanaangamiza yanaumiza.

Mhe. Spika, nimefarajika sana na kitabu cha hotuba. Nilianza pale kwenye sherehe zetu zilizopita za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu.

Mhe. Spika, tumefanikiwa, Mapinduzi yalileta heshima, utu wa Muafrika mweusi wa visiwa hivi. Ndani ya mafanikio yaliyotajwa na malengo ya Mapinduzi haya yanawezekana kabisa, bado dhamira ni njema, lakini utekelezaji wake bado, ama kwa makusudi na ni makusudi kuliko bahati mbaya.

Mhe. Spika, dhana ya Mapinduzi kwa idhini yako nanukuu kidogo kuleta maisha bora pale, lakini kuondoa ubaguzi. Suala la ubaguzi mama yangu Asha Bakari Makame katoka nje, kama linamuuma sana, bado namwambia lipo na linafanywa kwa makusudi.

Mhe. Spika, mtoto wangu mimi Asaa mwaka juzi kamaliza chuo hichi hapa cha Karume Mbweni kaondoka na *grade two*, hajawahi kufeli hesabu toka siku aliyoripoti, anaondoka anarudi, hivyo vyeti siku vimetolewa anaambiwa umefeli hesabu. Siku ile aliyochukua cheti kaja nyumbani na furaha kubwa hajaona viliomo, maana walisoteshwa nenda rudi.

Mhe. Spika, hivyo, kuna mambo nashindwa hata kusema, maana ni aibu kubwa, siku aliyopewa nikakipitia nikamwambia mbona hesabu umefeli na wewe unajilabu hapa, anasema mimi sijawahi kufeli hesabu, nikamwambia hii hapa, nenda tena, rudi, alipofika chuoni akaulizwa umejuaje? Kumbe ilikuwa imepangwa, anaulizwa ulijuaje na sisi tulifanya siri.

Mhe. Spika, papatu hiyo ikaonekana kwenye kumbukumbu ni kweli hajawahi kufeli, ilipotolewa hiyo kwa nafasi aliyoondoka nayo pale, apewe mkopo kwa masomo ya juu, lakini ile asipewe, akwamishwe tena jina lake kule . Jina lake kule *NECTA* hadi hivi nazungumza mimi hapa baba yake halijapelekwa, natoa mfano wa mtoto wangu mimi mengine nanyamaza.

Mhe. Spika, lakini nataka niseme tu ninapokutaja kwa jina, bado haya mambo yanaendelezwa na kwa makusudi kabisa. Hilo la ajira hayasemeki, nafasi za ajira vijana kule Pemba, tukaja tukasikia hapa Unguja kwamba kulikuwa na ajira hii, kulikuwa na polisi, kulikuwa sijui na majeshi, maana wakija hao majeshi wanakuja na watu wao tayari, leo ni KMKM tunaona hayo, hivi ni kweli haki hawana vijana hawa.

Mhe. Spika, haya mambo yanafurahisha kuyafanya kwa sababu unamdhalilisha na unamnyima haki yake, lakini ubaya wake ni mkubwa mno na tungekuwa tumeyakataa kweli kwa kumuenzi Mzee Abeid Amani Karume kama alivyofanya yeye leo miaka 50, tusingekuwa na sababu ya kuyazungumza tena, maana yangekuwa hayapo.

Mhe. Spika, lakini kwa sababu yanaendelezwa tunayazungumza watoto wetu wanayasikia na wao wata-*revenge* na wajukuu na hivyo, lakini sababu inatokana na nani? Ni sisi tuliopo hapa sasa, ndio pale ninaposema Waheshimiwa nyimbo mbaya hachombezewi mtoto.

Mhe. Spika, naomba unielewe sana kwa nia safi kabisa, hakuna haja kwenda kutafuta adhabu isiyo sababu, hawa ni waja wa Mwenyezi Mungu, kama una mengine unayoyaona wewe mhukumu kwa hapa duniani, usimnyime haki yake, usimnyime kwa asili yake, usimnyime kwa jina lake.

Mhe. Spika, dhana ya Mapinduzi, Mzee Abeid Amani Karume baada ya Mapinduzi aliwaambia mawaziri waoeni hao wale weupe, matunda yamo mpaka humu ndani ya Baraza lako tukufu na matunda yale hayakuibuka tu, wala hatuna sababu ya kudharauliana.

Mhe. Spika, na-*challenge* mimi leo, hebu na asimame miongoni mwetu atwambie kwa fahamu yake babu yake yupi? Ama bibi yake yupi? Alichangia kipi mpaka siku ile ya tarehe kumi na mbili tukafika hapa tulipofika leo, hebu na aseme. Mimi Asaa ninao uwezo huo, mimi Asaa Othman bin Hamad ninao uwezo wa kulabu hapa na kama ukiniruhusu nitafanya hiyo kazi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, yaliyopita yamepita, sasa tugange yajayo. Tugangeni uchumi na siasa ni uchumi, siasa sio hasama. Mfuko huu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, huu mfuko unavyotolewa kuwafikia hao walengwa sivyo, umejazwa siasa, umejazwa upendeleo, rushwa balaa, maana yake Zanzibar hii ni nakama na inaletwa na Zanzibar tu, tena anayeongoza nchi. Hii ni balaa, ni hatari sana. Hivi tutakwenda hivi hadi lini? (*Makofi*)

Mhe. Spika, hebu chonde chonde, hayo tunayoyakimbilia hatimaye tutayaacha hapa, kila mmoja atakayejaaliwa. Mfuko ni ule wa pipi, unalazwa chini hata kama mvua inanyesha, watu maji watayatoa na utalazwa utaacha yote. Hivi unarapa, unarapia nini na hatma yako umekuja kwa udongo na utarudi kwa huo huo. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Unazo dakika 5.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, ni tano au ni kumi? Mimi sizijui. (*Kicheko*)

Mhe. Spika: Ni mkono mmoja wa dakika.

Mhe. Assaa Othman Hamad: Mhe. Spika, ninakuja kwenye maafa haraka haraka. Kitengo ni muhimu sana. Tunaishi ndani ya visiwa na nimetangulia kusema bahari inavila visiwa hivi tena kwa kasi kubwa. Tunakubaliana kwamba kuna mabadiliko ya tabia ya nchi, lakini kumeingia na mengine ya tabia ya ubinadamu, ndio inayoleta hiyo nakama ya visiwa kutafunwa na bahari.

Mhe. Spika, tabia ya binadamu ni haya mengine niliyoyataja, nafsi za wanadamu na bahati mbaya zikiingia kwa watu wakubwa kama walio ndani ya nyumba hii huzidi. Tuna kila sababu ya kujitizama mara tatu, kumi, kumi na tano, ili heri ya Mwenyezi Mungu iingie ndani ya visiwa hivi.

Mhe. Spika, maafa tunashuhudia, tena makubwa. Kwa visiwa hivi ni mazito mno. Ninaiomba serikali ione umuhimu wa eneo hili, maafa yetu yapo baharini kwa asilimia kubwa, lakini kwa sababu pia kushindwa kutunza miji yetu, mipango miji mibovu na inayovunjwa na watu wakubwa wenye akili zao timamu.

Mhe. Spika, maafa haya ya majanga haya ya moto na uchafu uliotushinda kuisimamia na kuidhibiti ndani ya miji yetu mikuu ni majanga mengine ya kuleta madhara na juzi nilimwambia Sayyidina Omar kuwa afya ya binadamu ni sehemu moja ya kujenga uchumi wa Taifa, afya za watu wetu ni mbovu, tena mbovu sana hasa akina mama ambao wanasulubika kutafuta riski za watoto na waume zao, hawa mama zetu wana shida kubwa sana, leo barabara zetu sijui Mheshimiwa gani, hata kufagiwa na kufanyiwa usafi barabara inashindikana kweli? (*Makofi*)

Mhe. Spika, ningekuwa mimi Rais, *Wallahi* ningemfukuza kazi huyu mtu, barabara hizi gharama namna hii, barabara ya lami si mchezo, barabara hii ya Mombasa hebu twendeni tukaiona ni aibu tupu, tunashindwa hata kuisimamia barabara jamani! Tutaweza kuwasimamia wananchi hawa jamani! Hii si aibu, ni kitu gani?

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, unayehusika na mambo hayo, tunakuomba sana tafadhali hebu tufunike angalau kuna wageni visiwa hivi, tunawakaribisha na tuna shida nao kubwa kwa maendeleo yetu ya leo na kesho na watoto wetu.
Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna dhamana tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, sio wenzetu tu, wenzetu wamebarikiwa watubarikie sisi. Chokochoko, mdomo mdomo, kilimilimi, cheche ndio inayozaa moto.

Mhe. Spika, ninakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe nchi hii tuipelekeni salama na wenzetu wabaki salama na amani ili tupate heri ya Mwenyezi Mungu, lakini kama hivyo akiona mtu sivyo, hewala na afanye atakavyo yeye, lakini Mwenyezi Mungu huchagua huko mbele, mwanzo hutupeleka sote kwa pamoja.

Mhe. Spika, ninakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Saleh Nassor Juma, baadae Mhe. Ali Abdalla Ali na hatimaye tumsikilize Mhe. Viwe Khamis Abdalla.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa ya kuweza kueleza machache katika hii hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kama ingelikuwa serikali ni gari, basi *engine* yake ingelikuwa hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kabisa kabisa. Kama serikali ingelikuwa ni chombo cha moto, basi *engine* yake ingekuwa ni hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo, wizara hii inataka umakini mkubwa sana katika kuiendesha na katika kuisimamia. Napenda kwanza nichukue fursa hii kumpa pole nahodha wa hii ofisi kutokana na jinsi anavyoendesha mambo yake katika mazingira magumu sana. Sisi hapa kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tupo pamoja naye katika kuona kwamba, pamoja na hali mbaya ya uchumi, pamoja na mazingira mabaya sana ya nchi yetu katika masuala ya uchumi kwamba tuna-*support* bajeti zenu kuona hawa Wazanzibari kupitia *GNU* wanapata kile wanachokihitaji. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama vile vile sikumpongeza Waziri katika ofisi hii, mdogo wangu hapa na mpiga kura wangu Mohammed Aboud Mohammed. Kwa kweli huyu kijana ile kuwepo kwake katika ile wizara inayohusiana na Afrika na Mashariki ilimsaidia sana kupata maarifa mazuri kwenye masuala ya diplomasia na masuala ya haki ya *Public relations*. Hata pale anapotujibu maswali yetu asubuhi. Kwa kweli mimi nimevutika sana na mpiga kura wangu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed. (*Makofi*).

Mhe. Spika, na kwa niaba yangu na kwa niaba ya mama yake Cholo, yaani mke wangu pamoja na familia na wapiga kura wote, pamoja na walipa kodi wa nchi hii tunakupongeza sana Sheikh Mohammed Aboud Mohammed kwa kazi yako kubwa unayoifanya.

Mhe. Spika, baada ya hiyo, nadhani sasa niende katika hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nianze na huu ukurasa wa 4 katika Ibara ya 8, hii hali ya siasa. Hapa pamezungumziwa uwepo wa amani na utulivu katika nchi. Kama kuna kitu ambacho huwezi kukinunua kwa thamani yoyote, huwezi kukipata kirahisi hata uwe na dola hata uwe na shilingi ngapi, huwezi kukipata kirahisi, basi ni amani na utulivu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kama kuna kitu kinachohitaji kuenziwa, kuthaminiwa na kukijali kama tayari kipo, basi ni amani na utulivu. Ninasema hivyo kwamba amani na utulivu ikipotea katika nchi, basi kupatikana kwake ni taabu mno.

Mhe. Spika, mimi kwanza ninachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo sasa hivi ina umri wa miaka minne hii, tangu *GNU* ikae madarakani, mimi nashukuru kwamba ninapata kutembea vizuri barabarani. Ninafurahi sana kuona ninapata kutembea hapa Unguja na nikatembea na *wife* hapa, nikapita kila kichochoro bila ya kubughudhiwa wala kunyanyaswa.

Mhe. Spika, nimefurahishwa sana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa tangu akae Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein na serikali hii sijawahi hata kwenda jela hata mara moja katika kipindi hichi cha miaka mitano ambapo katika awamu zilizopita hata vikimaliza vipindi vitano, basi nishakwenda jela mara nne au tano, almuradi mashaka tu. (*Makofi*)
Mhe. Spika, nashangaa sana kwamba wanakuja watu wanataka kuichezea hii amani iliopo, mimi naamini kwamba nilichofaidika nacho katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni utulivu na amani, si jengine lolote. Mimi kama Saleh ni Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na wapiga kura wa Jimbo la Wawi, tulichofaidika na hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni amani na utulivu, si chochote.

Mhe. Spika, mimi hapa sikuletwa na *GNU*, nimeletwa na wapiga kura wa Jimbo la Wawi na nilipoingia hapa sikupata uwaziri ni *backbencher* na munaona kazi ninayoifanya hapa kwa niaba ya wananchi. Kwa hivyo, nilichofaidika nacho ni hicho tu mimi kabisa kabisa. Sasa anapokuja mtu akaanza kuchezea kitu hichi amani na utulivu ambacho kwa kiasi kikubwa sana imechangiwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, anahitaji kwenda Hospitali hapa Kidongo Chekundu kwa sababu atakuwa ana tatizo la ubongo na ikiwa yupo Bara, basi tumpeleke Merembe akafanyiwa *checking*, atakuwa na tatizo la ubongo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, inasikitisha kwamba leo unaleta hoja ya kuondosha *GNU*. Wakuu wa Mikoa kule Pemba na hata katika maeneo mengine hapa Unguja walikuwa hawathubutu kutembea katika mikoa yao bila ya kuwa *group* huku la maaskari. Leo hii Mkuu wa Mkoa Kaskazini, Mkuu wa Mkoa wa Kusini anakuja wilayani kwake kufanya ziara kule Pemba akiwa anatembea kwa miguu na zawadi za ndizi anachukuliwa mpaka kwenye gari yake, imetuunganisha *GNU*.

Mhe. Spika, leo unataka kuiondosha hapa na ije hiyo hoja ya kuondosha *GNU* na ije hiyo hoja ya kuwahoji Wazanzibari kuhusu Muungano na zije sambamba. Mimi nitakachofanya ni ku-*turn mind set* yangu tu, kurudi pale pale kwenye, "Ngangari ngangari pale pale, jino kwa jino vile vile, nitarudi tu hapo kabisa kabisa. Sina tatizo. (*Kicheko*/*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya hapo niende pengine kidogo. Sasa niende kwenye masuala haya ya Muungano, tangu Muungano huu uasisiwe, kama kuna watu wanapoteza katika nchi yao ni sisi...

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe unapotaka kunukuu wimbo, basi unasema angalau naomba kunukuu kitu fulani, lakini unaanza tu mpaka. Endelea bwana. (*Kicheko/Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika, kama kuna watu wanaendelea kupoteza na kudharauliwa na Watanganyika, basi ni Wazanzibari.
Mhe. Spika, huu ni Muungano wa nchi mbili, yaani Tanganyika na Zanzibar. Inatakiwa kila *cake* inayopatikana katika Muungano huu, iwe *evenly distributed*, huku wapate na huku wapate, ijapo kwa uwiano, lakini sio kama tena wachukue kwa mapande.

Mhe. Spika, kama kuna watu wana akili sana katika hii Tanzania, basi ni sisi Wazanzibari. Ninadhani kwa kutumia hivi vitu vya bahari vinatusaidia sana kuwa na akili, tena katika kila fani.

Mhe. Spika, tangu Muungano huu uasisiwe inasikitisha sana kuona sisi hatujatoa na hatujawahi kutoa viongozi wakuu wa vyombo vya ulinzi, wakati wenye uwezo huo wapo makamanda wenye uwezo huo wapo. Sisi tulikuwa na Brigedia Yussuf Himid katika uhaki wao, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. Alikuwa na uwezo huo tangu miaka hiyo. Sasa tunao zaidi kwa sababu wana taaaluma na uwezo wa kuongoza mapambano ya kijeshi, kwa nini tushindwe na kuwa na *CDF* hapa tangu Muungano huu uasisiwe? Kwa nini tushindwe kuwa na Mkuu wa Usalama wa Taifa hajatoka Zanzibar hata mara moja. Sikumbuki sina uhakika wa *IGP*, nadhani na nasikia kwamba aliwahi kutoka *IGP* mara moja, lakini sina uhakika, kama ni mara moja, basi katika miaka 50 jamani, inasikitisha sana.

Mhe. Spika, sasa ikiwa Muungano wenyewe ndio huu na mimi siku zote huwa ninasema, mimi si muumini wa mambo ya Muungano, tena katika dhana hii, kwamba sisi tunadhalilishwa na huku uwezo tunao, nani aliyekuwa hajui hapa kama huyu Kamanda wetu kutoka Matemwe ana uwezo wa *IGP* mbona hapati? Bwana Abdi Mosi ana uwezo. U-*CDF* ninaamini muna watu wana uweza humu humu kwenye Baraza, tusiende kwenye vikosi humu humu kwenye Baraza, huko kwenye vikosi ndio haisemekani kwamba vijana wetu wana uwezo huo, lakini leo hivi sasa inasikitisha sana kwamba hatupati hizo nafasi.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba sijui ni mabalozi ngapi tulizonazo katika nchi za nje. Ninadhani hivi sasa Wazanzibari walio-*hold diplomatic post* za kibalozi, ukimtoa huyu Mheshimiwa anayemaliza muda wake, huyu aliyekuwa Waziri wa Elimu zamani hapa ambaye anamaliza muda wake Mhe. Mwinyi Mzale, ninadhani hawazidi watatu, ninafikiri na Al-Ahmed kishastaafu pale Oman, hawazidi watatu na wakati wana-dipolomasia tumo, humu ndani wanadiplomasia tuliobobea katika mambo haya ya *International relations* na *Conflict resolution* tumo. Kwa nini hawatupi, akina Mhe. Makame Mshimba pale ana uwezo mkubwa wa kuwa balozi, tena katika nchi mbali mbali, sio hizi za ki-Afrika tu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nadhani kwa Muungano wa *simple* hii hauna maana, unatudhalilisha.

Mhe. Spika, twende kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, sasa ambalo nalo ni jambo la Muugano hili, ni tatizo vipaumbele vinavyotumika katika Bodi ya Mikopo ya Elimu Juu vinaangalia zaidi vipaumbele vya Tanganyika. Sasa unakutia kipaumbele cha Tanganyika, ni mambo ya *Computer science*, ni mambo ya *Human relation* na mambo kama hayo. Huku watoto wetu wanaotaka kufanya *Economic* Zanzibar hawapati, wanaotaka kufanya *Political science* hawapati, wanataka kufanya *Education* hawapati, hili ni tatizo.

Mhe. Spika, sasa na serikali imekaa kimya. Sasa namuomba Mhe. Balozi Seif Ali Iddi katika hili tunanyimwa, katika hili watoto wetu wanadhalilika, wanategemea mkopo huu wa Zanzibar sana kuliko ule wa Bara. Kama tungepewa 4.5 ya kwetu sisi kwenye ile Bodi ya Mkopo, tukaambiwa hii yenu Zanzibar, tungeweza kuvitayarisha vipaumbele, lakini sasa inasikitisha kwamba kwa mujibu wa vipaumbele vya watu wa Bara, watoto hawa hawawezi kuweza kuvi-*focus* vile vipaumbele vyao. Matokeo yao wengi wanaachwa na ni wachache wanaopata ile mikopo.

Mhe. Spika, sasa katika hili mimi ninapendekeza tu hapa Barazani kwamba na wale na wakubwa wetu munaokwenda kule musije mukapata kigugumizi hata kidogo, maana sisi ndio hatuwezi kusema kule huku *back beachers* hatushiriki kule kwenye vikao vya Jamhuri, tungeweza kusema sana. Sasa nyinyi munaokwenda musiogope kusema watupe 4.5 yetu ili watoto wetu tupate kuwasomesha huku.

Mhe. Spika, hofu ni tatizo, inaonekana hiyo *front bench*, Baraza letu la Mawaziri lina hofu, linawahofu Watanganyika, musiwe na hofu, sisi tumewakomboa mwaka 1964 katika utumwa ule wa bwana na mtwana, sasa msijiingize katika utumwa wa hofu, huu utumwa wa hofu ni mbaya kwa mujibu wa bwana Lenni.
Mhe. Spika, naomba uniruhusu ninukuu;

Bwana Lenni anasema katika *freedom and unity*, anasema;

"*The most worst slavery in the world is the slavery of fear*" katika utumwa mbaya sana katika uso wa ulimwengu ni utumwa wa hofu. Wanasema bora ule wa bwana na mtwana, lakini ukiwa na hofu ni utumwa mbaya sana. Sasa katika kutetea maslahi ya Zanzibar, nyinyi *front bench* huko mbele musiwe na hofu, laiti mngekuwa mnaruhusiwa kwamba mpeleke Wazanzibari tu, hata huku *backbencher* aaah! ningewaambia siku moja mnichukuwe, lakini maskini

Mhe. Spika: Mjumbe, una dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, lakini maskini hamna uwezo wa kunichukua. Sasa niende moja kwa moja kwa kumalizia na hili suala la Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.

Mhe. Spika, katika idara hii mwaka 2013/2014 tuliidhinisha shilingi bilioni 2,189,103,000, lakini zilizotolewa ni bilioni 2,480,329,652. Sisi tuliidhinisha bilioni 2.1, wao wakatumia bilioni 2.4. Namuuliza Balozi sasa atuambie, kwa sababu fedha tulizoziidhinisha humu, kuna karibu shilingi milioni 200.Nani kawaruhusu mzitowe hizi ajira na mzipeleke kwenye sherehe? Nani kawaidhinisha? Sisi hatukuwaidhinisha. Mtupe maelezo hizi milioni 200, nani kawaidhinisha na kama mmezitoa tu, basi mzirudishe Hazina sasa hivi. Hilo moja.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Mohammedraza amesema hapa, kwamba kumbe pamoja na fedha hizi mlizozichukua za ziada, mmeshindwa kufanikisha hizi sherehe mpaka ikabidi mambo ya soka haya ambayo ndiyo yanawavutia zaidi Watanzania aingie Mhe. Raza na hadi leo hii, kwanza nakupongeza Mhe. Raza kwa kuweza kufanikisha hizi sherehe kwa upande wa soka, halafu inanisikitisha sana kuona kwamba Mhe. Raza hadi leo hii anadai dola 45,629. Kwa kweli alipodai alipelekwa mpaka kwenye Tume ya Rushwa akahojiwa na yeye ndiye anayedai hiyo hela, inasikitisha.

Mhe. Spika, mimi naamini tungelikuwa na watu watano wa dola tu kama Mohammedraza Hassanali hapa mdogo wangu, basi naamini mara hii tungeshiriki katika kombe la dunia sie, kwa jinsi anavyopenda michezo huyu kijana. Vile vile, napata tatizo hata yule kocha wa simba yule wa kizungu waliowekwa kule kwenye hoteli ile, mpaka kenda Mhe. Raza kulipa pamoja na mapesa yote mliochukua haya, *shame* inasikitisha sana aibu kabisa, aibu, aibu. Mimi naiomba sana serikali iwe makini sana katika kufanya mambo, sio iseme maneno tu, ifanye matendo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Zanzibar ina kisiwa cha Unguja na kisiwa cha Pemba. Niipongeze serikali kwa kuuendeleza ule Uwanja wa Ndege pale, lakini inasikitisha sana kwamba kila siku uwanja wa ndege wa Pemba tushafika hapa, tushafanya hasara ya *Feasibility Study*, tangu tuingie humu maneno ni hayo hadi leo hii. Leo pale Waziri wa Fedha anatwambia yale yale ya mwaka juzi.

Mhe. Spika, mimi nadhani sasa ikiwa imeshindikina kuutengeneza ule uwanja, basi katuwekeeni mishumaa, ili ndege zituwe usiku, Rais akitaka kuja kuangalia raia wake kule wakati wa usiku apate kutua pale Pemba. Sasa nyie mnatutenga na Rais wetu katika nyakati za usiku kwa namna gani jamani, tuwekeeni vibatari ili Rais wetu mpendwa akitaka kuja kutuangaalia usiku aweze kuteremka pale Pemba na yeye. Mnatubagua sana, kwa kweli serikali inatubagua sana kabisa kabisa Mheshimiwa, kama bado dakika moja, nimalizie kwa walemavu sasa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika: Muda wako umemalizika Mhe. Mjumbe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Wanahitaji kutunzwa, kuenziwa na kudhaminiwa katika nchi hii. Miundombinu Mheshimiwa ya nchi hii sio rafiki kwa watu wenye ulemavu. Mimi naomba tu sasa, kwa sababu juzi tulipewa takwimu hapa kwamba watu wenye ulemavu wameshasoma sana, wana mpaka *Degree* za Uzamivu, basi waingie katika Baraza hili kwa nafasi zao maalum na hata wawekewe nafasi ya uwaziri maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu iwepo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Saleh Nassor, lakini mwache Mhe. Waziri wa Fedha na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano watengeneze uwanja wenye taa nzuri na sio mishumaa bwana (*Makofi*)

Naomba nimkaribishe Mhe. Ali Abdalla Ali na baadae Mhe. Viwe Khamis Abdalla.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema na kuweza kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2014 - 2015.

Mhe. Spika, pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, tatu nimpongoze Mhe. Balozi kwa kuweza kuwasilisha hotuba yake vizuri sana na imeaandikwa vizuri. Nimpongeze na waziri wake Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea hotuba nzuri.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia sehemu 4 tu katika hotuba hii; Sehemu ya kwanza ipo ukurasa wa 19, kifungu cha 35 kuhusu migogoro ya ardhi. Kwanza naipongeza serikali kwa jitihada kubwa inayochukua katika kurekebisha migogoro hii na kututaka sisi viongozi kuanzia shehia, majimbo tusishiriki katika migogoro kama hii.

Mhe. Spika, naomba nimwambia Mhe. Waziri, kwamba yako mengine huwa hatutaki tunalazimishwa kushiriki. Sasa wameshakuja wananchi wako na tatizo, watakuja kutaka msaada, itabidi lazima uingie ukitaka usitake. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri tunapoingia kwenye migogoro hii, hatuingii kwa kutaka, isipokuwa tunatumwa na wananchi wetu na mimi katika migogoro mingi ya jimbo langu, nitazungumzia miwili tu na yote ipo Selem Mfenesini.

Mhe. Spika, nashukuru serikali imechukua jitihada kubwa, lakini bado matatizo hayajamalizika, labda tuseme yamefikia nusu. Kwanza Selem pana Historia kubwa, miaka ya nyuma kwenye miaka ya 1980 huko, katika kutafuta vitu vya kuongeza uchumi wa nchi yetu, ikapendekezwa tupande minazi ya mbegu fupi na eneo moja lililopendekezwa ni Selem, wananchi walikubali mashamba wakayaachia serikali na ukafanywa mradi huo, lakini kwa bahati mbaya hawakufanikiwa. Sasa baada ya kuwa hawakufanikiwa ikawa wananchi sio wote waliorudishwa pale. Maeneo yale kwa bahati wakapewa viongozi, sio mbaya.

Mhe. Spika, lakini kuna maeneo yalibakia na tukaomba serikali ije kutupimia ili wananchi wale ambao waliondoshwa kwenye maeneo yale waweze kupata na wao rizki japo kidogo, serikali ilifanya hivyo ilipima, lakini hadi leo ni muda mrefu wananchi hawajakabidhiwa. Naiomba sana serikali kama kuna tatizo viongozi ndio sisi, tupo tuzungumze, lakini wananchi bado wana kilio kikubwa cha eneo lile hawajakabidhiwa na lilipimwa muda mrefu, lakini hawajapewa. Kwa hivyo, maeneo yamekaa tu na wananchi wanapata shida ya kuyatumia.

Mhe. Spika, kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri kama jawabu nitapewa hapa hapa au utanitafutia siku ukanipe na wananchi wangu kule hakuna tatizo. Katika upande huo huo wa Mfenesini tulikuwa na tatizo sehemu ya Mbuzini, Nguruweni. Nashukuru kumepimwa na wananchi wameshapewa hati na sasa wanalima.

Mhe. Spika, suala la pili lilioko Mfenesini ni mashine ya maji, pale wananchi wamekaa tangu mwaka 1964, baada ya Mapinduzi hadi hii leo na eneo lile wananchi walikuwa hawajui kwamba ni la Wakfu, lakini mwaka jana wamezuka wenye Wakfu ule na wenyewe wameutaka na wamekuja na watu wa Kamisheni. Chakusikitisha ni kwamba Kamisheni imewataka wale watu waondoke kwa siku 100 na wawe wameshahama, yaani miezi mitatu na siku kumi. Sasa tumezungumza na Kamisheni, kuhamisha haiwezekani kwa sababu watu wana mali zoa, kaka watafanyiwa thamani hakuna tatizo.

Mhe. Spika, lakini rai ya pili ilikuja kwamba wananchi waendelee kukaa, lakini pafanywe hesabu waweze kufidia muda waliokaa. Pia, hilo ni gumu, wananchi wanyonge na kosa ilikuwa sio lao. Sasa na hili vile vile liko Wakfu, lakini *speed* yake ni ndogo. Wananchi sasa hivi wanaugua maradhi ya hofu, wangeugua homa, wangekwenda Hospitali wanapata dawa ya homa dozi unapon, au kifua unapona, lakini hofu haina maradhi, mpaka linalokutia hofu liondoke, sasa hatujajua litaondoka lini na wananchi bado maradhi hayo wanayo. Naishauri serikali kwa kupitia kwa Balozi kwamba na hili litizamwe, ili wananchi waishi kwa raha katika eneo ambalo wameshakaa kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, la tatu katika sehemu ya ardhi ni kwamba palikuwa na zoezi la kuhakikiwa mashamba ya serikali pamoja na heka tatu zilizotolewa na serikali. Je, zinakwenda vizuri na zinatumika inavyotakiwa? Zoezi hili naomba niulize wizara imefikia hatua gani na mafanikio gani yamepatikana katika kuhakikiwa mashamba, pamoja na heka ambazo walipewa wananchi kwa kutumia?

Mhe. Spika, suala la nne, nije ukurasa wa 21 kifungu cha 39 juu ya suala zima la madawa ya kulevya. Naishukuru serikali inachukua jitihada kubwa, lakini madawa ya kulevya ni kilimo cha dunia nzima na nchi nyingi sasa hivi zinazoendelea, ndio zinazokabiliwa na masuala haya, kwa dhana kwamba kijana kama hana ajira anaona akitumia madawa ya kulevya anapunguza matatizo, lakini kumbe kwa nchi ni tatizo kubwa zaidi, kwa sababu vijana ndio

wanaoleta maendeleo katika nchi na ndio nguvu kazi. Sasa kama watatumia madawa ya kulevya itakuwa nchi haina maendeleo.

Mhe. Spika, tunashukuru jitihada zimechukuliwa na baadhi ya *NGOs*, zinatafuta na kukusanya vijana katika nyumba za *Sober House*, wanapata matibabu, lakini hatari iliopo akimaliza matibabu yale, pengine mieizi 6 ama mwaka anarudi tena kijiweni anaanza tena pale pale. Kwa hivyo, nashauri mambo mawili kwa serikali, kwamba wenzetu wameonesha nia ya kuwasaidia vijana hawa, serikali iunge mkono.

Mhe. Spika, kwanza tusikodi nyumba tu za mitaani, inakuwa kidogo haileti picha nzuri, patafutwe maeneo pajengwe nyumba rasmi, vijana wapelekwe kule na wahudumiwe, wakishapona wapewe na mitaji ya kuweza kujiendeleza, vyenginevyo itakuwa tunaweka konokono mmoja, tukenda kumchukua mwengine yule wa kwanza kaondoka. Sasa naomba serikali hili suala jitihada iwe kubwa.

Mhe. Spika, lakini la pili ambalo linaweza kusaidia suala hili, tungejaribu kuzuwia mianya na kisiwa chetu hiki kina madiko mengi ya kienyeji. Siku hizi kuna askari jamii, tungeweza kuwapanga askari jamii kwenye madiko ya kienyeji ambayo nina wasi wasi, ndio sehemu kubwa inayopitishiwa dawa hizi, ikaweza kuisaidia serikali kuzuwia uingiaji wa dawa. Kama zitakuwa haziingii, basi na walaji watakuwa hawapo, lakini tukiziwachia kuingia walaji haweshi, kwa sababu kitu chochote cha kutumika ni lazima kitumiwe.

Mhe. Spika, kwa hvyo, nashauri mambo hayo mawili *Sober House,* serikali itie mkono wake na vijana wakishapona, basi wapewe mitaji ili wasirudi vijiweni, lakini na hizi njia za kupitishia hizi dawa zitafutiwe utaratibu wa kuweza kuzuiwa ili dawa zisiingie katika nchi yetu.

Mhe. Spika, suala la tatu, nije kwenye ukurasa, hii haina ukurasa, sitaki kuinukuu ukurasa, lakini ni kuhusu mfuko wetu wa maendeleo ya jimbo, tunashukuru kwamba vipindi vyote tangu tulipoanza tunapata hizi fedha na sasa hivi tumeshafikia hatua kubwa. Niipongeze serikali kwamba katika kipindi cha mwaka huu kuna ongezeko kidogo, kutoka milioni 15 kwenda milioni 20, lakini ningeomba kwa kuwa hivi sasa vitu vya ujenzi na vitu vya aina yoyote vinazidi katika gharama zake, basi tungeomba kila serikali ikipata uwezo iwe inatuongezea, kwa sababu mara ya mwanzo walipotoa mfuko huu ili kuwa mfuko wa saruji shilingi 8,000, sasa saruji mfuko ni shilingi 13,500, mfuko ule ule wa shilingi 8,000, ukija kwenye nondo za milimita 10 zilikuwa shilingi 8,000, sasa hivi shilingi 14,000, milimita 12 shilingi 18,000. Sasa utakuta kila mwaka vitu vinazidi bei, lakini fedha ziko pale pale.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ningeshauri kwamba serikali ikaweza kila tunapokwenda mbele, basi na fedha wakatuongezea, kwa sababu kubwa inayofanywa miradi ya huku ni kujengwa mashule, leo ukijenga banda moja la *Primary,* mwakani kama hukujenga, basi vijana wale Wahemishiwe skuli nyengine. Sasa sisi miaka yote tunajenga na wewe nadhani uko kwenye jimbo unaelewa hilo. Kwa hivyo, tunaomba suala hilo tusaidiwe fedha ili mabanda kila mwaka tujenge, ili kila aliyekuwa keshafikia umri wa kuweza kusoma, asome na aweze kujiendeleza.

Mhe. Spika, sehemu yangu ya nne nije ukurasa wa 46, kifungu cha 75 kuhusu Idara ya Kukabiliana na Maafa. Niipongeze serikali kwa kuunda idara hii, kwa sababu hivi sasa wenyewe wataalamu watu wa dini wanasema tuko kwenye karne za mwisho mwisho. Kwa hivyo, maafa yanakuwa mengi na halafu maafa yakija hayakuletei taarifa, yanazuka kwa upepo au kwa mvua na hii kwa kuwa tuko duniani na sisi tutakuwa hatuwezi kuyaepuka. Kwa hivyo, naiomba serikali iongeze mfuko katika suala hili.

Mhe. Spika, pia, nimeziona jitihada zake kwamba tayari zimeanza kutoa mafunzo katika maeneo mbali mbali na nimebahatika katika jimbo langu, shehia mbili zimepata mafunzo. Shehia ya Kama na Shehia ya Mwakaje, bado shehia sita. Sasa naomba na hili pia lingezingatiwa ili wananchi wakapata kujua vya kujikinga kama yanapotokezea haya maafa.

Mhe. Spika, lakini maafa yako ya aina nyingi, safari hii mvua zimekuwa kubwa sana hapa kwetu na bado zinaendelea. Watu wengi waliolima mavuno hawakupata, hasa mpunga wa mabondeni mwingi umeshazama. Mpunga kama utazidiwa na maji bila ya kutokeza nchi juu, basi unaoza. Kwa hivyo, wananchi wengi waliolima mpunga mabondeni sasa hivi hawategemei kuvuna. Isipokuwa wale ambao wanalima sehemu za juu ndio wanaweza kupata mpunga. Sasa tuwaangalie na wale walioathirika kwamba hawana chakula kwa kipindi hiki, basi serikali ifanye utaratibu wa kuweza kuwasaidia, kwa sababu juhudi za kulima wamefanya, lakini Mwenyezi Mungu hakuwajaalia kupata chochote.

Mhe. Spika, kwa hivyo, nilikuwa nawaomba watu wa maafa wangepita katika maeneo mbali mbali ili wakaliangalia hilo, sio mpunga tu, lakini hata mihogo, muhogo ukilala ndani ya maji siku moja tu, basi siku ya pili umesharembuka hauliki tena, kiazi hali kadhalika. Sasa tungeshauri wakapita katika majimbo mbali mbali, hasa yale ambayo yako vijijini wakaangalia athari gani wakulima wetu wamepata ili serikali ikaweza kuwasaidia, wakapata nguvu mpya za kuweza kulima katika kipindi kijacho. Nadhani serikali imesikia na naomba hilo lifanywe kwa jitihada kubwa, kwa sababu bado mvua zinaendelea kunyesha.

Mhe. Spika, mchango wangu wa mwisho nakuja katika ukurasa wa 63 ambao unahusika na Baraza letu la Wawakilishi. Kwanza niipongeze serikali na kuishukuru kwamba katika bajeti iliyopita fedha tumepata asilimia kubwa kidogo na mambo mengi tumeweza kuyatekeleza katika Baraza letu, lakini yako mambo mawili haya naona bado utekelezaji wake haujaanza na umo katika maandiko tu na mwaka huu sikusikia vizuri. Sasa kama yapo nitaelezwa na malengo gani yamewekwa na serikali?

Mhe. Spika, jambo la kwanza pamoja na jengo letu tulilojengewa, lakini ilikuwa kujengwe na *Hostel* ili wale Wajumbe wenzetu wanaotoka Pemba, wanaotoka Kaskazini, wanaotoka Kusini na sisi tunaotoka Magharibi tuweze kukaa kwa muda wote wa vikao. Unapata kutulia, unasoma masomo yako yaliomo ndani ya bajeti, pamoja na mambo mengine ya miswada unakuwa umetulia, zile hodi hodi zinapungua, lakini kama tunaishi nyumbani, halafu tunakuja Barazani, unakuwa ule muda wa kusoma huna na muda wa kupumzika huna. Sasa naona hili sikuliona kama lipo nielezwe kuwa serikali ina mpango gani wa kujengwa *Hostel* ili na sisi tupate kupumzika hapa tufanye kazi zetu kama tulivyopangiwa.

Mhe. Spika, lakini suala la pili, Ofisi za ajimbo ambazo tulisema serikali ijenge, wenzetu wa Bunge tayari wamejengewa. Hii inasaidia kitu kimoja, kwa sababu kule kwenye jimbo ukichaguliwa mwana CCM au mwana CUF kuwa Mbunge au Mwakilishi, basi unahudumia watu wote. Sasa wengine huona muhali mtu CUF akija kwangu mimi wa CCM kuja kusema lolote lile la kimaendeleo au lake yeye mwenyewe binafsi, akionekana kaja nyumbani kwangu watu watasema doo! keshamnunua yule, sasa utakuta maendeleo vijijini yanapungua kwa kutiliana shaka. Huyu akienda kwa CUF ataambiwa kamnunua na huyu akija kwa CCM ataambiwa kamnunua. Sasa tukijengewa ofisi itakuwa mtu yeyote anapata uhuru wa kuja, ili kupanga maendeleo ya majimbo na tuweze kwenda mbele zaidi.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo mfupi, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, tunaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Viwe Khamis Abdalla.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili na watendaji wake, kwa jinsi anavyosimamia ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Afisa Mdhamini kutoka Pemba. Pia, nichukuwe nafasi hii niipongeze Kamati ya Sherehe na Mapambo, kwa jinsi walivyojitahidi katika kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.*(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na yote hayo, lakini ipo haja ya kurudi kama zamani ilipokuwa inasomeshwa Historia ya Zanzibar kwenye maskuli.
Mhe. Spika, nasema hivyo kwa maana yangu, sasa hivi vijana wengi wa Zanzibar hawaijui Historia ya Zanzibar na hivyo hupelekea kuyabeza Mapinduzi ya Zanzibar kutokana kuwa hawaijui Historia hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nichangie kwenye madawa ya kulevya pamoja na jitihada za serikali kupambana katika kuyatokomeza madawa ya kulevya, lakini bado ipo haja ya kupatiwa ufumbuzi madawa haya ya kulevya, nilipokuwa kwenye Kamati ya Habari, Mifugo na Uwezeshaji nilibahatika kutembelea vituo vya *Sober house,* tulipofika pale tulikutana na vijana wa *Sober house* ambao walitueleza walitupa malalamiko yao, baada ya malalamiko yao, wao walisema wao wapo pale wanapewa elimu na taaluma.

Mhe. Spika, lakini bado baada ya kumaliza pale ile miezi ambayo wanatakiwa waishi kwenye *Sober house* baadae wanarudi mitaani. Mitaani kule kama hawana ajira na hawana chochote cha kujishughulisha wanarejea kwenye madawa yao ya kulevya, niombe serikali waweke vituo maalum vya kuwasomesha wale vijana elimu ya ujasiriamali ili watakaporejea mitaani waweze kujiajiri wenyewe, wasije wakarejea kule walipokuwepo mwanzo.

Mhe. Spika, katika sherehe za kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, Mheshimiwa Makamu wa Pili katika hotuba yake alituelezea kama kuna mnara ule pale unajengwa na sasa hivi ni miezi sita tokea kujengwa mnara ule pale na mpaka leo hii mnara ule haujamaliza, sasa namuomba Mhe, Makamo au Waziri anayehusika atakapokuja, anipatie hesabu ya ule mnara mpaka kufikia pale umetumia kiasi gani ya fedha za wananchi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye mradi wa *TASAF*, mradi wa *TASAF* ni kweli upo na unasaidia wananchi walio wanyonge na waliokuwa sio wanyonge, miradi hii baada ya kumaliza fedha ambazo kuwa wamesaidiwa kwenye mradi wa *TASAF*, baadae huwa wanaachiwa wenyewe, lakini kuna miradi ambayo inatokana na *TASAF* inakwenda kwenye uvuvi waliopatiwa maboti ya uvuvi, miradi ya mifugo, mabanda ya skuli, lakini baadae huwa serikali hawashughuliki nao tena miradi ile wanaiachia na matokeo yake huwa inakufa ile miradi. Niiombe serikali kwa kupitia mawaziri husika Waziri wa Mifugo, Waziri wa Uvuvi pamoja na Waziri wa Elimu, mara tu baada ya kumaliza mradi huu kupitia kwenye *TASAF* wao wawe wasimamizi wakuu wa kuilea miradi hii.

Mhe. Spika, pamoja na michango yangu yote hiyo, naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa niaba ya vijana wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Wazanzibar wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsane sana kuna dakika kama kumi na tano nadhani Mjumbe mmoja atusaidie na atumie muda huo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya mwisho mwisho kuzungumza machache kuhusu hutuba hii ya bajeti ya mwaka 2014/15 ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwanza baada ya shukurani hizo, naomba nianze moja kwa moja kuhusu idara ya kukabiliana na maafa, idara hii ni muhimu hasa kutokana na kuwa Zanzibar tumefikwa na maafa mara kwa mara, kuna maafa yanatokea katika bahari, kuna maafa yanatokea kwa mabadiliko ya hali ya hewa, mvua na kadhalika na maafa ya aina nyengine, kuwepo kwa idara hii mimi naunga mkono sana na naiombea Mwenyezi Mungu idara hii ifanye kazi stahiki ili japokuwa hatuombi panapotokea maafa ya aina yoyote yasiwe na dhara kama nyuma yalipotokea.

Mhe. Spika, idara hii kwa mwaka wa fedha 2013/14 ilipitishwa na baraza lako tukufu jumla ya shilingi 262,328,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufika mwezi wa Mei, jumla ya shilingi 112,283,670/= ikiwa ni sawa na asilimia 43.

Mhe. Spika, vile vile, kwa miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa na jumla ya Shs. 340,000,000/= kati ya hizo milioni 70 ilikuwa ni mchango wa serikali na milioni 270 ilikuwa ni mchango wa washirika wa maendeleo, idara hii mpaka kufikia mwezi wa Machi, 2013/14 wa fedha serikali ilitoa Shs. 10,000,000/= tu kati ya milioni 70, ikiwa ni sawa na asilimia 14 kwa idara kama hii yenye umuhimu wake, mimi nasikitika sana kwa hili na ningeliomba Wizara ya Fedha itueleze ni sababu gani Wizara muhimu kama hii ikapewa shilingi hizo milioni kumi ikawa na asilimia 14 tu.

Mhe. Spika, kwa upande wa washirika wa maendeleo kati ya shilingi milioni 270 zilizopatikana ni shs. 175,176,000/= ikiwa ni sawa na asilimia 65, sasa suala langu ilikuwa katika mwaka huu wa fedha unaofuatia wa 2014/15, idara hii imeombwa kupitishiwa jula ya shilingi 40 milioni kutoka mfuko wa serikali kwa shughuli za maendeleo, wakati kipindi hiki kinachomalizika ilikuwa ni milioni sabini, wakati siku zinakwenda mbele na tumeona matokezeo ya maafa yaliyotokezea na fedha nyingi inahitajika, ningeliomba kujua kwa nini kipindi hiki kilichopita iliomba milioni 70 kutoka kwenye serikali safari hii imeomba milioni 40 kulikuwa na nini mpaka ikapungua hivyo?

Mhe. Spika, vile vile, kwa nini kipindi kilichopita ilitarajiwa kupewa milioni 270 na washirika wa maendeleo, lakini safari hii wameomba Shs. 1,282,880,000/=, sasa kupunguza kwenye serikali na kuongeza kwenye washirika wa maendeleo kuna sababu gani ya kufanya hivyo? Hilo naomba nielezwe tena kwa makini kabisa.

Mhe. Spika, nitoe pongezi zangu kwa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, yaani *UNDP* kwa misaada yao muhimu kwa idara hii ikiwa ni pamoja na gari moja, redio za mawasiliano kumi, pikipiki 3 na kompyuta, yaani *laptop* 4, pamoja na kazi nzuri idara hii inayofanya kazi kutekeleza shughuli zake ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii, kurusha vipindi katika redio na kutoa taaluma kwa wafanyakazi wake, lakini idara hii inakabiliwa na kazi kubwa na nzito.

Mhe. Spika, sikuona katika maelezo yake imejipanga vipi, yaani kwa vifaa stahiki ili kuweza kupambana kama itatokezea na maafa yoyote kwa wakati ikiwa maafa hayo Mwenyezi Mungu atunusuru itatokea katika anga, ikiwa ni nchi kavu au katika bahari. Ule mpango wa kutokea ajali tukangoja misaada, helkopta kutoka wapi na mengieneyo imeshapitwa na wakati, uzuri panapotokea maafa, panatakiwa uokozi wa haraka ili maisha yaweze kuokolewa. Kwa hivyo, mmejipanga vipi kuwa na dhana hizo za kisasa na wakati umeahidi kufanya hivyo baada ya kutokewa na shughuli kama hizo katika siku zilizopita.

Mhe. Spika, jengine ninalopenda kuzungumza ni kuhusu Tume ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi ni Tume muhimu sana kwa sababu ni tume ambayo kama ikifanya kazi kwa uadilifu, amani itapatikana na kama haikufanya kazi kwa uadilifu, maisha yote tunakwenda katika matatizo.

Mhe. Spika, ukiangalia ukurasa wa 80 kwa Katiba yetu ya Zanzibar, Tume hii ya Uchaguzi imepangiwa majukumu makubwa, mimi hapa sitazungumza yote, lakini nitazungumza kifungu 119, kifungu kidogo 12,13 na 14. Kifungu kidogo cha 12 kinasema kuwa katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yoyote au idara yoyote ya serikali au maoni ya chama cha siasa.

Mhe. Spika, kifungu 119, kifungu kidogo 13 kinasema kwa ruhusa yako;

"Hakuna Mahakama yoyote itakayokuwa na Mamlaka ya kupunguza jambo lolote linalotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza Madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii".

Mhe. Spika, kifungu kidogo cha 14 na kifungu hicho hicho 119 kinaeleza kuwa katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, tunaingia mwaka 2015 na ni mwaka wa uchaguzi na zaidi ya hayo, Tume hii vile vile ina mamlaka ya ugawaji wa majimbo kwa kuona hali halisi inayofaa, nasema hivyo kwa sababu ndivyo ilivyoelezwa katika Katiba, sasa mimi linalonisikitisha sisemi kuwa ni Tume, lakini nasema kuna utashi, sijui unatoka wapi? Mwenyezi Mungu alivyojalia nchi hii tokea mwanzo na mpaka leo imeendelea kuwa na viongozi makini sana, kulijulikana kuna visiwa vikubwa viwili; ikiwa ni Unguja na Pemba na wameweka mgawanyo wa mambo kwa mfano mikoa iliyopo Pemba ni miwili na majimbo na mikoa iliyopo Unguja ni mitatu, hiyo ni *rate* ya mbili kwa tatu.

Mhe. Spika, wilaya zilizoko Pemba ni nne, wilaya ziliopo Unguja ni sita, hiyo ni *rate* ile ile ya mbili kwa tatu, majimbo yaliyokuwepo Pemba ni 21 na majimbo yaliyokuwepo Unguja ni 29, ni ile ile *rate* ya mbili kwa tatu, hivi ndio mgawanyiko walivyouweka na hivi tulikuwa tunakwenda vizuri sana.

Mhe. Spika, kwa sababu nchi hii kwa mipango yake mibovu na nasema hivyo kwa sababu ndio hali ilivyo, hakuna udhibiti wa kuingia watu katika visiwa hivi na kwa mazingira ya kimaendeleo, bila ya kupinga wengi wanakimbilia kuja Unguja, si watu kutoka Pemba au nje ya Zanzibar, wote wanakimbilia kuja Unguja, kimaumbile watu wa Unguja wamekuwa wengi na Pemba wamekuwa kidogo, kule wanakimbia kutokana na maendeleo duni, kwa sababu ya kuwa sijui kwa kuwa kumetupwa au ndio ilivyo tokea zamani. Sasa kwa wageni wanaoingia na idadi ya watu ikaongezeka, ikawa sio Wazanzibari wenyewe, watu ambao sio Wazanzibari, ikasababisha kuwa na ugawaji wa majimbo upya kwa idadi ya watu hivi, Zanzibar hatuitendei haki.

Mhe. Spika, naomba kwa hili tuwe makini, sasa Zanzibar ijue wageni ni wangapi, Wazanzibari ni wangapi, wenye haki ya kupiga kura na haki ya wanayopata Wazanzibari na shehiya itumike kwa misingi hiyo, ni misingi ya kuingiliwa na watu kutoka nje, halafu ikasababisha kutumia nguvu za kisiasa, tukaidhoofisha Pemba katika hadhi yake ya kupunguza majimbo na wakati ule ule kuongeza Unguja, hii haitupeleki popote.

Mhe. Spika, nchi zote za watu duniani inapofika wakati wa kura, wanaohusika tu ndio wanaopiga kura, wachilia mbali kuwa kuna watu chungunzima, kuna majimbo yana watu mpaka 60 elfu, hivi sasa ikija jimbo moja lina watu saba, sijui yatakuwa mangapi? Hii itakuwa tunaweka vurugu kwa sababu ya wageni, sio kwa sababu ya sisi wenyewe hii nasema tena kwanza huu uwazi uliowekwa kwa kila anayetaka aje bila ya masharti maalum utatuharibia katika utawala huko tunakokwenda.

Mhe. Spika, jengine ninaloomba kuzungumza ni kuwa kupiga kura ni haki ya kila Mzanzibar na Mzanzibari hatopiga kura kama hana kitambulisho cha kupiga kura, watu wanaongezeka sana, lakini bado kuna watu wanaostahiki kupiga kura, ni wachache sana wengine hawapewi haki zao.

Mhe. Spika, kwa kuweka mazingira mazuri, nakuomba yale yote yaliyopita kwa makosa yamepita na sasa bado upo muda tuanze ukurasa mpya, tuone kuwa kila mwenye haki ya kupiga kura, amepiga kura, ule utashi wa kisiasa uondoke. Kwa hivyo, wale ambao hawapewi vitambulisho vya kupiga kura, eti tu kwa sababu Sheha hajatoa maelekezo. Kwa hivyo, naomba ifuatiliwe ili haki hii itendeke.

Mhe. Spika, jengine ambalo napenda kulizungumza ni kuwa kwa wale waliokuwa wamo kwenye Baraza hili, kwa miaka mingi wameona mambo yalivyokuwepo huko nyuma namna ulivyokuwa ukipata tabu na dhiki katika kuendesha baraza lako kwa sababu ya kutoelewana, tulikuwa na matatizo makubwa, mara chama cha upinzani hakiungi mkono, wara wanakwenda zao, almuradi mashaka tu, Mwenyezi Mungu kajaalia kumekuja Tume ya Maridhiano, naipongeza wakatoka viongozi wakuu wahusika katika nchi, akiwa ni Mwalimu Seif Sharif Hamadi, sasa hivi ni Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Abeid Amani Karume Rais wa awamu iliyopita walikaa. Rais wa awamu iliyopita walikaa.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa Mjumbe ndio ukae tena.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nakaa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunakusudia kumaliza mjadala leo jioni ili kesho asubuhi tuende kwenye majumuisho, sasa Wajumbe waliopo ambao wameomba kuchangia na waliobaki wanafika kiasi ya kumi na nane na tuna uwezo wa kumudu kuwasikiliza Wajumbe wapatao kumi na mbili, kama watatumia muda vizuri. Hivyo, bila ya shaka itakuwa kuna baadhi ya Wajumbe hawatapata nafasi ya kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe, nategemea kwamba Wajumbe watakaopata nafasi ya kuchangia kwa jioni ni pamoja na Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Mahmoud Moh'd Mussa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, nafikiria hao itakuwa ni idadi ya kutosha kama utakuwepo muda labda mmoja au wawili. Kwa hivyo, wale walioomba ambao sikuwataja, nadhani wangejitayarisha ila kuna Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri wa Habari Utamaduni na Utalii na Michezo atakuwa na maneno kidogo na yeye kuzungumza.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo, tukiachia wale ambao sikuwataja wajitayarishe kupeleka michango yao kwa maandishi, baada ya hayo, basi tuakhirishe shughuli zetu hizi hadi saa 11:00 jioni.

(Saa. 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea naomba nafasi ya kwanza jioni hii nimkaribishe Mhe. Fatma Mbarouk Said, baadae Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii, kwanza niipongeze hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais iliyosomwa kwa ufasaha na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Idd.

Mhe. Spika, na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kushuhudia sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu, Mapinduzi ambayo yalimkomboa mnyonge wa nchi hii nikiwemo na mimi...

Mhe. Spika, niseme kweli kama *styles* za Wajumbe humu ndani walioanza na nukuu mbali mbali na mimi nanukuu haya. "Tanzania ndipo petu hatuna pengine katu" kwa maana hiyo, basi tunatakiwa tuwe na umoja na mshikamano ili tuweze kusonga mbele kwa maendeleo ya nchi hii, si busara hata kidogo kubeza Mapinduzi haya, wala kuwabeza waasisi wetu.

Mhe. Spika, wengi humu tumefaidika, ama kwa hili, ama kwa lile, tulinde amani na utulivu wetu, tusiichezee amani na utulivu, tusome kwa wenzetu Somalia, Nigeria na kwengineko.

Mhe. Spika, naomba na hasa wanawake wenzangu tusikubali kuribuniwa kwa kuivuruga amani hii, kwani amani ikivurugika wanaoumia ni wanawake na watoto. Baba atakukimbia akuache wewe na watoto, ni lazima tuliangalie hilo.

Mhe. Spika, na mimi niseme ubaguzi si mzuri, hata Mwenyezi Mungu hatokuwa pamoja na sisi. Mwenyezi Mungu anasema nimekuumbeni makabila mbali mbali, rangi mbali mbali ni kwa sababu mjuane, mbora ni yule atakayemcha Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, hii ni dhambi na kama alivyosema Mwalim Nyerere kwamba ukianza ubaguzi, basi dhambi hiyo itaendelea, kwani ndani ya Tanzania, ukisema mimi ni Mzanzibari na yule ni Mtanganyika kumbe ndani ya Zanzibar kuna Wapemba na Waunguja na ndani ya Unguja kuna Wamakunduchi na Wadonge na pia, Pemba kuna Wamtambwe na Wakisiwa Panza, je, tunakwenda wapi? Hotuba za wazee hapa zinakwenda na wakati na zitafanya kazi mpaka mwisho wa dunia.

Mhe. Spika, Muungano ni muhimu sana na wajibu wetu kuulinda na kuutetea ili uweze kudumu milele na milele kwa faida ya vizazi vya sasa na vya baadae na mafanikio ni mengi kama ilivyoelezwa kwenye kitabu hiki kuanzia ukurasa namba 9 mpaka 12.

Mhe. Spika, hali ya uchumi inakuwa ni kweli na naamini na ukitakakujua kwamba uchumi umekuwa ni kuona ni namna gani watu wake wanavyoishi; magari na majumba mazuri, hiyo ni moja ya kukua kwa uchumi na mengi mengineyo ambayo yameelezwa kwenye bajeti hii kuanzia ukurasa namba 12 mpaka 13.

Mhe. Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi kwenye ukurasa 14, nimefarijika sana kupata habari ya kwamba kuna mfuko wa uwezeshaji kiuchumi wenye thamani ya 1.1 bilioni, basi ningeomba Makamu wa Pili, fedha hizi uhakikishe zimefika kwa walengwa wenye ulemavu na makundi maalum ya wanawake na vijana waliomaliza masomo katika maeneo yote ya Zanzibar ambako ugawaji utafanyika kupitia njia yoyote ambayo mtaona inafaa na sisi Wawakilishi tujuwe maeneo ambayo zimepelekwa fedha hizi.

Mhe. Spika, migogoro ya ardhi ni moja ya changamoto tulizokuwa nazo kwa muda mrefu na hii inasababishwa na kutokufuatwa sheria pamoja na kutokuwepo *regulation* kwa baadhi ya sheria na vile vile kutokuwa na elimu ya kutosha kwa wananchi, kwa kusema ardhi hii nimerithi kwa babu bila ya kujua ardhi ni mali ya serikali, ni lazima kama unahitaji ardhi hiyo upate kisheria upimiwe na uweze kuitumia.

Mhe. Spika, madawa ya kulevya ni tatizo ambalo linaathiri *new generation* yetu ambayo ni Taifa la baadae, ni lazima serikali iongeze juhudi kwa kutoingizwa madawa haya kama hakukuwa na juhudi ya ziada Taifa hili baadae halina nguvu kazi.

Mhe. Spika, wizara hii ina idara muhimu ikiwemo Idara Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu, idara hii ina changamoto ya kukopwa sana na hasa taasisi za serikali, ningeomba sana serikali deni si zuri inapelekea taasisi kama hizi kutojiendesha vizuri na ni moja ya vianzio vya mapato ya serikali hii.

Mhe. Spika, Idara ya Kukabilana na Maafa, maafa ni matatizo yanayojitokeza bila ya kutarajia na wakati mwengine husababisha vifo vingi kwa pamoja na hata mtu mmoja mmoja, lakini ni maafa. Niulize hii mivinje barabarani ina faida gani, imeshaua sana na kwa nini iwepo barabarani na mengine imeshakuwa mizee kama mimi?

Mhe. Spika, naomba sana tupande miti iliyokuwa haiendi juu sana itapendeza kuweka vivuli na kuleta haiba ya mji wetu huu.

Mhe. Spika, *characteristic* ya mivinje haiendi chini sana, isipokuwa inakwenda juu na mara ikipigwa na dhoruba inaanguka, kabla ya kwenda Dodoma nilikuwa Kwerekwe nikashuhudia mvinje, umeanguka ukapiga ki-*carry* kikawa nyanganyanga na watu waliomo ndani ya gari ile wakaumia. Niko Dodoma nikasikia umeanguka tena mvinje umeua askari, naomba sana na hasa nikizingatia njia ambayo mnapita viongozi wetu Mnazi Mmoja, kumejaa sana miti hiyo hatari na mizee kweli, kama ni lazima kuwepo mivinje, basi tuing'oe ile ya zamani na tupande mengine.

Mhe. Spika, hebu *imagine* jiti lile likianguka popote pale, si maafa hayo tutahadhari kabla ya athari.

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 99.5, asilimia 5 mpaka nitakapopata jibu la mivinje upande wa Barabarani, ni kwamba hakuna miti mengine ya wastani? Baada ya hayo, naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii nikaweza kuchangia katika hotuba hii. Nampongeza Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuwasilishia hotuba iliyo nzuri kwa wananchi wetu, Pia, nawapongeza na watendaji wote.

Mhe. Spika, namuunga mkono Mhe. Salmin kwa kutaka kuleta hoja yake binafsi, mimi namuomba ailete kwa sababu hapa ndio pahala pake. Sasa niende katika hotuba hii ya Makadirio.Naipongeza serikali kwa kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, sherehe hizo zilikuwa za aina yake katika nchi yetu ya Zanzibar wananchi wengi waliifurahia.

Mhe. Spika, pia, naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa kutimiza miaka 50 (nusu karne) tangu ilipoasisiwa tarehe 26 April, 1964. Pia, naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuzipatia ufumbuzi changamoto za Muungano.Pia, naiomba serikali ifanye haraka kuona changamoto zilizobakia zinafanyiwa kazi kupitia Kamati Maalum inayoongozwa na Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, niende Idara ya Maafa, naiomba serikali ianzishe mfuko wa maafa ili kukabiliana na changamoto mbali mbali hasa kwa vile nchi yetu ni visiwa, tusisubiri mpaka yakatufika ndio tukaanza kuchangisha.

Mhe. Spika, pia, niendelee mapambano dhidi ya madawa ya kulevya, mara nyingi wanaokamatwa ni wafanyabiashara wadogo wadogo wa mitaani. Kwa hivyo, naiomba serikali kuanzisha mikakati ya kupambana na matajirio wakubwa wanaoingiza biashara hiyo haramu katika maeneo yote ikiwemo bandarini, *airport* na bandari zote bubu.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Upigaji Chapa, naipongeza serikali kwa kusimamia idara hiyo vizuri na kukamilika jengo jipya la Kiwanda cha Uchapaji huko Maruhubi na tayari jengo hilo limeanza kutumika. Kwa hivyo, naiomba serikali iwapatie wafanyakazi wa idara hiyo ya Uchapaji mafunzo ili waendane na vifaa vilivyopo.

Mhe. Spika, nije katika mradi wa *TASAF*. Mradi wa *TASAF* ni muhimu ya kijamii kama maji, madarsa na hospitali, hii inatokana na msaada wa benki ya dunia kupitia Jamhuri ya Muungano.

Mhe. spika, baada ya kusema mchango wangu huo, naunga mkono hoja pamoja na wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi, mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia bajeti hii iliyoweka mezani kufuatia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunifikisha hapa nikiwa mzima wa Afya, mimi pamoja na wenzangu ili kuipangia bajeti hii ya serikali yetu ili kuhakikisha kwamba tunapanga bajeti nzuri kwa ajili ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwanza sina budi nichangie ukurasa namba 20, kifungu namba 38 kutokana na hali ya walemavu, kwa kweli serikali inasaidia sana walemavu, lakini utaona walemavu wengi wanaopata misaada ni kutoka hapa mjini, lakini walemavu ambao wako katika mikoa yetu ya mashamba, walemavu hao kwa kweli wamesahauliwa muda mrefu.

Mhe. Spika, walemavu wa mjini kwa kweli wanapata kila huduma hata baskeli, sehemu za kukaa na sehemu za chakula, lakini sisi wengine katika majimbo yetu tuna walemavu hali zao ni mbaya sana, sio walemavu wa kuanguka kwenye mnazi, wala si walemavu wa kuanguka kwenye gari, walemavu wamezaliwa nao ulemavu ukiwakuta wanasikitisha sana. Katika jimbo langu kuna mwananchi wangu amezaliwa hana miguu yuko upande wa Machui, mwananchi huyo kwa mara nyingi walipewa ahadi wazee wake atasaidiwa kutokana na majenzi ya nyumba ama kupatiwa pesa, lakini hadi leo mwananchi yule anakwenda skuli kwa njia ya kukokotwa na wenzake, ndio afike skuli na ukiona kukokotwa kwenyewe hana miguu kabisa, sio kama mguu mmoja anao mmoja hana, miguu hana kabisa mwananchi huyu anaitwa Mariyam katika sehemu ya Machui.

Mhe. Spika, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili pamoja na shughuli zake ahakikishe kwamba kwenda kumuona kijana wetu huyo ambaye hivi sasa ana umri wa miaka 11, lakini bado hajashughulikiwa anatembea hali ngumu, ingawa Mbunge na Mwakilishi wao tunajitahidi huduma nyingi, lakini huduma nyengine zinatushinda hasa za kumjengea na kumuwekea *account* benki.

Mhe. Spika, kwa kweli hilo ndio kilio chetu tuache kuwasaidia wa mjini tu na vijijini nako kuna wananchi wa nchi hii ambao wanaipendelea sana nchi yetu kuwa na amani kwa muda wote. Kwa hivyo, iko haja wananchi wote wa sehemu za mikoa ya mashamba na Mkoa wa Mjini wote washughulikiwe namna moja.

Mhe. Spika, nichangie katika sherehe yetu ya Mapinduzi ya miaka 50 hapa Zanzibar, kwa kweli niishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na yeye mwenyewe Makamu wa pili kwa shughuli zake nzuri zilizofanyika za sherehe na mapambo pamoja na maonesho mengi ya sherehe hizo ambazo zilifana sana za aina yake, kwa kweli sina budi nimshukuru sana na nimtakie kila la heri miaka inayokuja 51 iendelee kuliko hivi sasa.

Mhe. Spika, kwa sababu hakuna kitu chochote kisichofanyiwa sherehe kila mwaka, Sherehe ya Mapinduzi ni wajibu wake tuhakikishe kwamba inasherehekewa kila mwaka kwa sababu ni kumbukumbu nzuri za vijana wetu ambao wamekuja sasa kujua kwamba Zanzibar yalifanyika Mapinduzi, nisiseme kama ni Zanzibar tu kwamba Unguja yalifanyika Mapinduzi na Unguja yalipofanyika Mapinduzi wengi wengine hawakuyaona, wengine tuliwaambia tu kwamba Unguja tumeshapindua waje hapa kula starehe zao na ukweli ndivyo walivyokuja wengine kula matunda ya Mapinduzi.

Kwa hivyo, nahakikisha kwamba hao waliokuwa hawapo na walisikia tu kwamba Unguja imeshapinduliwa ndio wanaoleta matatizo, kwamba hawajui maana ya Mapinduzi wala faida yake. Mapinduzi yana faida yake na ndio sisi watu wa Unguja tukawa bado tunasherehekea kwa nguvu zote. Tutayalinda Mapinduzi haya kwa uhai wote hata tukifa potelea mbali, lakini tuhakikishe Mapinduzi bado yanaendelea na watoto wetu waendelee kula neema za Mapinduzi kama tulivyokula sisi na kama wanavyoniona kuwa nimetulia mbele ya ofisi yako Mhe. Spika, kuweza kuitetea sherehe hii ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwa kweli wako watu huwa wanayabeza Mapinduzi na watu kama hao sisi wanatuudhi sana Wanachama wa Chama hiki cha Mapinduzi. Kwa sababu ndio walioleta Mapinduzi katika nchi hii na ndio tunasherehekea. Sasa utashangaa mtu kusema kwamba mimi sipendi kila mwaka kuwa sherehe ya Mapinduzi isherehekewe. Watu wanasherehekea kila kitu baada ya mwaka mmoja mtu anasherehekea baada ya kuowa, sherehe yake kila mwaka anasherehekea, mtu anazaliwa, anasherehekea *birth day* yake.

Nakumbuka hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliniarifu sherehe yake ya kufikia miaka 72 wakati niko Dodoma na nilisherehekea sherehe hiyo. Alivaa suti na alipendeza katika sherehe ile, nikajua kwamba kweli leo ni siku yake ya kuzaliwa. Iweje tusisherehekee sherehe ya Mapinduzi ambayo ndio iliyoweza kutufikisha hapa na tukaweza kupindua na kung'ara na kuzungumza hapa.

Namshangaa rafiki yangu hapa Manyege ana *Harria* sasa wakati alikuwa hana uwezo wa kupanda *Harria*, lakini kwa vile Mapinduzi yamemuwezesha sasa anapanda *Harria*. Hata kwao hakuna barabara na nina hakika hawezi kwenda na gari hilo la *Harria* huko kwao atamalizia hapa hapa Unguja kwamba amepanda *Harria*.

Mhe. Spika, hivi sasa nichangie ukurasa wa 19 kifungu cha 25 kuhusu migogoro ya ardhi. Kwa kweli tuna matatizo mengi ya migogoro ya ardhi.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 37 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi "Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali…" lugha chafu aliyotumia Mhe. Mjumbe hivi sasa naomba afute msemo wake kutumia neno 'Manyege'.

Mhe. Spika: Mhe. Mussa Ali Hassan kuna maelezo hayo ambayo Mheshimiwa ametukumbusha.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, ahsante kwa kunieleza masuala hayo, lakini ukweli kila mtu ana umaarufu wake. Kwa sababu kuna wengine wanaitwa mabangi humu na hilo jina ndio umaarufu wake, yule mwenzetu kama ukimwita jina hilo haonekani wala hajulikani na mwenyewe analipenda. Hata yeye mwenyewe nilimuuliza akanambia kama sikuitwa jina hilo sitoingia tena madarakani mwaka 2015, mwenyewe yupo na ukweli siwezi kufuta hilo suala kwa sababu ndio jina analoitwa na ndio analolipenda.

Mhe. Spika: Mhe. Mussa Ali Hassan kama lugha haiko sahihi kwa mujibu wa Kanuni, tunakushauri uliondoe halafu tupate kuendelea.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Asante Mhe. Spika, kwa kusawazisha hili jina ambalo si zuri ingawa lina umaarufu. Kwa hivyo, nafuta hili jina lakini jina lake Hassan Hamad Omar, *into bracket* hilo jengine. Asante sana.

Mhe. Spika, kuhusu suala la migogoro ya ardhi. Kwa kweli hivi sasa nchi yetu ina matatizo sana ya migogoro ya ardhi kwa wananchi wetu wa vijijini. Utaona sehemu kubwa ya migogoro hiyo ya ardhi hivi sasa ni mikoa ya mashamba, lakini hii inasababishwa na serikali yetu kwamba inataka kujenga sehemu ambazo ni zile zilizorithiwa na wazee wetu, mashamba ya miaka mia iliyopita. Lakini serikali inapokuja kujenga sehemu ile mara nyingi inakuwa hailipi fidia. Kwa hivyo, naishauri serikali inapochukua sehemu iweze kusawazisha wananchi na kuweza kuwalipa fidia zao ili migogoro hii iondokane kabisa, wananchi wasilete matatizo katika serikali au kuisema vibaya.

Mara nyingi wananchi wetu wanakwenda Mahakamani kwa sehemu za ardhi kuwa zimechukuliwa na hawapati malipo yoyote, na sehemu zile sio za heka isipokuwa wamerithi kwa mababu na mabibi, hizo ni mali zao. Ingawa ardhi ni mali ya serikali, lakini utakuta mle ndani ya ardhi mna miembe, mishokishoki, mibuyu, mna kila kitu cha muda mrefu sana. Kwa hivyo, vitu vile angalau serikali ingelikuwa inalipa fidia kwa kuweza kuwasaidia wananchi kuepukana na matatizo kila wakati katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hivi sasa tuna matatizo makubwa sana ya vijana wetu kuhusu madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni mengi kwa vijana wetu na wengi wao wamejiingiza katika madawa haya kama ndio starehe zao, lakini starehe hizi zimepelekea serikali ama nchi kupata matatizo. Serikali ilipopata habari hizi imewasaidia wananchi wengi kuweza kuwajengea *NGO,s* na kuwajengea nyumba za *Sober House*. Kwa kweli mjini pote pana nyumba za *Sober House*, kinachosikitisha kwamba katika mikoa yetu ya mashamba Zanzibar *Sober House* nyingi hamna. Naomba Mhe. Waziri atapokuja atusaidie kwamba kila mkoa ahakikisha unawekwa *Sober House* kwa sababu madawa ya kulevya ni mengi.

Mimi katika jimbo langu kuna kijiji cha Kidimni sehemu inaitwa Paris, watu wengi wameathirika kwa madawa lakini utakuta *Sober House* hamna sehemu ile na utaona kwamba zinasaidia sana wananchi kuwa wanapata kusomeshwa, wanapata chakula na kulala pazuri. Hivyo namshauri Mhe. Waziri atakapokuja ahakikishe kwamba analitolea ufafanuzi kuwa kila mkoa tunaweza kupata *Sober House* kwa ajili ya kusaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea nazungumzia kuhusu suala la Maradhi ya UKIMWI ambayo yameingia katika nchi yetu. Kwa kweli matatizo ya UKIMWI ni mengi lakini utakuta sehemu nyingi katika hospitali zetu za mikoa hakuna dawa hizi na wala hakuna daktari wa kuweza kuwapima wagonjwa wetu. Utakuta wengi wanaumwa lakini hawajui wanaumwa na nini, kumbe vile ni UKIMWI, matatizo yake watu wanaambukizana na utakuta kila wilaya au jimbo watu wenye maradhi haya ni wengi, hasa ukitizama katika jimbo langu la Koani ni wagonjwa wengi ambao wameathirika na maradhi haya. Namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba Wilaya na Mkoa wake hadi jimboni dawa hizi ziwe zinapatikana ili wananchi wetu waweze kufaidika na kuishi kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, wenzetu wengi sana humu ndani wanazungumzia habari ya Bunge la Katiba, hapa sio mahala pake kuzungumzia Bunge la Katiba, humu tunazungumzia mambo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuweza kupitisha bajeti yake ama Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hapo mtu azungumze lolote.

Anapogusia Bunge la Katiba kwa kweli hapa sio sehemu yake, sehemu yake imewekwa na tarehe 5/8/2024 hiyo ndio tarehe ya kuweza kufika kwenye Bunge la Katiba. Huko tunaweza tukazungumzia Bunge la Katiba. Lakini kwa kweli iwe ni marufuku ndani ya jumba hili kuzungumzia jambo la Katiba.

Mhe. Spika, kwa leo sitokuwa na mengi angalau naachia dakika zangu na wenzangu waendelee nafikia hapa, isipokuwa naunga mkono hoja na naipongeza kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii iliyowasilishwa jana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nimeingia sasa hivi hapa, lakini wakati niko njiani nilikuwa nasikiliza redio, kwa hiyo, karibu hotuba yote ya Mhe. Mussa Ali Hassan nimeisikia. Nataka kuweka wazi kitu kimoja muhimu. Katika hotuba yake alisema kwamba, Unguja ndiko kulikofanyika Mapinduzi na wao ndio waliopindua na wengine wote wasiokuwa hao tupo hapa kula fadhila za Mapinduzi hayo.

Mhe. Spika, hakuna jambo baya kama mtu kumsumbulia mwenzake, haya ni masumbulizi lakini nataka nimwambie tu kwamba, Wapemba wao hawaoni tatizo chao kuja huku kikaliwa, yeye aone tatizo Mapinduzi ambayo tunasema ni Mapinduzi ya Zanzibar akayagawa kwamba waliopindua ni wengine na wanaofaidi ni wengine.

Baada ya masikitiko hayo sisi Mhe. Mussa Ali Hassan tunamwita Kamanda itabidi jina sasa tumnyang'anye, mana yake anatupeleka mahali siko. Sasa hivi kila mtu anayesimama hapa anazungumzia umoja, mshikamano, mashirikiano, suala la Unguja na Upemba linakaribiwa kufutwa linabaki kama lipo kwa sababu kuna Unguja na kuna Pemba, lakini unapozungumza huyu ni Mpemba, huyu ni Muunguja, sidhani kama hao ndio viongozi wanaotufaa. Ajitahidi kwa sababu bado bajeti ipo asitufikishe mahali ikawa sasa hivi ni Muunguja na Mpemba, Baraza hili ni la Wawakilishi wa Zanzibar, majimbo 50.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye kitabu hiki cha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuna Idara hii ya Maafa. Mwaka 2011 mwisho mwisho kule kijijini kwangu nilikozaliwa na katika jimbo langu, Kijiji cha Kangagani kulitokea maafa.

Mheshimiwa maafa yanasababishwa na mambo mengi, mafuriko ni maafa, moto ni maafa, ajali za meli watu kuzama wakafa ni maafa, upepo mkali unaoondoa mapaa nayo ni maafa. Kule ulitokea upepo mkali zaidi ya nyumba 25 mapaa yao yakachukuliwa yakapelekwa na upepo unakokujua. Lakini kinachonisikitisha sio hilo ni kwamba serikali iliarifiwa na serikali ilikwenda wakafanya tathmini, wakawapa watu matumaini. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni shahidi, lakini sasa hakuna chochote ambacho tangu siku hiyo kimefanyika, ni bora watu waambiwe kwamba tumekuja kama serikali kuona tu yaishe, lakini unapowapa watu tamaa hakuna chochote kinachofanyika na sehemu nyengine yanafanyika tutatafsiri kitu gani?

Kwa hivyo, mimi nataka waziri akija hapa atwambie wale watu wa Kangagani ambao nyumba zao ziliezuliwa na upepo mkali na si Kangagani peke yake hata Msikiti wa Mjini Kiuyu paa lilichukuliwa likenda likatupwa Kambini huko Kichokochwe, wamewekwa wapi? Awaambie kwamba hakuna chochote ambacho mtapewa na kama kiko basi awaambie watapewa lini, vyenginevyo mnaweka watu na tamaa. Hilo la pili.

Jengine katika kitabu hiki ukurasa wa 64 kitabu cha Hotuba ya Makadirio iliyowasilishwa jana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Baraza la Wawakilishi katika mwaka 2013/14 liliidhinishiwa shilingi 14,8452,000,000, mwaka 2014/15 mwaka ambao unakuja, linaombewa shilingi 14,564,000,000; hii ni tofauti na shilingi 288 milioni. Sasa ni vizuri wakati wa kufanya majumuisho tofauti hii wengi walitegemea kwamba mwaka jana au mwaka huu ni kiasi hiki, mwakani kiasi hiki, lakini maelezo ya hizi shilingi milioni 286 ambazo ni pungufu ni kwa sababu zipi?

Shughuli za mwaka jana nyengine zimeachwa. Lakini ninavyofahamu mimi Baraza la Wawakilishi shughuli zake ni *very common*, vikao vingapi, kamati ngapi, safari ngapi na posho lingepunguzwa, mimi ningesema sina hoja kwamba pengine ni kupunguzwa kwa posho, au ingekuwa vikao vimepunguzwa ningesema sawa. Sasa naomba

atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho basi atueleze kwa nini tafauti ni kubwa kiasi hiki ya bajeti ya mwaka na hii inayoombewa ya mwaka kesho.

Mhe. Spika, kuhusu Tume ya Uchaguzi *ZEC*. Wadau wote wa uchaguzi isipokuwa CCM wanailalamikia sekretariet ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mimi imetokea kwamba ni kiongozi wa chama tena Naibu Katibu Mkuu Chama cha Wananchi *CUF*, kwa hivyo nahudhuria vikao vingi vya Tume ya Uchaguzi na Vyama vya Siasa, sizungumzii hii kutoka usingizini na kama mimi sipo basi kuna watu wanakwenda wanaotuwakilisha wanatoa ripoti ndio maana nikasema hivyo.

Mhe. Spika, sekretariet ya Tume ya Uchaguzi iliyopo ni mbovu, ni chafu, si adilifu, haifai. Katika masuala ya watu wengi, wabia wengi, washiriki wengi wa jambo kama kuna suala la uadilifu, suala la haki, kuna kitu kinaitwa *benefit of doubt*, kama watu wanakulalamikia unatakiwa uachie ngazi, uking'ang'ania kwamba ni mimi, mimi sibadiliki, sibadilishwi una lengo gani?

Mhe. Spika, hivi karibuni uchafu wa *ZEC,* Sekretariet yake sizungumzii Wajumbe, sizungumzii Kamishna 7, nazungumzia sekretariet ya *ZEC.* Hivyo Mheshimiwa kuna watu hapa tangu *ZEC* ilipoundwa, tangu chaguzi za vyama vingi zilipoanza mwaka 1995 mpaka leo wanageuzwa kama chapati; imewekwa upande huu, weka upande huu na hawa hawa kila baada ya uchaguzi basi utamkuta mtu kama alikuwa anaendesha *COROLLA* ana *PRADO,* si zawadi! si choyo, mimi nina *PRADO* mbili. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, si suala la choyo, si rahisi mfanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ukamkuta ana vitu ambavyo haiwezekani kabisa kumiliki, utatia wasi wasi tu, na kazi kama hii anayofanya Mheshimiwa tunazungumza haya si kwa sababu thamani sio sawa lakini na haya yapo.

Natoa ushahidi wa Secreteriet ya *ZEC* ilivyokuwa haifai na inaipa mzigo Serikali hii ya Zanzibar tena mfano wa juzi sikupeni ya siku nyingi. Mhe. Spika, tulifanya uandikishaji hapa huu uliopita majimbo yote 50, wakatoa taarifa kwamba majimbo 5 baadhi ya majina sijui yameliwa na nini maana yake haiingii katika akili. Umeme ulikuja uka-*fluctuate* ukafanyaje, majimbo 5 kuna baadhi ya walioandikishwa wakafutika. Mambo haya aambiwe mtoto mdogo wasiambiwe watu wenye akili zao, wanaojua *System* za *IT,* Jimbo la Donge likatajwa, Jimbo la Kitope, Bumbwini, Mfenesini, Bububu tukaandikiana sana na Tume ya Uchaguzi lakini hata majawabu hupati. Utaalamu sijui vipi na vipi.

Hivyo kweli, kazi muhimu kama ile unashindwa kuwa na kifaa ambacho umeme ukikatika hakuna athari inayotokea katika ku- *save data* zako. Baadae wakasema wanarudia hii haisomwi kwenye bajeti, fedha hizi za kurudia wamezipata wapi? Lakini si hayo mambo ya fedha peke yake baada ya kurudia watu mia tano na ushee hawakuweza tena kuandikishwa. Hii Mhe. Spika, ni kawaida hata *by election.* Lakini sasa kosa la nani? Kosa ni la Tume ya Uchaguzi. Sasa watwambie fedha zile wamepata wapi, udanyanyifu huu maana mimi naita udanganyifu waliotufanyia wasitufanyie tena. Serikali wanaitia gharama isivyo lazimika.

Daftari la wapiga kura Mhe. Spika, halifai linataka uhakiki tena wa hali ya juu kama tunafanya uchaguzi wa haki na huru wanaoingia kwenye uchaguzi wajiridhishe ndio maana yake. Uhakiki wa daftari tena uhakiki huu Mhe. Spika, wadau wote wa uchaguzi kila anaependa ashiriki. Sio kwamba tunafanya mambo mapya hata kidogo ni mambo yanafanyika.

Hili la *Data* kupotea la Majimbo 5 lilifanyika Zimbabwe *System* ile ile wanakopia tu ...

Mhe. Spika: Una dakika tano Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Kwa hivyo, Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi Sekreteriet yake iondolewe, vijana wenye uwezo kuliko wao wapo, *system* iandaliwe ili tuwe na Sekreteriet mpya. Mhe. Spika, zaidi ya miaka 15 mtu yuko hapo hapo ana lipi jipya, uhakiki wa daftari kama tuwe na uchaguzi wa haki na huru ni jambo la lazima.

Kwa hivyo, akija hapa Waziri au Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Mwenyewe atwambie Sekreteriet hii inaondoka lini na lini wengine watawekwa. Uhakiki wa daftari unafanyika lini na fedha hizi zilizotumika kwa ajili ya marudio ya uandikishaji wa majimbo 5 walizitoa wapi na hatua gani zimechukuliwa kwa wazembe hawa waliosababisha hasara hiyo kwa serikali.

Mhe. Spika, la mwisho kwa sababu ya wakati. Watu wamezungumzia na humu imeelezwa kwamba moja kati ya mambo serikali itakayofanya mwaka huu wa fedha unaokuja ni Tume kufanya uchunguzi, yaani lugha imeviringishwa lakini kwa ufupi " Lisemwalo lipo kama halipo linakuja" ishaenea kila mahali hii ni geresha tu. Tume ya Uchaguzi ishakusudia kukata majimbo na inasemekana Waheshimiwa kama wenzangu walivyosema "toba sikio" Pemba majimbo 3 yatapunguzwa.

Mhe. Spika, Katiba imeeleza vizuri vipi wanagawa majimbo kuna *criteria* 5 zitayochukuliwa pale eti ni Sensa. Sasa nawaambia Tume ya Uchaguzi sensa maana yake ni idadi ya watu. Mwaka 2012 ilifanyika sensa na nyote mnajua sensa ilivyofanyika mpaka Serikali ikaomba viongozi wengine wende katika maeneo maalum kuzungumza na watu.

Sasa ukichukuwa *data* za uandikishaji wa *NIDA* vitambulisho vya kitaifa na sensa iliyofanyika mwaka 2012 ni mbingu na ardhi. Kwa hivyo, msije mkatueleza hapa maana yake sensa tumezungumzia *Current Population. NIDa* wameandikisha watu tofauti ya maelefu kila Jimbo kila Sheha. Kwa hivyo, kinachozungumzwa maana yake Wapemba wamehama, si kweli Waheshimiwa na kwa utaratibu huu miaka 10 iliyopita Majimbo 21 matatu yakapunguzwa yakabaki 18 keshokutwa tena mnataka kupunguza. Kwa utaratibu huu inaonekana kabisa dhumuni kubwa ni kupunguza Uwakilishi kwa Pemba na labda anayosema Mhe. Mussa Ali Hassan hatukupindua. Kama hamtutaki twambieni msitudhulumu, msitutie unyonge, kila kitu kwa utaratibu huu maana yake ni kwamba itafika wakati Pemba iwe majimbo mawili si ndio sababu yenu, msitufikishe hapo. (*Makofi*)

Zanzibar ni Unguja na Pemba au leo semeni hapa kwamba Zanzibar maana yake ni nini? Chonde chonde Tume ya Uchaguzi, Sekreteriet imesababisha mambo chungu nzima maafa tangu 1995 wasituletee tena maafa mengine 2015. Sekreteriet haifai mbovu si waadilifu wanatumika isivyostahiki, iondoke bwana hatuna tatizo hata kidogo na kuweka watu wengine wenye uwezo mkubwa kuliko wao.

Inakuwaje Jimbo la Kiembe Samaki watu wanaopiga kura wanatoka Kidoti? Inakuwaje unakwenda umepiga kura 2010 unakwenda pale jina lako halipo? Ah ni *IT* ni *IT* nani asiejua kwamba Mhe. Jaku Hashim kichwa chake kinaweza kutolewa kichwa changu mimi kikawekwa pale *IT* hivyo vichwa ni vingapi kwani vyote viwili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, chonde chonde Tume ya Uchaguzi wasije wakatuletea tena maafa ambayo washayasababisha. Sekreteriet haikubaliki iondoke itafutwe nyengine ambayo wadau wa uchaguzi wataridhika nayo, uhakiki wa daftari ni jambo la lazima kama mnakusudia kufanya uchaguzi wa haki na huru. Vyenginevyo tutakuwa tunaimba hapa wala hakuna muitikiaji. Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kutuwezesha kufika hapa na tukaweza kusimama na tukazungumza na vile vile nakushukuru na wewe kunipa nafasi nikaweza kuzungumza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais na watendaji wake wote.

Mhe. Spika, nitakuwa katika ukurasa wa 20 watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, ukitaja watu wenye ulemavu basi mimi naona uchungu mkubwa sana kwa sababu nililokuwa siwezi kulifanya mimi najua na mwenzangu hawezi kulifanya. Hapa tunaambiwa watu hawa wako waliosoma wana Shahada za Uzamili, wana Vyeti ya Utawala na mengine. Hapa pana Jamii na Kisiasa mlemavu hawezi akaingia kwenye siasa na hata akiingia Mhe. Mwinyihaji Makame nikienda pale wala hawanipi kura zao.

Kwa hivyo, watu hawa namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais waliokuwa wana sifa hizi kwa kila itakapotolewa ajira basi aweze kumega kidogo kidogo, angalau watu hawa waweze kupewa ajira kuweza kuwainua kimaisha ili waweze kufaidika na wao. Ikiwa panatakikana watu 50 wapewe 5 tu 3 watatoka Unguja na 2 watoke Pemba kwa Mikao. Kila kipindi wakimegwa megwa hawa watapata nafasi. Kilio ni kikubwa sana cha watu wenye ulemavu hawapati ajira, hawapati kitu chochote.

Mhe. Spika, ujika katika udhalilishaji wa watu wenye ulemavu; jamani dunia hii ni dunia gani tuliofika karne hii kwa sababu sisi tulipokuwa watoto tuko walemavu kutwa tunashinda maporini tunachuma mapera, tunachuma embe na hatubakwi na wala hatudhalilishwi. Leo kuna udhibiti wa watu hawa wako majumbani tu hawatoki saa zote watu hawa wanafanyiwa vitendo vya kusikitisha na linalotusikitisha Mhe. Spika, ni kuwa watoto hawa wakifikwa na

matatizo kesi hizi zinamalizia Mahakamani, ukihoji unaambiwa hakuna ushahidi neno ninaliona mwenyewe mtoto wangu kafanyiwa lakini siku mbili siku tatu utaambiwa hakuna ushahidi. Ushahidi mdogo ni mtoto wa Mkoani mama yake aliona mwenyewe kitendo lakini yule ni wa mkubwa fulani, alikamatwa na akaekwa ndani siku mbili akatolewa baba yake akamtorosha.

Hili jamani ni jambo la kusikitisha namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais watakaokamatwa na udhalilishaji wa kijinsia wakiwa ni kwa mtoto mwanamke aliefanyiwa, akiwa ni mtoto mwanamme hii mijitu ipewe adhabu kali wakome. Hii kuchezea chezea ndio maana wakafika hapa hawaogopi. Mtoto anabakwa ndani, ukipeleka kesi unaambiwa ushahidi haupo na huko Mahakamani kuna nini? Watu hawa wao hawana watoto wenye ulemavu, hawana jamaa zao walizaa walemavu mpaka tukapata kudhalilishwa namna kama hii?

Tunaomba serikali isimame makini sana hawa ni watu kama watu wengine na kitabu kinaeleza hapa wanastahiki kwa mambo yote wafanyiwe na huruma iwepo. Hata alie mzima baadae huwa mlemavu, wangapi waliopata ulemavu katika hali ya juu kabisa wala hawajui kama watakuwa walemavu, tunaiomba serikali.

Mhe. Spika, mie mamshukuru sana yule babu na namuombea dua Mwalim Khalfani. Mhe. Spika, Mwalimu Khalfani ndie alietufikisha hapa walemavu, alikuwa akipita kila kijiji na ulemavu wake bwana yule kutushajihisha, tulikuwa hatujulikani tumefungiwa majumba hatuonekani, hatujui chochote. Bwana yule akaweza kutushajihisha kuweza kuunda chama mpaka tukafika hapa tulipo katika Jumuiya ya watu wenye ulemavu. Akija pale kutufanyia semina anatufundisha, maana kuna watu wengine hata kusema hawawezi basi ananyanyuliwa anaambiwa sema, panaandikwa kiambazani azunguze kama muombaji wa kura. Sasa asimame ajue anatoka kijiji gani, elimu gani, halafu aombe watu walioko pale kura, akitufindisha hivyo bwana yule.

Kwenye mambo ya biashara sie katufundisha Mwalimu Khalfan, katuletea semina si mara moja wala mbili na wataalum kutufundisha mambo ya biashara na wala hatukusoma biashara kabla; ndio kisa mimi cha kupata mkopo ukaninyanyua mimi mpaka nikajenga. Mhe. Spika, Serikali tunaiomba iwe na juhudi kuwanyanyua hawa, inaweza.

Nije kwenye ukurasa wa 46 na 48. Mhe. Spika, Idara ya Maafa inaonesha hapa kuwa inafanya semina Unguja na Pemba Mikoa na Wilaya zote watu hapa wanashiriki wakiwemo watoto mpaka watu wenye ulemavu pia. Lakini sasa nataka niulize haya maafa yaliyokusudiwa humu ni maafa yepi? Maana maafa yapo ya aina nyingi.

Mhe. Spika, yakiingia maradhi ni maafa hivi sasa tunasikia kushaingia maradhi wala hayajulikani. Je, Mheshimiwa anajipanga vipi kupata chanjo za watu wake na dawa za kupuuliza kumuua huyu mdudu atakaetuletea nakama?

Mhe. Spika, Mhe. Makamu Pili wa Rais naomba awe makini kwa sababu akisema maafa, maafa ni mengi si maafa ya kuingia moto au kuzama meli tu. Ulipoingia moto Micheweni mimi nilikuwa Singida nikapigiwa simu ilikuwa nimefiliwa pale tukasikia Micheweni kumeingia moto, hangaika hangaika ya Mkuu wa Mkoa hajampata mtu yoyote na Zima Moto wako Chake chake, tizama kutoka gari ya Mkuu wa Mkoa Wete kuja Chake chake kuwatafuta watu wa Zima Moto huo moto wewe ni rafiki yako, utakubakishia nini? Hata lilipopatikana Zima Moto maafa yameshaingia.

Namuomba tu Mhe. Makamu wa Pili, tunajua serikali yetu ni masikini lakini alau kama ilikuwa kama lile gari kila Mkoa pale lipo basi maafa huwa yanapungua. Maana litakimbilia kwenda kuzima moto. Si kama kutoka kule kuja kufuatia Chake chake.

Halafu Mhe. Spika, vyombo vya usafirishaji, walemavu wanasafiri, meli ipatwe na matatizo nani atamshughulikia mlemavu gani, waliopo pale wote watavaa ma-*life jackets* wewe unasota huku kwenye kiti, ikiwa hamna mtu angalau alie pale wa kumtupa kwenye maji na yeye. Tunamuomba Mhe.Makamu wa Pili wa Rais awe makini katika vyombo vyetu kutuwekea watu ambao wanaweza kuwasaidia watu kama hawa. Kwa sababu tukisema tu tunangojea wategemezi waliomo kwenye meli wale na wao saa nyengine wana mambo mengi wala hawakumbiki.

Halafu Mhe. Spika, nikija katika Baraza la Wawakilishi. Baraza la Wawakilishi mimi nimeingia mwaka 2005. Jumba hili linajengwa mimi nipo, inaundwa kamati tunakuja hapa kukagua na siku moja nilisema Barazani lile jumba mbona silioni kipandio cha walemavu halina *lift*. Kwa sababu haiwezekani kujengwa nyumba kama hii na isiwekwe sehemu ya watu waliokuwa hawajiwezi. Siku moja sie kulikuwa na mkutano huko juu alitokea Mhe.

Shawana Bukhet Hassan anaumwa na mgongo alimalizia kwenye ngazi, alisema mimi ngazi siziwezi Mhe. Shawana Bukhet Hassan sikwambi mwengine au mimi.

Naomba kupitia Serikali na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais japo *lift* ya dharura ya kuibandika hapo juu iwekwe. Yule bibi anaekuja hapa akija mimi namuonea imani sana kwa sababu mimi najiona mzima kuliko yeye alivyo, namuonea huruma sana na kila siku napiga kelele hizo hizo jamani jengo halina urafiki wa watu wenye ulemavu, tunamalizia hapa kwa sababu wengine hatuwezi lakini ni mtihani.

Mhe. Spika, nyie ndio mlienipeleka India kuniunga kiungo; nna kiungo cha kuunga, haya tizama ngazi ile nikidondoka huu mguu ukifunguka si mtihani? Lakini kama pana *lift* ni haraka kukupeleka huko juu na lazima wakati mimi ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nihudhurie kwenye vikao.

Kuna wenzetu mimi nilichangia mara moja ilikuwa 2008 Kikwajuni, nikasema jamani iko siku tutakuja mpata mwenzetu anakwenda kwa mafuti au tumbo na ataingia katika Baraza hili, ataingiaje? Tunaomba kwa kupitia Mhe. Makamu wa Pili kama alivyosema pale, alisema hii ilikuwa ni gari Serikali yeye ndie *engine* , basi tunampa malalamiko yetu na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa uwezo na kumsaidia kwa nia yake safi aweze kutusaidia na kutuona.

Mhe. Spika, mambo mengine ni aibu kwa sababu saa hizi mfano atokee mwenzetu kutokea mbali huko aseme anakuja ni mlemavu, kwa sababu wenzetu wameendelea akifika hapo juu atapanda vipi, ukienda kwao wanaingia na vigari mpaka chooni, unaingia na kigari chako mpaka kwenye lifti. Mimi nimesafiri kwenda India nimepakiwa kwenye kigari napandishwa kwenye lifti naingia huko. Sasa leo hapa sisi tunapata matatizo, tuoneeni huruma sana.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atupe uwezo, atupe salama na amani. Lakini mimi bibi yangu alinambia maneno haya, akitwambia kila siku, na bibi yangu amekufa ana miaka 110. Akitwambia vuta n'kuvute ya moja inachanika. Halafu babu yetu akarudi akamwambia wewe usiwaambie hivyo, wanaovutana ikikatika wanaanguka wote.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii ya kutoa mchango wangu mfupi sana, maana Mhe. Raya Suleiman Hamad karibuni *points* zangu tatu ameshazichukua. Kwa hiyo nitachukua muda wako mfupi tu.

Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya ya kuweza kusimama hapa nikaweza kuchangia kitabu hiki cha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, mimi nitaanza mchango wangu katika sekta ya huduma za jamii. Mhe. Spika, huduma za jamii ni nyingi, lakini Serikali yetu ina utamaduni wa huduma za jamii nyingi kuwepo maeneo ya mjini kuliko vijijini. Mhe. Spika, Serikali siku nyingi inasema kuna watu wanaoishi katika mazingira magumu, kuna watu waliokuwa na kipato cha chini, na tukiangalia asilimia kubwa ni watu wanaotoka vijijini. Kwa hiyo kwa sababu Wizara hii ndio wasimamizi wakuu wa shughuli za Serikali, mengine tutamwambia yeye Mhe. Waziri pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kusikiliza vilio vyetu katika huduma hizi za jamii.

Kwanza Mhe. Spika, nikiitizama ile Wilaya ya Micheweni huduma za jamii zilizoko kule ni hafifu. Serikali yetu inajitahidi kwa kuzingatia masuala ya maji safi, umeme na halikadhalika. Lakini tuangalie skuli nyengine zilizoko vijijini zilivyokuwa zina matatizo na ukosefu wa umeme, nimepita maeneo mbali hawana uwezo walimu kusogeza huduma ile ya umeme katika maskuli yao. Mhe. Spika, pana skuli ya Tumbe pale siku zote ni kilio cha suala la umeme. Wana kompyuta walizogaiwa huu hata sijui mwaka wa ngapi wanashindwa kuzitumia. Na ukizingatia skuli ile pana madarasa mpaka la kumi na mbili. Sasa skuli kama hizo lazima Serikali izizingatie kuwapelekea karibu ile huduma ya umeme pale ili na wao wale wanafunzi wetu na watoto wetu wafaidike na haya.

Jengine mpaka leo tumeshindwa hata kituo pale. Wilaya ya Micheweni ni watu wanaoishi katika mazingira magumu lakini hata kile kituo pale cha kununulia umeme tumeshindwa kuwawekea. Siku zote tunapiga kelele kwa Waziri wa Nishati huduma zote zipo mjini Wete, Chake Chake. Sasa wale watu wanaodaiwa kuwa wamo katika mazingira

magumu ndio wale waliokuwa huduma zile muhimu wao hawazipati, wao ndio wafuatilie huduma maeneo ya mjini. Kwa hiyo tunaiomba Serikali kwa hilo izingatie kidogo angalau huduma nyengine maeneo kama hayo basi ziweze kupita.

Jengin analolizungumza Mhe. Raya Suleiman Hamad ni suala zima hili la majengo; miundombinu iliyokuwa haikidhi haja kwa watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, hili jengo sidhani kama kuna mategemeo ya kuja kuvunjwa tena ili kujengwa jengine. Hili ni Baraza la Wawakilishi pesa nyingi zimepotea hapa na huduma hazikidhi haja kwa watu wenye ulemavu. Kwa hiyo tunaiomba Serikali wafanye hali yoyote kama humu ndani haiwezekani japo huko nje basi waweze kuwawekea miundombinu ya watu wenye ulemavu, ili na wao waweze kufikia huduma hiyo kwa sababu chombo hiki ni muhimu kwa jamii zote.

Mhe. Spika, jengine ni suala la mazingira, pia tunaishukuru Serikali kwa juhudi zao wanazochukua kwa kushughulikia masuala ya mazingira. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki kasema hapa kwamba suala la kutunza mazingira lina umuhimu mkubwa sana katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii na kupunguza umaskini. Sasa Mhe. Spika, suala hili juu ya kuwa Serikali wana malengo mazuri lakini pia Serikali wameshasema watasimamia katika suala hili. Lakini Mhe. Spika, kuna tatizo kubwa linalotukabili mabonde mengi yanayoingia chumvi hasa katika kisiwa cha Pemba. Juhudi zinafanywa na Serikali lakini hili nalo pia waliangalie kwa makini sana. Itafika pahala watu watalima na watashindwa kuvuna kutokana na chumvi inayoingia katika maeneo mengi ya mabonde.

Suala jengine ni Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa Kwanza wa Rais hasa katika kisiwa cha Pemba kuna suala zima la ofisi hii kukosekana kwa usafiri. Ingawa katika kitabu hiki Mhe. Waziri ameshasema mwelekeo wa vipaumbele vya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mwaka huu moja ni ununuzi wa gari ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini hilo halitoshi Mhe. Spika, hawa ni viongozi wetu wa kitaifa na Zanzibar ni visiwa viwili vya Unguja na Pemba, sasa licha ya usafiri lakini sasa hivi umeshafika wakati viongozi kama hawa kukawa na nyumba za kudumu kule za kufikia viongozi wetu, kile ni kitu muhimu.

Kwa hiyo Serikali ilione hili suala, siku zote isitowe gharama kubwa ya kukodi majumba, watakodi majumba mpaka lini. Lakini zikishajengwa zile nyumba basi viongozi watakuwepo wakiondoka wale wataendelea wengine nyumba zile zitabakiwa na jukumu la ukarabati tu. Kwa hiyo tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais suala hili aliangalie kwa umakini sana.

Jengine ni suala la uratibu wa shughuli za Serikali. Katika kitabu hiki Idara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi 8 za viongozi wakuu wa kitaifa zilizotolewa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, nashukuru kwa hili. Lakini leo nataka kumkumbusha Mhe. Waziri kwa sababu mimi nikishasema jambo langu na mtu akishakuniwekea ahadi basi siku zote nitamkumbusha suala hilo. Mhe. Spika, nakumbuka kikao cha pili Mhe. Waziri nilimuuliza swali langu na akanambia suala hili atalifuatilia. Nilimuuliza kuwa huyu aliyekuwa Waziri Kiongozi wa Awamu ya Sita yeye ni miongoni mwa Viongozi Wakuu wa Serikali. Mhe. Spika, Mhe. Waziri akanambia ni kweli na yeye ni miongoni mwa Viongozi Wakuu wa Serikali.

Kwa hiyo lile suala langu akanambia atalifuatilia. Lakini sijaona ufuatiliaji ule matokeo yake ni yapi. Kwa hiyo na hapa tumeshaambiwa kuwa Idara hii tayari kuna ahadi hazipungui 8 zilizofuatiliwa. Sasa Mhe. Waziri bora kusema ule ukweli tu ulivyo kuwa hili haliwezekani, lakini ukisema kwa sababu unafuatilia ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali ina maana zifuatiliwe zote zile zilizoahidiwa. Au kuna nyengine ni muhimu na nyengine si muhimu kwa wananchi?

Hapa asubuhi liliulizwa swali hili hili la kiongozi huyu huyu katika Skuli ya Kisiwandui pia alikwenda akaweka ahadi. Sasa watu hawasahau wanapowekewa zile ahadi ni wao wanafika pahala wakajenga matumaini kuwa suala hili litatekelezwa. Kwa hiyo Mhe. Waziri hebu njoo utwambie haya masuala ya viongozi ni viongozi ambao pengine mnatumia Rais tu. Lakini kama ni viongozi wote wa kitaifa basi wafuatiliwe wote, au hakuna uratibu tuambiwe tu kuwa hakuna uratibu shughuli zinazofanywa ni zile ambazo pengine mnazipa kipaumbele.

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa; kama alivyouliza Mhe. Raya Suleiman Hamad na mimi sikufahamu hivyo hivyo. Lakini nataka niseme mimi kwamba maafa kuna ya aina nyingi, kama yalivyoelezwa kuna uingiaji wa moto, kuna uzamaji, kuna maafa ya kila aina. Sasa katika suala hili Mhe. Spika, matokeo mengi yanajitokeza;

Tumbe nakumbuka kuliingia moto majumba mengi yakateketea. Moto ule ukaendelea na Micheweni majumba mengi yakateketea. Tatizo hasa ni kukosa kuwepo na kituo. Haiwezekani kuwa gari itoke *Chake Chake Airport* kwa kupitia maeneo hayo ikaweza kuokoa majumba yale.

Sasa Mhe. Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu suala hili hata humo kwenye Mawizara yanayohusika na masuala haya mimi siku moja niliuliza kwenye Kikosi cha Zima Moto lakini wakanambia kuwa walitafuta viwanja maeneo ya Micheweni na Wete wakavikosa. Lakini kwa sababu hili suala linatuathiri sote nilimfuata Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na yeye akanambia kuwa si kweli. Nilipokuja kulisema hapa Waziri mwenyewe akasema kwa kuwa mimi watendaji wangu hawawezi kusema uongo. Lakini na mimi nikaamini kwamba si kweli kwa ajili ya kuwa Micheweni hakuwezi kutokea kiwanja cha kujengea Kituo cha Zima Moto japo gari moja ikawekwa pale. Kwa sababu wananchi wetu tunawajua hasa wanaoishi katika maeneo hayo, hawana utaalam hata ule wa kujenga miundombinu ya mazingira mazuri katika majumba yao. Sasa kama hakuna huduma hiyo ina maana nyumba moja tu ikishika moto zote zinaendelea, kwa sababu hakuna utaratibu mzuri.

Kwa hiyo Mhe. Waziri hili suala mlione hasa huku Wilaya ya Micheweni muweze kutujengea kituo pale japo kuwepo na gari moja ikitokea athari kubwa wanaweza wakawaita wenzao. Lakini kama hapana hata gari moja mpaka pengine ipigwe simu mara mia mtu hapatikani, hili ni tatizo.

La mwisho Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho kuna suala zima lile la ujenzi wa Ikulu ya Micheweni. Mhe. Spika, ni lini ujenzi ule utamalizika. Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uhai na uzima akatuwezesha kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Lakini pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kunipatia nami fursa hii ya kuweza kusema machache katika hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, niseme kwamba nampongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais jinsi alivyoiwasilisha bajeti hii katika Baraza lako hili tukufu. Lakini pia sina budi niwapongeze watendaji kwani najua chochote ambacho kinawasilishwa ukumbini kuliwa basi huwa kuna watu ambao walifanya matayarisho hayo nao ni watendaji wake.

Mhe. Spika, mimi nianze na kusema kwamba "Usipoziba ufa utajenga ukuta". Hiyo ni falsafa iliyozoeleka sana kusemwa na watu huona ni methali ya Kiswahili. Lakini la pili niseme hivi "Zanzibar ndipo petu hatuna pengine katu asitudanganye mtu".

Baada ya utangulizi huu haya nayaacha hapo naingia katika bajeti hii. Mhe. Spika, katika kitabu hiki ukurasa wa 19 katika kifungu cha 35 kimezungumzia migogoro ya ardhi. Tangu tumeanza hapa linazinduliwa Baraza hili Rais alilizungumzia sana jambo hili la migogoro ya ardhi, jambo ambalo inakwenda miaka mitatu na ushei sasa. Na alisema kwamba hili ni suala ambalo linahitaji utatuzi wa wale ambao wamehusika na migogoro hiyo. Kwa muktadha huu inaonesha dhahiri sasa kwamba wale ambao wametenda imekuwa ni vigumu kuweza kusuluhisha suala hili. Mbali ya migogoro mingi ya ardhi iliyoko Mahakamani lakini bado migogoro ya ardhi imekuwa ikiibuka siku hadi siku, suala ambalo limeleta mtafaruku mkubwa baina ya wananchi wenyewe kwa wenyewe katika taifa letu.

Mhe. Spika, tatizo hili mara nyingi kabisa inaonesha dhahiri kwamba hakuna jambo lolote lililokuwa halina mwanzo wake. Kwa vyovyote vile itakavyokuwa naamini tangu Mapinduzi ya 1964 tulijiwekea taratibu mbali mbali na sheria tukizitumia kuona nani mmiliki wa eneo fulani na nani anahusika na eneo fulani. Napatwa na mshtuko mkubwa kuona kwamba viongozi wetu tuliotarajia waondoe migogoro hii, lakini wao wanashadidia migogoro ya ardhi. Nasema hili ikiwa kuna mambo mbali mbali yaliyojidhihirisha. Tuliunda Tume hapa, Mwenyekiti wake akiwa Mhe. Ali Mzee Ali tuliona yaliyoibuka. Haya tulitarajia kwamba kwa wakati huu kungekuwa kumeshaanza *process* ya kuona mambo haya yanafuatiliwa kwa sababu tayari Tume ambayo imetumia fedha kadhaa za walipa kodi, tayari inapatiwa ufumbuzi. Lakini ukiangalia maeneo mengi ya wananchi ambayo wamekuwa wamepewa heka tatu tatu na Serikali yetu baada ya Mapinduzi matukufu ambayo tunajivunia hapa na kila mmoja kutaka kusema na kujilabu kwamba yeye ni mwana Mapinduzi, tukisahau kwamba sote ni wana Mapinduzi.

Niseme kwamba unakwenda wewe kwa sababu ya pesa zako, ukijinadi kwa sababu ya uwekezaji, kumbe wewe una unachukua tu na kumuonea yule mnyonge. Hivi ndivyo tulivyo na haya yamefanyika katika maeneo kadhaa na

waliohusika na migogoro hii tunawajua na tunawafahamu. Ninalirudia tena lile neno langu "Udugu wetu wa damu isiwe sababu ya kudhulumiana, isiwe sababu ya kuoneana, isiwe ndio sababu ya kuona kwamba mkubwa amle mdogo".

Nchi yetu inaongozwa katika misingi ya demokrasia na utawala bora sio huu tulionao leo. Tunalazimika tujifunze na tuthamini kile kidogo alichonacho mnyonge ambacho yeye anajiendeleza au wanajiendeleza wananchi kwa shughuli zao. Serikali inasahau hili. Serikali inapotaka kufanya uwekezaji nayo inalazimika kuangalia na kufanya tafiti mbali mbali na kuweza kuridhika kwamba eneo hili tukiwaondoa akina fulani na fulani litafaa kwa namna fulani, lakini wao tutawaweka wapi, tutawafanyia nini.

Maeneo ya wananchi ya kihistoria ambayo kabla ya 1964 walikuwa wanayo, leo tumekuwa tumefanya ya uwekezaji. Hivi ni vitu vya ajabu sana, haya tunayoyasema ya uwekezaji tunasema ni kwa maslahi ya wananchi. Kama hivyo ndivyo tunavyofanya hivi kwa maslahi ya wananchi hawa, sasa inakuwaje wao usiwashirikishe na kuona kwamba wana faida gani na hasara gani kuwepo pale. Tunachukua tu, wewe hujui serikali! serikali bwana ina mkono mrefu, serikali maana yake itafanya. Si kweli, ki-Katiba wananchi wamekasimu madaraka yao wakawapa ndugu zao wakakaa kwenye madaraka na wao wakaona kwamba wamekuwa watii juu ya serikali yao. Hiyo ndio demokrasia. Huu ndio utawala bora wa kwamba kiongozi amuonee huruma mdogo. Migogoro ya ardhi ninapenda nimwambie Mhe. Rais...

Mhe. Mjumbe Fulani: Rais tena!

Mhe. Ashura Sharif Ali: ...ndio Rais ambaye aliyesema kwamba migogoro hii waachiwe wenyewe waliyoianzisha wanaweza. Hawawezi wanaendelea kuchukua ardhi nyengine na migogoro kadhaa ipo Mahakamani na haipati ufumbuzi. Ninaiomba sana serikali kama tumefikia hatua hizi, hebu jamani kama kweli sisi ni wana demokrasia wa kweli, tunafuata utawala bora, tunakwenda kwenye misingi ya haki za binadamu, tutangaze mali zetu sasa.

Maana tutaondoshana wasi wasi na shaka tulizonazo kwamba hii ni ya nani, hii ni ya bwana mkubwa. Hakuna hilo, si tulifanya Mapinduzi ya 1964 tukasema hawa mabwana wakubwa ambao wamechukua ardhi, watu wetu wanalipa fidia, sasa waondoke ili ardhi hii imilikiwe na serikali. Serikali ina watu wake nao ndio wanaostahiki.

Maana Hayati Karume alisema tuwape eka tatu tatu wanyonge ili waweze kutafuta maisha yao. Leo tatizo la ardhi limekuwa tena ni tatizo tena sugu, dawa yake haijaonekana. Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wewe ndiye mtendaji wa shughuli za serikali, hebu liangalieni upya suala hili.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye ukurasa wa 21 katika kifungu cha 39 "mapambano dhidi ya madawa ya kulevya". Mhe. Spika, ninataka niseme nguvu kazi ya taifa letu ni vijana na tumevamiwa na hali ngumu ya madawa ya kulevya nchini kwetu, vijana wetu wote sasa wanarembua macho tu, ni mtihani. Nguvu hizi tunazozitarajia waweze kushiriki katika shughuli mbali mbali za uzalishaji, wao wajikimu kwa wao lakini na taifa lipate kuchukua kodi kwao kwa kuliendeleza taifa. Hakuna mambo lakini tujiulize sisi, haya madawa yanalimwa kwetu, ndio swali. Madawa hayalimwi kwetu, yanaingizwa.

Mhe. Spika, hivi kweli sisi ulinzi tulionao, mzunguko mzima wa vikosi vyetu likiwemo na Jeshi la Polisi kwa Jamhuri ya Muungano, jamani hatuwezi kudhibiti! Mbona yale tunayoyahitaji tunafanya upekuzi mkubwa, karafuu moja isisafiri na tunazishikilia. Tuna nini? Mimi ninasema tena tukiendelea kuogopana baina ya wananchi tutaliuwa taifa hili, hatimaye huyo wa kulirithi wa kuliendeleza na viongozi wema hawatopatikana. Hivi ndivyo tulivyo.

Serikali ninaiomba iwaambie askari wanakamata madawa ya kulevya, yakifika unaambiwa hayakuwa ndio yale, ilikuwa ule ni unga wa sembe. Huo si uwongo! Mimi ninasema serikali imefika wakati sasa wa kujituma kwa juhudi na maarifa na kutoa zawadi kwa wale maaskari wetu watakaofanya hili, kwani taifa linaangamia.

Mhe. Spika, jengine ni ukurasa wa 22 katika kifungu cha 40 kinachogusia mazingira. Mhe. Spika, ni vyema tukajielewa kwamba sisi chetu ni kisiwa na visiwa vimezungukwa na mzunguko wa bahari. Maji yale wenyewe kupiga na kurudi tu basi huwa mara nyingi yanakula kidogo kidogo ndivyo yalivyo. Na sisi wenyewe tumetayarisha mambo kwa ajili ya uchumi wetu, tunafanya uwekezaji.

Mhe. Spika, lakini pia tuna mashughuli mbadala, tunasema kwamba mawe na mchanga ni moja katika jambo ambalo linakuza uchumi wetu. Niliyasema mwaka jana, bajeti mbili ninasema na hii ninarudia kusema Ofisi yako Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mazingira yetu kwa hali hii tuliyonayo ya uchimbaji wa mchanga, ardhi yetu hasa sisi watu wa Kaskazini, wenzangu watu wa Kusini wana kifusi, mimi kama Kaskazini B mchanga.

Mhe. Spika, juzi tu baada ya mvua hii mafuriko kwenye mashimo yote yamejaa maji na tayari kijana wetu miaka 14 darasa la 7 amefariki. Na hayo ndio maafa lakini pia ndio uharibifu wa mazingira. Ardhi hiyo maji yake huwa hayakauki, inaweza kufika mwaka bado maji yapo. Ukipanda mti hapo ndio maana yake hauoti, hapo ndio haitumiki tena kwa kilimo, mashimo yameshaachwa. Maana yake alimuradi hali ipo hivyo.

Mhe. Spika, mimi ningeomba serikali ifanye tathmini ya maeneo haya ambayo yametumika kwa wakati huu. Yameshatumika kwa wakati huu kwa uchimbaji wa mchanga na mawe, waangalie mazingira yake yale yanaweza kutumika kutumika vipi na kuweza kuondoa tatizo hili.

Mhe. Spika, niende kwenye hii Idara ya Maafa. Mhe. Spika, ni bora kinga kuliko tiba. Ni vyema basi tukawa tunaandaa taratibu za kukinga zaidi na isiwe kama ile kwenda kutoa elimu na taaluma, lakini na kuviangalia vile vyombo ambavyo vinaweza vikasababisha hayo maafa. Serikali itupie macho badala ya kusema kwamba wizara husika tu kama meli labda, lakini kuna viboti vidogo vidogo, kuna majahazi, kuna vyombo vya uvuvi mbali mbali, kuna magari mengine hayafai kuchukua abiria. Ndio maafa hayo yakitokea na yatawakuta wananchi wetu. Taratibu hizi hazipo.

Mhe. Spika, maadam ana leseni kalipa, haya wewe nenda tu, sukuma huko. Ukaguzi wenyewe ni mtihani mtupu. Rushwa ndio maradhi yetu yaliyotutawala kwa wakati huu. Hatufiki na tutakuwa na walemavu wengi, maafa kadhaa na kisiwa chenyewe ni kidogo.

Mhe. Spika, sasa nije niseme kwamba serikali ninaipongeza kwa kutoa huu mfuko wa jimbo kuwapa hao wenye majimbo yao lakini na mimi nina malalamiko. Mhe. Spika, ninamuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais afikirie kwa kina kabisa juu ya mfuko huu kwa wanawake ambao wana asilimia kubwa ya wanawake kwani na wanaume kadhaa huwa tunawafikia na huwa tunawahudumia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, utakapotoa kwa hao wenye majimbo tu na sisi umetuita ni Wawakilishi, tuna maamuzi sawa na wao, si vyema na sisi ukatutenga katika hili, tunajisikia unyonge na kuona kwamba hukututendea haki mheshimiwa. Mhe. Hamza Hassan Juma anasema nigombee jimbo. Ni kweli ndivyo hivyo lakini ni mwakilishi na nina mafao sawa kama alivyo mwakilishi mwengine. Tena Katiba yetu ndio iliyosema habari hii ya kuwa na wanawake viti maalum na hatutumiki katika jimbo moja. Bahati nzuri sisi tunatumia ama wilaya au mkoa mzima, tena hatuchagui wanaume au wanawake, hatuchagui kama skuli au kituo cha afya, tunazihami jamii ambazo wanaume wengine wamezitelekeza hizo familia, hawana nafasi ya kwenda kwa wanaume, maana hawachezeleki sana ndio wanakuja kwetu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, ulione hilo yawezekana mimi sikuwepo hapa lakini wenzangu watakuja lakini waone kwamba na wao wanapata fursa hii ya mfuko huu kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wenzetu mbali mbali ambao wanaendeleza shughuli zao za kiuchumi, iwe ni rahisi kuwafikia. Kuna wanawake kadhaa hutufikia, watoto wao maskini, sare mbovu au wameshindwa ada ya skuli, wakifika kwetu kama mfuko huu tunao tutautumia na ninaahidi kwamba kwa kuwa sisi wanawake ni wa kweli na tuna uwezo wa kuufanyia marejesho kabisa kabisa.

Mhe. Spika, ninaiomba serikali ilione hilo, ilifikirie na hatimaye mutuibulie jibu ambalo na sisi twende sambamba na tujisikie sisi kama ni wawakilishi kama walivyo wa majimbo. (*Makofi*)
Mhe. Spika, sasa niseme kwamba Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais ndio yenyewe yenye kugusa shughuli za utaratibu wa mambo ya muungano...

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Ashura Sharif Ali: ...Mheshimiwa Spika, ahsante sana.Kama hivyo ndivyo kwamba ofisi yetu hii ndio inayogusa uratibu wa mambo ya muungano na hapa tulipo ni Zanzibar na Zanzibar ni mshirika katika ushirika huo wa Jamhuri ya Muungano, mimi ningependa labda Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais atakapokuja hapa atueleze katika mtengenezo huu wa Bunge la Katiba, yeye kama mdau kwa upande wa Zanzibar ambaye ni mtendaji

wa shughuli za serikali lakini pia ofisi yake yeye ndio inayoshughulika na mambo ya muungano, atwambie alituunganisha vipi sisi Wabunge wa Bunge la Katiba tukitoka hapa kwenda kule kukwamua kero za muugano ambazo ndio kikwazo kikubwa cha uchumi wa Zanzibar, ambapo ndio hilo tatizo, unaona vidole machoni, bajeti hazikutumia mambo hayakuwa.

Mhe. Spika, ninaomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais utakapokuja hapa utwambie kwamba sisi kama Zanzibar ni wadau wa muungano, sisi kama Wazanzibari ambao tumeungana kule na Tanganyika, Wajumbe wa Bunge la Katiba ulikaa nao vipi kuona kwamba kwa umoja wetu, kwa namna moja tunakwenda kule kwa maslahi ya Wazanzibari wote. Atakapofanya majumuisho Mhe. Spika, ninaomba nipatiwe jibu hilo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa baadae Mhe. Salmin Awadh Salmin wakati Mhe. Said Ali Mbarouk - Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo anajitayarisha.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii leo tukawa tupo pamoja hapa. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru na wewe pia kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa nianze kwa usemi ambao Mzee wangu Dkt. Salmin Amour Juma alikuwa mara nyingi anapenda kuutumia na mimi naomba leo kuukariri hapa. Dkt. Salmin Amour Juma alikuwa na maneno anasema, *"Khulqal insanu halua, idhaa massahu sharru jazu'a, waidhaa massahul-khayru manu'a, allal musaaliyn"*. Mhe. Spika, maneno haya yalikuwa na maana kwamba, "Nimemuumba mwanadamu kwamba ni kiumbe asiyefahamika, asiyetegemeka, asiyeeleweka, ukimpa mitihani utaona anavyohangaika lakini unapomjaalia heri anaing'ang'ania hataki imtoke". Sasa haya ndio maumbile yetu sisi wanadamu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nilikuwa ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza Ndugu yangu Ali Salim ambaye kwa siku ya leo alijitahidi sana kukisoma kitabu hiki na baadae akaweza kututolea takwimu kwa namna ambavyo mwenzetu aliwahi kuja kuzungumzia hapa. Nimejaribu kwenda ndani zaidi lakini kutokana na muda wenyewe kuwa mdogo na mambo ni mengi, nikaona kwa sababu hili limeshazungumzwa na limezungumzwa katika utaratibu ambao ndio, sitokuwa na haja tena ya kwenda kule katika hili buku.

Mhe. Spika, zaidi nilipata fursa ya kupitia *hansard*. Hii *hansard* ni hoja ile iliyokuja ikaletwa hapa na Mjumbe Mhe. Abubakary Khamis Bakar juu ya uanzishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, hoja hii ililetwa tarehe 28/01/2010.

Mhe. Spika, nitaomba kuna kipande kidogo nikariri ili niweze kuzungumza yale ambayo nilikuwa nimekusudia. Naomba kunukuu Mhe. Spika,

"Kwa maana hii sisi kwa pamoja bila ya kujali nafasi ya mtu, chama cha siasa anachotoka au itikadi aliyonayo hatuna budi kuwashukuru na kuwapongeza viongozi hao kwa hatua yao hiyo ya kijasiri na ya kizalendo na tuungane nao kwa pamoja kama ni Wazanzibari tunaoipenda nchi yetu kwa maslahi ya Zanzibar na watu wake kwa maendeleo ya Zanzibar yetu na Tanzania kwa ujumla"

Mhe. Spika, *paragraph* ya pili, "Kuna haja pia sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tukiwa ni Wawakilishi halali wa wananchi wa Zanzibar kuchukua hatua madhubuti na ya kihistoria kwa lengo la kuyapa nguvu maridhiano hayo, kwa lengo la kustawisha umoja na mshikamano miongoni mwa Wazanzibari na kujenga misingi imara ya amani na utulivu wa kudumu hapa Zanzibar".

Mhe. Spika, lakini *paragraph* ya mwisho inasema kwamba, "Ninaamini kwa dhati kwamba tukiwaacha fursa hii ya kihistoria bila ya kuchukua hatua ya kutilia nguvu na kujenga misingi madhubuti, upo uwezekano mkubwa wa hali ya kisiasa kurejea kule tulikotoka na hivyo kuendelea kuiathiri nchi yetu kijamii, kiuchumi, kisiasa au hata watu kupoteza maisha yao pamoja na mali zao au vyenginevyo hali ya Zanzibar kiamani kuvurugika, umoja kukosekana, uzalendo kupotea na hivyo kuwapa mwanya maadui zetu kutugawa, kututawala na kufanya watakavyo katika nchi yetu sisi wenyewe".

Mhe. Spika, nilikuwa ninayakariri haya, nilitaka kuunganisha na uhalisia wa Wajumbe ambao walianza kuchangia mada mbali mbali juu ya uhalisia wa hali ya kisiasa ndani ya Zanzibar yetu. Mhe. Spika, ni muda mfupi tu uliopita ndani ya Zanzibar yetu hapa tulikuwa na matukio mazito, magumu na yenye kuhatarisha na kudhalilisha maisha na amani katika nchi yetu.

Mhe. Spika, tukiangalia misingi ya kuanzishwa kwa hoja hii ya kuleta Serikali ya Umoja wa Kitaifa, haikuwa na maana hoja hii kwamba watu katika Zanzibar waweze kuishi katika maisha ya hofu, maisha ya kutokuaminiana, maisha ya kuharibu umoja na mshikamano, bali tulikuwa na malengo ya kuleta umoja, mshikamano, maelewano na vile vile kuweza kuisaidia nchi yetu iweze kwenda vizuri.

Mhe. Spika, cha kusikitisha sasa kipindi kifupi kilichopita Zanzibar yetu tulikuwa na kundi hili la UAMSHO, kundi ambalo Mhe. Spika, mambo yake sina haja ya kuyakariri tena hapa, lakini tulifika pahala kila mmoja akawa hana amani na usingizi wake wala maisha yake ndani ya Zanzibar yetu. Lakini haya hayakuwa malengo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Malengo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa tuwe na umoja, tuwe na utulivu na tuwe na mshikamano. Lakini kama hiyo haitoshi, kukawa na utaratibu wa kumwagiana tindikali, ambapo jambo hili lilikuwa linahuzunisha sana, kwa sababu yalikuwa yanaelekea upande fulani wa chama bila upande mwengine kutokuona athari za namna kama hii.

Mambo haya na mambo mengine ambayo yalitokezea ndani ya Zanzibar, ndio yaliyopelekea mpaka kufikia pahala wananchi na wanachama wa chama fulani kuona kwamba sasa wamekithirihishwa, sasa wamechoshwa na sasa wanaona kwamba kumbe hii sababu ya kuleta Serikali ya Umoja wa Kitaifa haikuwa na maana kama ambavyo tulikuwa tumezungumza kwenye waraka huu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nayazungumza haya katika kuthibitisha kwamba lile suala ambalo lilikuwa limezungumzwa hapa, la kwamba iko haja ya kuja na hoja binafsi kuja kuzungumzia suala la Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa, sio suala ambalo linapingwa na mwana makubaliano ambayo yalikuwa yamepita katika *hansard* hii.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja katika suala zima la uwajibikaji na utawala bora ndani ya nchi yetu. Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba pahala popote pale kwenye maeneo ya watendea kazi au wafanyakazi, kuna vigezo vinachukuliwa ili mtu aweze kuwa ni mfanyakazi bora au mfanyakazi makini ambaye anaweza kuendelea na shughuli zake za kiutendaji siku hadi siku, hata kama muda wake wa kazi unakwisha basi mtu yule anaongezewa muda na kuweza kufanya kazi katika utaratibu ambao tumejiwekea.

Mhe. Spika, nimesikitishwa sana kuona kwamba baadhi yetu tunapofika hapa tunazungumzia suala zima la kukosa imani na watendaji ndani ya secretariat ya Tume ya Uchaguzi. Mhe. Spika, watendaji hawa ndio waliofanya kazi nzuri na makini hadi leo hii tukaweza kufikia hapa tulipo na tukawa tunaishi kwa amani na utulivu katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Kama hayo hayatoshi, hawa watendaji katika secretariat ambayo ilikuwa inazungumzwa, ni watu ambao wanafanya mambo ambayo wanakuwa wanapewa na kukabidhiwa na wale makamishna pamoja na viongozi ambao wapo katika maofisi ambayo yanahusika. Sasa leo kuja hapa tukaanza kuwashutumu kwamba watendaji hawafai, hawana maana, naona ni kuwakosesha haki watu hawa na kutokuwatendea mema. Kwa sababu wao hawana nafasi ya kuweza kuja katika chombo kama hiki na kuzungumza kwa namna ambavyo walikuwa wanazungumza, kwa namna ambavyo ilikuwa sio.

Mhe. Spika, kuna waliotangulia vile vile walikuwa wakizungumzia suala la ubaguzi. Kuna mjumbe mwenzetu hapa ambaye alizungumzia suala zima la kusema kwamba Zanzibar ndiko kumefanywa Mapinduzi, lakini Pemba hakukufanyika Mapinduzi, isipokuwa watu wanalipana fadhila. Lakini kuna mwengine akajitokeza kuzungumzia suala zima la kwamba tunanyanyasana, kana kwamba kundi fulani ni bora na kundi jengine sio bora. Mimi suala hili naliona halina msingi wowote Mhe. Spika, kwa sababu kama ikibidi kuna suala la unyanyasaji, kama ikibidi kuna suala la kubaguana basi upande mwengine unafanya shughuli hizi kwa uwazi zaidi na kwa namna ambavyo kila mtu anatulia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hawa ambao watakuwa wamekuja hapa na kuzungumzia kwamba Zanzibar kuna ubaguzi, kuna majimbo ambayo yanaongozwa na watu wa chama hiki ndani ya Unguja hii hii, lakini hakuna majimbo ambayo yanaongozwa na chama cha watu wengine kwa upande wa Pemba vile vile. Je, kule hakuna wana CCM?

Sasa naomba Mhe. Spika, hoja kama hizi zinapokuja tuziangalie kwa makini na tusizungumze vitu vya kusababisha watu kuweza kuwa na mifarakano na vile vile kuzungumza lugha za uchochezi, ili watu wetu watuelewe katika namna ambayo sivyo ambavyo tulivyo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nakwenda katika suala zima la vijana wetu 17 ambao walikuwa wamechukuliwa na kupelekwa Chuo kile cha Diplomansia pale Dar es Salaam kwa ajili ya kuwa katika orodha ya watu ambao walikuwa wanasubiri kupatiwa nafasi ya kazi katika Wizara ya Mambo ya Nje. Ningeomba Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais atakapokuja hapa anisaidie, suala la vijana hawa 17 mpaka sasa hivi limefikia hatua gani, ili tuweze kufahamu hasa ni kitu gani kilichopo vijana hawa mpaka leo wakawa hawajaajiriwa na sasa hivi ni mwaka wa tatu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo, mimi niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuiondosha ile Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Kiserikali pale Dar es Salaam, katika Wizara ya Fedha na kuipeleka katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, mimi matarajio yangu, kitendo cha kuiondosha ofisi hii katika Ofisi ya Wizara ya Fedha na kuipeleka katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni kuweza kuwaenzi, kuwatunza na kuwasaidia viongozi wetu wa kiserikali ambao wanaondoka Zanzibar na kwenda upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano katika shughuli zao za kikazi.

Mhe. Spika, nimesikitishwa sana na kiwango cha bajeti ambacho kimewekwa katika wizara hii. Katika wizara hii Mhe. Spika, kumeombwa pesa shilingi milioni 353,178,160. Ukiangalia fedha hii shilingi milioni 208,178,160 ni mshahara, lakini shilingi milioni 145,000 hizi zinakuja katika matumizi mengineyo. Sasa ukiangalia umuhimu wa ofisi hii na fedha ambazo zimekwenda na kazi ambazo zinatarajiwa kufanywa katika ofisi hii na namna ambavyo ofisi hii tumeiondosha Wizara ya Fedha, ili viongozi wa Serikali ya Mapinduzi wanaotoka Zanzibar kwenda upande wa pili wa Muungano waweze kuitumia ofisi hii kwa shughuli hizi ni ndogo sana na hazitoshi.

Napenda kuchukua fursa hii Mhe. Spika, kumuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maelekezo ya namna gani wataweza kuhaulisha baadhi ya vifungu katika vifungu ndani ya wizara yake, ili fungu hili litononoke na angalau basi liweze kufikia angalau milioni 500 na kidogo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, ningependa kufahamisha kwamba katika ofisi hii vile vile hapana hata gari ya kuweza kufanyia shughuli zao. Ningeomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, wafanye utaratibu wa kuangalia mafungu yao ili iwezekane kupatikana angalau kijigari basi cha kuweza kuwepo pale na kuendelea na shughuli zao, ili shughuli za ofisi hii ziweze kwenda vizuri.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nilitaka kuingia katika vifungu, lakini baada ya kupata baadhi ya wajumbe wakanifahamisha kwamba kulikuwa kuna makoseo ambayo tayari yamekwisha kurekebishwa, naomba suala hili niliwache na zile taratibu zilizopo ili ziweze kuendelezwa vizuri.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni tunakubaliana na tunaunga mkono hotuba hii ya bajeti ya Makadirio na Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Salmin Awadh Salmin wakati Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo anajitayarisha na Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya na yeye pia anajitayarisha. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya dakika 20 na mimi nikaweza kuchangia hotuba hii muhimu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, sikutaka kuchangia katika hotuba hizi; ile ya kwanza na hata hii ya pili, kutokana na hali ya afya yangu mafua na kadhalika. Lakini nimelazimika niseme baada ya kutajwa sana tokea ile hotuba ya kwanza ya bajeti, lakini

hata hotuba hii nayo nimetajwa sana. Kwa hivyo, nimeona sio vyema nikanyamaza kimpya, kwa sababu nahitaji kutoa baadhi ya maelezo juu ya kutajwa tajwa kwangu.

Kabla ya hayo nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi katika ofisi yake. Kwa hivyo, bahati nzuri mwaka huu amewasilisha mwenyewe, hakutumwa mtoto. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hotuba hii imezungumzia mambo mengi, lakini mimi nitatumia nafasi hii kuzungumzia baadhi ya mambo tu ambayo pengine kwa upande wangu nimeona niyazungumzie.

La kwanza kabisa nitazungumzia juu ya suala la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, mimi niipongeze sana Tume ya Uchaguzi, hususan Secretariat ya Tume ya Uchaguzi. Kwa kweli Mhe. Spika, Secretariat ya Tume ya Uchaguzi imekuwa ikifanya kazi vizuri sana na kwa sababu secretariat ile inaongozwa na Tume ya Uchaguzi, lakini inaongozwa na taratibu za kisheria na miongozo mbali mbali. Kwa hivyo, tuwapongeze sana wanafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Hamad hapa ameivuruga sana Tume na hasa secretariat, Mhe. Hamad Masoud Hamad kasema haifai imekaa muda mrefu sana. Lakini mimi ningeshangaa sana kama mpinzani akaisifu Tume ya Uchaguzi, au secretariat ya Tume ya Uchaguzi. Hata siku moja haiwezi kutokea duniani. Mpinzani vyombo kama vile ni lazima aviponde, avione havina maana na huo ndio upinzani na ningeshangaa sana kwamba angeisifu secretariat ya Tume ya Uchaguzi. Hiyo ndio kawaida ya wapinzani popote na hasa katika nchi za Afrika. Kwa hivyo, wenzetu hawa wanafanyakazi vizuri na wanafanyakazi katika mazingira magumu na tunastahiki tuwapongeze sana.

Kinachoonekana ni kwamba kumeshakuwa na dalili za kuwaingilia ingilia, Baraza hili kuanza kuwaingilia ingilia katika majukumu yao. Sio vyema hata katiba yetu haielekezi hivyo. Vyombo hivi vinatakiwa viwe huru, vifanyekazi kwa uhuru bila kuingiliwa na wanasiasa. Sasa leo mtakapowaambia kwamba eneo fulani msifanye hivi, huko ni kukiingilia chombo hiki. Lakini pia kuna lugha za vitisho juu ya secretariat. Mimi nawaambia secretariat, fanyeni kazi yenu vizuri, mjiamini na mnafanyakazi vizuri na msibabaishwe na vitisho vya mtu yeyote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba moja kati ya jukumu la Tume ya Uchaguzi ni kuyagawa majimbo, kukata majimbo pale inapostahiki. Haiwezekani jimbo moja la uchaguzi lina watu 200 au 2,000 jengine lina watu 20,000, haiwezekani. Kama watu wanatoka sehemu moja ya makaazi wanavamia katika maeneo mengine, kwa hivyo majimbo yao yatatoka kule yatakuja huku waliko na kama hawataki majimbo yale basi wabakie kule waliko. *(Makofi)*

Unatoka Pemba unakuja Fuoni unahamia huku, unavamia katika majimbo ya Zanzibar, halafu munataka majimbo kule yasipunguzwe yabakie vile yalivyo, yatawezekana hayo? Tume ya Uchaguzi fanyeni kazi yenu vizuri, angalieni sensa ya watu, angalieni maboresho ya daftari na mtumie vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria, serikali iko pamoja na nyingi na wananchi wako pamoja na nyinyi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nije eneo jengine la Maadhimisho ya Sherehe za miaka 50. Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais imezungumzia juu ya maadhimisho ya Sherehe ya miaka 50. Sisi Mhe. Waziri tunakupongeza sana, tunampongeza Mhe. Rais Dkt. Shein pamoja na watendaji wote wa serikali, kwa kufanikisha Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kweli zimefana sana na kila mmoja ameridhika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mfululizo wa sherehe zile serikali inajenga mnara wa kumbukumbu za Mapinduzi. Mimi nipongeze sana juu ya juhudi za serikali ya kujenga ule mnara, mnara ambao sasa hivi unaendelea kujengwa. Nchi zote duniani Mhe. Spika, zinakuwa na kumbukumbu juu ya mambo yao makubwa. Mapinduzi ni jambo kubwa sana kwa Wazanzibari. Kwa hivyo, ni vyema ukajengwa mnara wa kisasa na taarifa humu imeturidhisha na matumizi ya mnara ule yameturidhisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimeshangwazwa na kitu kimoja. Juzi wakati wa bajeti ya Mhe. Waziri Mkuu, alikuwepo mbunge mmoja akichangia hotuba ya Waziri Mkuu. Alisema kwamba mnara wa kumbukumbu ya Mapinduzi umejengwa kwa pesa za *CDF* za Wabunge, kwa kweli kauli ile imenisikitisha sana na mbunge yule anaitwa Khatib ni Mbunge wa Jimbo la Konde nilivyoambiwa. Alijaribu kuitumia fursa ile kuponda sana Serikali ya Mapinduzi pamoja na Mapinduzi, kusema Serikali ya Mapinduzi ni wezi wameiba fedha za wabunge za mfuko wa *CDF*. Akathubutu

kuendelea kusema kwamba bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ni sawa sawa na imeshindwa na bajeti ya Kampuni ya AZAM. Kwa kweli nimesikitishwa sana na kauli zile za Mzanzibari, japokuwa anaishi Tanga, lakini yule ni Mzanzibari na ni Mbunge wa Konde, anathubutu kukejeli Mapinduzi ya Zanzibar na serikali yake na kusema ni wezi, kwa kweli imenisikitisha.

Hata hivyo leo nimefarajika kuona kwamba kumbe fedha zinazojenga mnara ule ni fedha za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *ZSSF*. Lakini nimeshangazwa sana na kauli ile ya mbunge, kasahau kwamba fedha zile zimetoka katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huu Muungano ndio ule mbaya. Leo anapiga kelele kwamba anazitaka pesa kwa ajili ya kwenda kufanyia maendeleo katika Jimbo la Konde, ama kumbe kweli 'baniani mbaya kiatu chake dawa'. *(Makofi)*

Mhe. Spika, fedha zile zimetoka katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na zimeletwa Zanzibar katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar. Fedha zile sio za wabunge, fedha zile kwa ajili ya maendeleo ya Wazanzibari sasa kama fedha zile zingekuwa ni zake.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Mjumbe samahani kidogo nimeombwa na vijana wetu watu wa mitambo kwamba tukipiga sana *mic* hizi tunazipunguzia nguvu, moja lakini la pili tunapopiga mayowe sana huyu Mheshimiwa Mjumbe hatumsikii vyema kwa sababu ya hiyo *eco* ambayo imetatiza kwa muda mrefu, tupige makofi kwa utaratibu ili Mheshimiwa Mjumbe tumsikie na wananchi wasikie vizuri. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mheshimiwa Spika, zote ni furaha hizo kwa hivyo watu wanapofurahi wanakuwa wanahamasika, mimi nataka kumwambia Mbunge yule wa Konde kwamba fedha zile zilizotoka kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar si fedha zake, na kama zingekuwa za kwake angeingiziwa kwenye account yake, kwa hivyo kama fedha zile zimetoka kwenye Jamhuri ya Muungano zimekuja Zanzibar zitatolewa wakati wake muafaka utakapofika kwa ajili ya maendeleo ya watu. Haya ndio yale tunayosema kwamba wenzetu hawa hawana nia safi juu ya Mapinduzi ya Zanzibar, huwezi ku- *create* ambacho kinabughudhi Serikali yako na mambo yake anayoyafanya, huwezi kusema eti fedha za CDF zimekuja kujengewa mnara wa Mapinduzi maana yake ni kupinga Mapinduzi yale ndio tafsiri yake hiyo, sisi ndio tunavyotafsiri. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nimefarijika sana kuona mnara ule ujengwe na utaendelea kujengwa na kumbe fedha zinazojengewa sio zile za CDF kile ni kijungujiko tu cha CDF fedha halisi zimetoka katika mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya ZSSF Zanzibar, na tunautakia heri mnara ule ujengwe na ikifika siku uje uzinduliwe.

Jengine nililotaka kulizungumzia juu ya suala lile ambalo nimesema mumenilazimisha niseme, pamoja na kuwa pakizungumzwa sana hapa juu ya hoja binafsi ambayo inategemewa kuwasilishwa hivi karibuni katika chombo hiki. Mimi nimeshangazwa na maneno yanayosemwa sana ya kuhimiza hoja iletwe isiletwe hoja hivi hoja hivi, kwa nini tunahimiza hii wakati wake ukifika itakuja tu na suala la kuwasilisha hoja katika chombo hiki ni suala la kikanuni tu. Mjumbe yoyote anayo haki ya kuwasilisha hoja juu ya jambo ambalo mwenyewe analihisi linahitaji kujadiliwa na kuamuliwa. Hili ni suala la kikanuni Mjumbe yoyote anayo haki ya kuwasilisha kama Mheshimiwa Hija alivyosema anataka kuwasilisha hoja ya kuuliza uhalali wa muungano, mwache awasilishe tutajadili hapa, wajumbe watapiga kura waliokuwa wengi wataipitisha, waliokuwa wachache watabakia, tuna wasi wasi wa nini?

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Serikali hii ya umoja wa kitaifa nayo iliwekwa kwa hoja Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari aliwasilisha hoja binafsi ndani ya Baraza la Wawakilishi lile lililopita, kwa bahati na mimi nilikuwa mjumbe. Aliwasilisha hoja akatoa *concern* zake, akaeleza faida zake, akaeleza mafanikio yatakayoweza kupatikana akajaribu kutu- *convince* Mhe. Spika, halikuwa jambo rahisi kuwa- *convince* wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM kukubaliana juu ya jambo lile, haikuwa rahisi. Lakini kwa bahati nzuri sana wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM waliunga mkono hoja ile. *(Makofi)*

Mjumbe wa mwanzo kuchangia hoja ile na kuiunga mkono ni Mhe. Ramadhani Abdalla Shaabani wakati ule akiwa ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa mpaka leo, na mjumbe wa pili kuunga mkono alikuwa ni Samia Suluhu Hassan alikuwa ni Mjumbe wa Kamati kuu kwa wakati ule na wajumbe wengine ambao humu wamo na wengine wametoka. Mhe. Ali Mzee Ali, Mhe. Suwaibah Edington Kisasi, Mhe. Mahamoud Thabit Kombo na Waheshimiwa wengine nimejaribu kupitia *Hansard*. Ni wajumbe wa Chama cha Mapinduzi ndio waliounga mkono juu ya hoja ile.

Sasa mimi nadhani wenzetu wajiulize kulikoni, wajiulize wanatakiwa wakae watafakari kwa nini Wajumbe hawa hawa wa Chama cha Mapinduzi waliunga mkono hoja hii kwa pamoja leo wanataka kuleta hoja ya kutaka kupinga juu ya jambo hili, lazima ujiulize kama binaadamu. Mhe. Spika, wamekuwa wakisifiwa sana hapa na mimi nawasifiya Shehe Abeid Amani Karume Rais wa awamu ya sita pamoja na maalim Seif Sharif Hamad kwa mazungumzo yao, wakatuletea maridhiano, leo tupo kwenye serikali ya umoja wa kitaifa. Lakini wanasahau kwamba maridhiano yale ni sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuloyajadili na tukayapitisha, Rais Karume hakuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Maalim Seif hakuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini ni sisi tuliojadili hoja ile na kwa umoja wetu tukaikubali na tulikuwa na sababu za kuikubali, lakini tujiulize hivi zile sababu za kuikubali hazipo tena?

Mhe. Spika, wajumbe wengi wamekuwa wakihubiri hasa wa upinzani kwamba amani na utulivu vitatoweka, amani haipo, umoja na mshikamano haupo kwani sasa hivi ipo katika Serikali hii ya umoja wa kitaifa mshikamano na umoja upo wengine wanathubutu kusema tunachezea shilingi chooni, maana yake tunachezea shilingi chooni ndugu yangu Subeti pale lakini vyoo anavyovisema ni vile vyoo vya kizamani siku hizi vyoo ni vya flashi. Shilingi ikitumbukia kwenye flashi unaitoa, unaikosha unakwenda zako kuitumia sio ile shilingi ya zamani ikitumbukia huipati tena. Siku hizi tunatumia vyoo vya flash, shilingi ikitumbukia unaitoa unaikosha, unakwenda nayo sokoni.*(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Spika, nadhani wenzetu wanazungumzia amani na utulivu mdomoni lakini ndani ya nafsi zao haziko safi, wakati tukijadili suala hili mimi Mhe. Spika, nilikuwa na mashaka makubwa juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na nilikuwa na wasi wasi mkubwa na nilikuwa nausema kwenye vikao mbali mbali vya chama na nilikuwa nasema hawa hawaaminiki, wanayoyasema sio wanayoyatenda lakini tumejaribu kuwa-*convince* tukakubaliana hatimae sote kwa kauli moja tukakubaliana Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, hoja ya Mheshimiwa Abubakar iliungwa mkono kwa asilimia mia moja na wawakilishi wote waliokuwemo mule. Lakini kwa kweli na kwa kuwa wenzetu hawakuwa na nia safi juu ya jambo lile, kwa kweli tumekuwa tunakwenda katika matatizo makubwa tusiyoyatarajia. *(Makofi)*

Mimi nataka niwaulize Waheshimiwa Wajumbe wanaozuangumzia amani na utulivu katika nchi hii, hivi hakuna watu waliouwawa katika kipindi hiki cha Serikali ya Umoja wa Kitaifa? Kifo cha Padri Mushi kimetokana na nini? Kisa cha Padri Kendwa kupigwa risasi kinatokana na nini na wakati gani.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika 5.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Kitendo cha Askari polisi kukatwa kichwa pale Bububu kimetokana na nini, watu kutiwa tindikali watu mbali mbali, Mashehe, watu wasiokuwa na hatia kutiwa tindikali inatokana na nini? Makanisa kuchomwa moto imetokana na nini? Nyumba za ibada kutiwa moto imetokana na nini? Watu kuharibiwa mali zao imetokana na nini? Matawi ya CCM kuchomwa moto imetokana na nini? Maskani za CCM kutiwa moto imetokana na nini? Mbona hatujashuhudia tawi la CUF hata moja kuchomwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo vitendo vilivyofanyika kabla ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na vitendo vilivyofanywa ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa havina tofauti ndio vile vile, kwa hivyo ndugu zangu, ndugu viongozi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi haja ya kuwauliza wananchi ipo. Kwa sababu sisi ndio tuliokwenda kuwawarubuni watu na tukawaambia kwamba wakubali na sisi wenyewe tukakubali na tukawaambia kwamba wakubali na sisi wenyewe tukakubali. Kwa hivyo kurejea kwa wananchi kuwauliza na hili suala la kufanya tathmini ni suala la kawaida. Unapofanya jambo lazima ufike pahala ufanye tathmini, hivi hii tathmini ya Serikali hii kwa muda wa miaka mitano tunaogopa nini, asilimia 66% ilisema ndio, asilimia 34% ilisema hapana naamini kama jambo hili litakuwa limefanywa vizuri basi sasa asilimia ya ndio itakuwa zaidi kuliko iliyokuwa mwanzo. Lakini kama tumekwenda vibaya basi asilimia ya hapana itakuwa zaidi tutarejea kule tunakotoka *(Makofi).*

Mhe. Spika, wenzetu wasiwe na wasi wasi tunafanya tathmini kuona kipindi cha miaka mitano. Kesho kutwa tunamaliza kama tumekwenda vizuri wananchi watasema ndio, kama tunakwenda vibaya watasema hapana na wakisema ndio maana yake tutaendelea nayo, wakisema hapana maana yake ndio hapana.

Kwa sababu Mhe. Spika, kwa mujibu wa katiba hii ya Zanzibar ibara ya tisa inazungumzia juu ya mamlaka ya wananchi juu ya Serikali yao; wao ndio wenye kauli juu ya namna gani Serikali hii iwe, kwa hivyo twendeni

tukawaulize kama tulivyowauliza mwanzo, sasa miaka mitano tunakaribia kumaliza wameridhika watakubali, hawajaridhika juu ya vitendo vinavyoendelea watakataa.

Kwa hivyo hatuna haja ya kuwa na mchecheto, hatuna haja ya kuwa na hofu juu ya jambo hili, tutulie suala la hoja ni suala la kikanuni mtu yeyote ana haki ya kuwasilisha hoja, hoja hii ikikubaliwa na bahati tunashukuru Wajumbe wa CCM humu ndio wengi kuliko wale wa upinzani, wajumbe wa CCM tupo 49 wajumbe wa Upinzani wapo 33 ninauhakika wa hoja hii ikija hapa itapita haina mashaka. Tuna uhakika kwa sababu chama kinachotawala ndicho chenye wajumbe wengi tutapitisha hoja hii.*(Makofi).*

Mhe. Rais akikubali kwamba twende kwenye *referendum* tutakwenda kwenye *referendum* kwani tatizo liko wapi. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru sana na naomba Waheshimiwa wajumbe wenzetu wawe wastahamilivu, watulie mambo mazuri yanakuja. Ahsante Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kati ya baadhi ya mambo ambayo tulikubaliana tusiyalete humu ndani leo sehemu kidogo nimeiona. Mheshimiwa nakuomba sana pale tulipokuwa kwenye Bunge la Katiba tulikuwa tunapiga makofi kwa kunyanyuka na leo nimeyaona humu ndani, sasa ni katika mambo ambayo tulikubaliana katika vikao vyetu vya awali vya matayarisho kamati ya uongozi kwenye *vetting* kwamba vitu vya aina hii hebu tujaribu kuepuka navyo na ndio maana kwa kifupi pale ndio tukasema kwamba kama kuna jambo limetufurahisha tupige makofi kwa utaratibu, kama kuna jambo lililoudhi liliyemuudhi atataja taratibu za kanuni, ili aliyeudhi aweze kufuta usemi wake.

Sasa naendelea kufahamisha tu kwamba hili ni Baraza la Wawakilishi, nia na madhumuni tutoke humu ndani bado tukiendelea kuwa wamoja, iwe ndio uongozi kwa wananchi wetu tunaowaongoza. Sasa tumejaribu kuepuka mambo ambayo hayatatufikisha pahala. Mheshimiwa Mjumbe kaelezea hoja yake kwa namna anavyoiona inavyoelekea, kuna wengine wamevutiwa na hoja hiyo na kuna wengine pengine hawakuvutiwa na hoja hiyo, na hiyo ndio demokrasia ya vyombo hivi. kwa hivyo tustahamiliane. Lakini hatimae tufike pahala ambapo tunakusudia kwenda. Kama muda ungekuwa umebakia kidogo ningesema basi tumalize kwa leo mjadala huu, lakini kwa kuwa kuna dakika kidogo na tayari nimekwisha wataja Waheshimiwa wawili waliokuwa wanataka kusaidia hoja hii, basi tuendelee kuwasikiliza ambayo nafasi ya kwanza itakuwa kwa Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo na baadae Mhe. Dk Sira Ubwa Mamboya Naibu Waziri wa Afya.

TAARIFA

Mhe.Hamad Masoud Hamad: Mimi taarifa yangu ni kufanya *clarification* ili baraza hili lisipotoshwe. Mamlaka ya Baraza hili ni kujadili chochote na kuisimamia Serikali, kuihoji Serikali na humu hatutakiwi tujadili jambo ambalo liko Mahakamani. Kwa hivyo si Tume ya Uchaguzi, sio Ofisi ya Rais chochote kilichoko Serikalini tuna wajibu wa kulijadili hapa, kwa hivyo si haki kusema kwamba Tume ya Uchaguzi secretariat isiguswe, ni watendaji wa serikali tuna haki ya kuwahoji na kuna siku hapa inshaallah kila mmoja tutamtolea alivyo wazi wazi ,tunaisimamia serikali utendaji wake. Lakini la pili Mheshimiwa katika Baraza hili hakuna *opposition*...

Mhe. Spika: Mheshimiwa Hamad hii si taarifa. Hii unaanza kujibu hoja, weye uliposema kwamba tume ile haifai wenzako walinyamaza kimya, kuna wengine wamesema inafaa na wewe unyamaze kimya. Ukiona umejibiwa na wewe unataka kujibu tunaharibu mjadala wetu na demokrasia, kwa hivyo hapo ulipofikia iwe basi namruhusu Mheshimiwa Waziri ili atoe maoni yake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake nzuri na kwa namna ambavyo alivyowasilisha katika Baraza lako tukufu, mzee bado yuko makini na nguvu nyingi, *speed* yake ilikuwa safi kabisa.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 5 wa hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alizungumzia maadhimisho ya sherehe ya miaka 50 ya Mapinduzi yetu. Nami nakubaliana sana na Mhe. Makamu wa Pili ya kwamba tunapaswa kujipongeza kwa hatua tuliyofikia lakini zaidi kwa namna ambavyo wazanzibari sote kabisa tulishirikiana katika sherehe ile. Ni moja katika sherehe ambazo kwa kumbukumbu zangu wananchi wote bila ya kujali itikadi zao za vyama, bila kujali mambo mengine kwa pamoja Mhe. Spika, tuliadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi yetu, jambo moja muhimu sana.

Kwa hivyo hili nami naomba sana nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa sababu yeye ndie aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sherehe na Maadhimisho. Kwa hivyo kazi yake aliifanya vizuri na ndio maana wananchi wote wa Zanzibar wakashirikiana kwa pamoja. Ombi langu ni kwamba mambo kama haya ya kinchi yakitokea, basi tuache mambo yetu ya itikadi na mambo mengine tupate nafasi ya kushereheka kwa pamoja, kama zuri na kama baya au msiba tuhuzunike kwa pamoja ndio jambo zuri.

Mhe. Spika, katika madhimisho yale Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tulipewa majukumu mawili makubwa. La kwanza ilikuwa kazi ya kukarabati uwanja wa amani ili ubebe hadhi ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi. Ninafurahi kwamba kwa msaada wa viongozi wakuu wa kitaifa Mhe. Rais mwenyewe, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kazi ile ilifanikiwa na ndio maana timu yako kabambe ya Baraza la Wawakilishi ilikuwa ya mwanzo kuonja mafanikio yale.

Jambo la pili Mhe. Spika, tulilopewa ni kuamsha vuguvugu la michezo yote nchini ikiwa ni pamoja na kuzialika timu kutoka nje. Naomba nifurahi kwamba klabu mbali mbali za michezo *takribn* yote zilishajiika na zilishiriki vizuri sana, mjini na mashamba. Kwa kweli kwa kiwango kikubwa zilipamba ile sherehe yenyewe, michezo yote takriban imefanyika vizuri na wananchi wengi mbali mbali waliweza kutusaidia katika kuhakikisha kwamba michezo nchini inachezwa vizuri, tunawapongeza sana. Mfano mzuri ni Kampuni ya Said Salim Bakhresa, kwa kweli alifanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba anasafirisha wanamichezo kutoka Bara - Unguja, Unguja - Pemba. Kafanya kazi moja nzuri.

Mhe. Spika, miongoni mwa wananchi wazalendo ambao Wizara yangu ilitegemea kupata msaada wake mkubwa ni Mhe. Raza. Mhe. Raza ni mzalendo sana na mpenzi mkubwa wa michezo. Sasa kwa nafasi yake tulidhani kwamba tutapata msaada wake mkubwa. Huko nyuma aliwahi kuchaguliwa na Wizara kuwa Mwenyekiti wa Kombe la Mapinduzi *Cup*, kazi aliifanya vizuri na ndio maana Mhe. Rais akaagiza kwamba Kamati ile ambayo Mhe. Raza alikuwa anaiongoza iendelee kuhakikisha kwamba inasimamia Mapinduzi *Cup* ya miaka 50 ya Mapinduzi.

Sasa mimi ninasikitika sana kwamba hili Mhe. Raza alisusia neno hilo, pamoja na agizo la Mhe. Rais hili la Mhe. Raza la kuisimamia Kamati ya Mapinduzi *Cup* kwa kweli alijitenga nayo ndio ukweli wenyewe. Sasa hili ni jambo ambalo sisi Wizara lilitusikitisha sana, niwapongeze sana wajumbe wengine waliobakia ambao kwa kweli walifanya kazi moja kubwa sana kuhakikisha kwamba jukumu lile linafanikiwa. Na kwa kweli walifanya kazi kubwa sana bila ya malipo kwa kujituma vizuri kuhakikisha kwamba mashindano yale yanakwenda vizuri na kwa mara ya mwanzo tulipata timu nyingi kutoka nje ya nchi yetu. Kwa mara ya mwanzo timu zile zilikwenda hadi Pemba kuhakikisha kwamba uwanja wa Gombani wananchi wa Pemba wanapata nafasi ya kuziona timu kutoka nje.

Miongoni mwa watu ambao wanapaswa kupongezwa sana ni bibi Sherry ambaye alikaimu nafasi ya Mhe. Raza kuona kwamba shughuli zile zinafanyika vizuri. Ni mama mmoja ambaye kwa kweli alifanya kazi kubwa sana.

Sasa Mhe. Spika, baada shughuli yetu kumaliza ghafla katika vyombo vya habari siku moja ninasikia kwamba Wizara ya Habari inadaiwa milioni sabiini. Siku ya pili Mhe. Raza kanifuata ofisini bwana; kama jana tayari keshaitisha mkutano wa vyombo vya habari kueleza hili siku ya pili ndio ananambia bwana ninadai shilingi milioni sabiini, lazima ulipwe. Nikamuuliza Mheshimiwa zinatoka wapi? Aa niliikopesha Wizara. Una *supporting document?* Sina. Sasa Mhe. Raza wewe unakopesha vespa tu hapa mtu anachukua mikataba mpaka benki ya kiislamu, leo unakopesha milioni 70 huna *supporting document*, mimi nitalipaje?

Sasa tatizo langu ni kwamba mimi kama Waziri wa Habari sina kumbukumbu yoyote kwamba Mhe. Raza alitukopesha shilingi milioni 70. Na kwa utaratibu wa shughuli za serikali huwezi kutengeneza *voucher* na ukatoa *cheque* bila kuhakikisha kwamba kuna *supporting document*, hiyo itakuwa ni *forgery* na Mdhibiti na Mhasibu Mkuu wa Serikali anaweza kufanya *query* na Kamati ya PAC hili nalo litakuwa ni jambo ambalo watakuja kunikalia mimi juu ya utosi. Sasa mimi sikumbuki kwamba alinikopesha lakini kama ana *supporting document* yoyote ambayo Mhe. Raza anaidai Wizara ya Habari basi hatuna tatizo, lakini sikumbuki na katika hali halisi ya mambo yanavyokwenda serikalini, haijafikia pahali kwamba nikwame mpaka nende nikakope kwa Mhe. Raza.

Mhe. Rais wa Zanzibar yuko makini sana katika hilo si mara moja, si mara mbili nimekwama na utekelezaji wa majukumu na ninapokwenda ananambia subiri, Waziri wa Fedha mpe pesa Mhe. Waziri wa Habari akatekeleze shughuli ambazo nimemkabidhi. Sasa isingewezekana Mhe. Spika, kwamba serikali ikwame mpaka irudi ipige

magoti kwa Mhe. Raza shilingi milioni 70 kutekeleza kazi zake, hiyo isingewezekana. Kwa serikali hilo haliwezekani. Sasa kama amefanya huba ya kutoa shilingi milioni 70, hili sina tatizo nalo ni mdau wa michezo tunamheshimu sana na tutaendelea kushirikiana nae katika hilo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo katika hili Mhe. Raza ni mjumbe wa Baraza lako tukufu lakini pia ni mjumbe wa Kamati ya Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako tukufu ambalo inaisimamia Wizara yangu. Sasa kama kungelikuwa na tatizo lolote baina yeye na Wizara, Ofisi ya Waziri anaijua iko wazi sana, kwa hivyo isingependeza kwamba yeye akimbilie katika vyombo vya habari akazungumzie jambo ambalo inalihusu serikali baada ya kumuona Waziri anayehusika. Ameandika mabarua mengi nakla Ikulu, nakla Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini mimi mwenyewe kama Waziri katika suala hili hajaniandikia bado.

Sasa ninachomuomba kwamba kama ana supporting document yoyote katika suala hili basi alete serikalini taratibu za malipo zitafuata. Lakini kama hana itakuwa muhali na haiwezekani kutoa pesa ya serikali kama pipi, haiwezekani. Pesa ya serikali inatolewa kwa utaratibu maalum. Mhe. Spika, nataka niseme hilo.

Jambo jengine ambalo nataka nizungumze katika hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ni Idara ya Maafa; hii ni Idara muhimu sana Mhe. Spika, lakini mara nyingi katika utekelezaji wa shughuli zetu hasa pale ambapo maafa yanatokea tunapata matatizo ya kufika katika maeneo ya maafa kwa sababu ya ujenzi mbaya. Kwa hivyo ushauri wangu ni kwamba sisi wananchi ambao tunakaa katika mitaa mbali mbali tuhakikishe kwamba ujenzi tunaojenga ni ule ambao unaruhusu vifaa vya kuzimia moto na vyengine vya kudhibiti maafa kuweza kufikia maeneo ya matukio. Vyenginevyo wakati mwengine moto huingia katika nyumba, nyumba kwa kweli kutoka kwenye barabara mpaka kuifikia nyumba huwa mtihani mkubwa kwa sababu ya ujenzi ambao kweli unakwaza magari ya Zima Moto kufika katika eneo. Sasa hilo jambo muhimu sana Mhe. Spika, hili ni letu sote wananchi kuona kwamba aina ya ujenzi ambao tunaufanya ni ule ambao unahakikisha kwamba vifaa vya kuzimia moto vinafika.

La mwisho Mhe. Spika, naomba sana suala la maridhiano na mshikamano katika nchi yetu tuliangalie sana. Mhe. Spika, ninakuelewa sana katika jambo hili ni mdau mkubwa. Ninakumbuka ulivyokuwa ukihangaika, nakumbuka mara moja ulikuja Wete ukatwambia jamani tutakwenda hivi mpaka lini? Ulipita kila Wilaya nakumbuka. Hatua iliyofikia mwaka juzi ya kupiga kura ya maoni kuwauliza wazanzibari ilikuwa ni jambo moja muhimu sana. Katika kura ile ya maoni asilimia 66 walikubali mfumo huu, asilimia 33 ilikataa, wale tuliokubali tusidhani hata kidogo wale asilimia 33 wametulia. Tunaelewa ni maeneo yepi na yepi wakati wa upigaji kura huu wa maoni wananchi walikuwa wapi wamekubali, wapi wamekataa.

Sasa ni maeneo yale yale ambayo walikataa mfumo huu ndio chokochoko zinaanzia tena pale pale. Ni maeneo yale yale angalieni *hansard*, angalieni matokeo ya Tume ya Uchaguzi yalivyotoa ripoti ile ya asilimia 66 *against* 33 utaona maeneo yepi na chokochoko hizi tena zimeanzia wapi. Kuna watu walidhani Serikali ya Umoja wa Kitaifa haitafika mwezi, kuna wengine walidhani haitofika miezi mitatu, wengine aa haifiki mwaka. Umekatika mwaka mmoja, ina changamoto zake na ndio kawaida ya serikali hizi, aa haifiki mwaka wa pili, tumemaliza mwaka wa pili, haifiki mwaka wa tatu tumemaliza na hii ni bajeti ya nne. Tukijaaliwa tutafika ya tano, ya kumi, na ishirini tukijaaliwa.

Sasa ninawaomba sana wananchi na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nchi yetu sasa hivi inapigiwa mfano dunia nzima katika hali hii. Kwa hivyo ni vizuri kuangalia mambo yalivyokwenda, matokeo ya kura ya maoni na chokochoko ambazo zinaendelea hivi sasa kuhakikisha kwamba Umoja na Maridhiano ya Wazanzibari ni muhimu sana katika mustakbali wa uchumi na maisha yetu kwa jumla. Na kama kuna kasoro basi wenyewe tupo tutahakikisha kwamba tunawekana sawa ili ile nia nzuri ya Mhe. Spika, ambayo aliipigania sana tuhakikishe kwamba Mheshimiwa inaendelea ili kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu unakwenda mbele.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Dr. Sira umedhulumika kidogo lakini utumie dakika 11 nawe useme yale ya kusaidia hoja hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi kuweza na mimi kuchangia. Lakini kwanza Mhe. Spika, nataka niwashukuru wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara. Mhe. Spika, nimepata mitihani kipindi kifupi lakini kila mtu kwenye maziko ya mama na mdogo wangu nimeona jinsi gani walivyonibeba

katika msiba huu. Walioko Bara wameshindwa kuja kwa sababu wako kwenye Bunge lakini ni salamu, ni *massage* kiasi ambacho sikutegemea, naomba niwashukuru wote kwa njia yoyote ile walioitumia kunifariji, ahsanteni sana.

Mhe. Spika, mimi ninafikiri nianze na yanayonikera kwenye Baraza halafu nitasema na yaliyonifurahisha. Mhe. Spika, mimi ni mgeni katika hili Baraza, mwaka wangu wa kwanza au labda tuseme awamu hii ndio nimeingia. Lakini nilipoanza kuingia niliyakuta mambo mengi.

Nataka nianze kwa kusema kauli zilizotoka hapa sikupenda kauli moja kwanza kuhusu Makamu wa Pili, nilivyosema na sikupenda kwa sababu kuna viongozi na ndio viongozi wetu wa serikali wana majukumu, wana nadhari, wanakwenda kwa sababu ya taifa letu. Leo Makamu wa Pili asubuhi hapa yamesemwa mengi sikufurahi.

Nataka niseme ninachokijua mimi kuhusu safari ya Makamu wa Pili. Makamu wa Pili kenda Marekani ilikuwa tarehe 7 mpaka 19 Novemba, 2013. Ziara ya Marekani nimefuata mualiko uliotoka ACC kwa Rais wa African *Chamber of Commerce of the Pacific Northwest*, katika jimbo la Seattle. Faida ninazozijua zilizopatikana maana watu walikuwa wanataka kujua faida, ninazozijua mimi baada ya hizo *computers* 2,500 zilizosemwa ambazo zitatolewa kwa *Rotary International Club* kwa Skuli za Zanzibar, ambazo thamani ya *computers* hizo ni bilioni nne za Kitanzania. Na awamu ya kwanza *computers* hizo ni 230 tayari zimeshafika hapa. Mheshimiwa mimi naona kama safari hiyo imekuwa na faida.

Katika mkutano huo alipokuwa anafungua mgeni rasmi kulikuwa na zaidi ya wawekezaji wa kampuni 250 waliohudhuria kwenye mkutano huo wameitambua Zanzibar kwa sababu ya Balozi kuwepo pale. Na makubaliano ya mashirikiano baina ya Zanzibar na *Chamber of Commerce* na *Africa Chamber of Commerce of the Pacific Northwest* yalifikiwa. Mimi hiyo ninaiona ni faida kwa nchi yetu.

Kulikuwa na taasisi ya *Microsoft* pale ambao wajumbe wake wameshakuja Zanzibar wamekwenda kwa Makamu wa Pili mwezi Disemba, tarehe 5 na baadae mwezi wa Februari wamekuja mwaka huu, kufanya mazungumzo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamelenga katika kusaidia maeneo ya *E-government*, sekta ya elimu, *Biz Park, IT Park, Cyber Security*, vituo vya *incubator* ambayo ni *IT Business.* Kuanzishwa kwa *centre of exellency* na pia walemavu; *disability of E-government, Electronic Accessibility* ya kuwasaidia walemavu kujiajiri kwa kutumia sekta ya teknolojia. Ninafikiri faida ipo.

Si hivyo tu pale kuna tajiri wa ulimwengu Bilget na mkewe wamekusudia kutusaidia Zanzibar kwenye kilimo na elimu. Wakulima wadogo wadogo wanawake kukuza kilimo chao, kusaidia kuwapatia wanafunzi wa shule za msingi, mradi maalum wa chakula katika maskuli ya vijijini, kutuma timu ya wataalam kusaidia kituo cha utafiti kilimo Kizimbani na kusaidia kilimo cha viungo; *spices,* hiyo ni ndogo!

Isitoshe kuna *Costco* ambayo ni *Gianty Super Market Chain* ya Marekani wamekuja kuzipatia soko karafuu za Zanzibar katika maduka na kampuni, hilo dogo? Kuna *Shumake Group* wao wamekuja hapa tayari wameshakutana na ZSSF, wako mwisho wa mazungumzo, wao watashirikiana na ZSSF kujenga nyumba 250 kwa kuanzia nyumba 70 zinajengwa katika eneo la Mbweni Zanzibar. Ninaona faida ipo.

Kwa upande wangu wa afya, kuna *path* ambayo tunayo tunafanya kazi nayo lakini bado. Wametuma timu ya wataalam wao 7, wamekuja kwa ajili ya kufanya utafiti mbali mbali kwa ajili TB Unguja na Pemba, ambapo ninawajua vizuri kwa sababu mimi nimefanya kazi miaka nenda miaka rudi. Kwangu mimi hilo ni faraja kama mfanyakazi na nimefanya kazi katika kituo hiki.

Mhe. Makamo w Pili alipotoka hapo akaunganisha akapita Ras el Khaimah, alipofika huko katika mkataba wa *Scout* kule wanataka kuja kuangalia rasilimali gani iliyoko chini ya ardhi ya Zanzibar ikiwemo maji na matumizi kwa ajili ya wananchi, kelele zote zinapigwa kwa ajili ya maji hapa. Kwa hivyo watu watakunywa hatukupata faida? Lakini kutembelea maeneo huru ya Sharjah EPZ, kukutana na uongozi wa *Trans World Company* huko Jebelal Ali kuna mambo tele pale. Na mafuta yakipatikana *Rifinery* itakuwaje *Warehouse* za kuwekea *spare parts* za ndege, na hoteli atajenga na sehemu za kutunzia mizigo na matatizo yote yaliyopo jamani.

Hivi kweli baada ya hayo yote ionekane safari ya Mhe. Makamu haina faida, mumenisikitisha kama hamjui ulizeni. Lakini viongozi tunao wengi, hakuna Makamu wa Pili tu na Makamu wa Kwanza kenda safari nyingi tu. Nataka Waziri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais atakapokuja kuzungumza atueleze na sisi kenda India mara mbili,

kenda UAE, kenda Dubai, kenda Sharja, kenda Oman, kenda Qatar kenda Afrika ya Kusini, nataka nijuwe faida. Makamu wa Kwanza kama na yeye kenda kupoteza pesa kama Makamu wa Pili au katuletea namna hiyo. Hilo ni moja.

Jambo la pili ambalo sikulipenda na leo ninashukuru nimepata nafasi ya kulisema hili liko kwa CCM na liko kwa CUF, mtanisamehe ndugu zangu wa Pemba lakini leo nataka nitoe joto. Na joto nimeanza kulitoa tangu Dodoma kwa kuwakataza mnavyofanya sivyo. Mhe. Spika, simuungi mkono Mhe. Mussa, la hasha, yale ni ya kwake lakini nataka niseme ya kwangu.

Ninachotaka kukisema hivi katika aliyoyasema Mhe. Mussa ninaloliona Mhe. Mussa kwamba suala la Mapinduzi kufanyika Unguja huo ndio ukweli wala haukataliki. Ni kweli Mapinduzi yamefanyika Unguja lakini kwa nchi ya Zanzibar kwa hiyo tusilibishie kwa sababu ukweli utabaki kuwa ukweli, bomani pale ndipo yalipofanyika Mapinduzi, hayakufanyika Pemba. *(Makofi)*

Sasa mimi ninachokisema suala la Pemba kubaguliwa jamani wamelianza wenyewe na hasa waliolianzisha ni CUF. CUF ndio waliowatia watu kasumba Pemba tunaonewa sisi, tunanyanyaswa sisi. Matokeo yake hajulikani CCM hajulikani CUF, Mpemba anasimama akitaka kutoa hotuba mimi natoka Pemba, akitaka kugombea kitu mimi natoka Pemba, humu kwenye Baraza la Wawakilishi nataka Wapemba wanisute. Hata cheo kidogo tu kile kikitaka kufanywa humu kina Bi Asha Bakari, kina Bi Zainab watasimama Wapemba mbili, Waunguja mbili, hivi jaamani hata kama mtu hana uwezo nalo lile jambo wanakaa tu wanalipapatikia.

Mimi nikawauliza watu wa Bara wakianza kusema nafasi mbili zigawanywe kwa Mkoa mzima Kilimanjaro atoke kule, kweli itakuwa. Hebu tuwapeni watu wenye uwezo na ninakawaambia kuanzia leo vyeo vya Baraza hili msinihusishe na kama wanataka hapa waseme, hapa kama wenyewe hawakusema nakuachia mkutano.

Kwa hivyo tumefika mpaka Dodoma yamebaki hayo hayo niliwashambulia, nikawaambia kuanzia leo tabia hii siitaki, kila kitu mnanyanyaswa nyinyi tu, mpaka lini?

Mhe. Spika: Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni kwa mashirikiano, tuendelee kujenga mashirikiano hayo ili tufanye shughuli zetu kwa ufanisi. Nilitoa taarifa mapema wakati wa mchana kwamba kuna wajumbe watakosa nafasi na nikawaomba kwamba kama wanaweza kuandika maoni yao kwa maandishi basi apelekewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sasa kama hawakuwahi ni suala jengine lakini hilo jambo nilitoe mapema kama maelekezo ya kanuni yanavyohitaji.

Waheshimiwa Wajumbe kesho penye majaaliwa tukiingia kipindi cha asubuhi mapema tunaanza majumuisho ambapo nategemea nije kumkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na halafu mwenyewe Makamu wa Pili wa Rais amalizie. Nimeelekeza ili tupate muda mzuri, kesho maswali asubuhi hayatakuwepo kwa hivyo tunakwenda moja kwa moja katika majumuisho ili tumalize kipindi kile cha asubuhi kabla hatujaenda Ijumaa.

Basi Wajumbe baada ya machache hayo sasa ninaakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 23/05/2014 saa 3.00 barabara za asubuhi.

(1:49 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 23/05/2014 saa 3:00 asubuhi)